# Nipashe

Jumatano Mei 22, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579924

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Mpina atangaza neema ajira, kufuta tozo mifugo

UKURASA 3





HOTUBA YA WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2019/2020

UKURASA 13

# JPM aagiza mawaziri kuwa na laini za TTCL

UKURASA 2




Rais John Magufuli akipokea gawio la serikali Sh. bilioni 2.1 kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania TTCL, Waziri Kindamba (wa pili kushoto), Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Isack Kamwelwe (wa tatu kulia) na Mwenyekiti wa Bodi ya TTCL, Omar Nundu (wa pili kulia), makao makuu ya shirika hilo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Mwalimu matatani sakata la mtihani

UKURASA 3

## Wapigwa 'stop' matumizi nguvu mifuko plastiki

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA: IRINGA NGOME NGUMU KWETU** UK.31

**MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# JPM awaagiza mawaziri kutumia laini za TTCL

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli ameagiza kuorodheshwa majina ya viongozi wa serikali wakiwamo mawaziri wanaotumia mtandao wa TTCL, baada ya mwezi mmoja atafanya ukaguzi kubaini ni kiongozi gani hatumii mtandao huo.

Amemwagiza Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, Waziri Kindamba, kumworodheshea namba za mawaziri wenye laini za TTCL.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akipokea gawio la Sh. bilioni 2.1 kutoka Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), ambapo alisema ni jambo la kushangaza kuona viongozi wa serikali, na taasisi zake wanatumia laini za simu za kampuni zingine badala ya kutumia TTCL.

Alisema ni aibu kuona wizara, Ofisi ya Makamu wa Rais, ofisi ya viongozi wa kiserikali hawatumii mtandao wa simu wa serikali.

"Mimi laini yangu ni TTCL, naomba naomba niletewe orodha ya viongozi ambao wanatumia laini za TTCL, sio ziwapo tu bila kutumika, huwezi kulipwa mshahara wa serikali na hutumii mtandao huo, sijamaanisha msitumie mitandao mingine. Ofisi na mashirika ya serikali natoa wito kwenu, muanze kutumia laini za TTCL, lazima tuthamini vya kwetu," alisema na kuongeza:

"Ombi kubwa kwa Watanzania ni lazima tujali vitu vya kwetu, nitoe ombi kwa viongozi wa dini, licha ya kazi kubwa ya kuliombea taifa na kutuombea kuzishika amri za Mungu, basi mtuombee pia kuthamini vitu vya kwetu, haswa matumizi ya TTCL."

Alisema Watanzania wanapaswa kuwa wazalendo kwa kuthamini vitu vya nyumbani, na kwamba kila Mtanzania akitumia mtandao wa TTCL itafanikisha kupiga hatua ya kimaendeleo.

"Kwa nini serikali msianzishe utaratibu kwa wafanyakazi wenu, kwa anayelipiwa vocha ni lazima awe na laini ya TTCL, asiyetaka kulipiwa ajiunge na mtandao mwingine," alisema Rais Magufuli.

Alisema TTCL imeweza kuongeza idadi ya wateja kutoka milioni 1.8 mwaka jana hadi milioni 2.2 mwaka huu, idadi ambayo ni ndogo.

Alisema kwa mujibu wa Takwimu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), wananchi wanaotumia simu ni milioni 40, lakini wanaotumia mtandao wa TTCL ni milioni mbili tu.

Alisema licha ya mafanikio waliyoyapata TTCL, bado wanasafari ndefu ya kuitwa Shirika la Mawasiliano la Taifa, kwa kuwa mashirika mengine ya mawasiliano kimataifa kama vile Ethiopia, linapata faida ya Dola za Marekani bilioni 1.3 na kutoa gawio la Dola za Marekani milioni tatu.

Mwenyekiti wa Kamati wa Bunge ya Miundombinu, Se-

INAENDELEA UK 8



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella (wa tatu kushoto), akiwasha mshumaa wakati wa ibada ya kumbukumbu ya miaka 23 tangu kutokea kwa ajali ya MV Bukoba iliyosababisha vifo vya watu zaidi ya 800, iliyofanyika katika makaburi yaliyopo Igoma jijini Mwanza. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Watendaji wazuiwa kutumia nguvu msako mifuko plastiki

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imewataka watendaji na watumishi wa mkoa wa Dar es Salaam, kutotumia nguvu kuwapigana virungu wananchi watakaokutwa na mifuko ya plastiki kuanzia Juni Mosi, mwaka huu.

Aidha, amepiga marufuku watendaji watakaosimamia kazi hiyo kutoingia kwenye maduka, ofisi na kwenye magari ya watu kutafuta mizigo ya mifuko ya plastiki.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira), January Makamba, alitoa angalizo hilo jana, wakati akizungumza na watendaji wa mkoa wa Dar es Salaam, wakiwamo wakuu wa wilaya, makatibu tawala, wakurugenzi, madiwani, wenyeviti na watendaji wa kata na mitaa, wasimamizi wa masoko, maofisa afya, mazingira na biashara kujadili utekelezaji wa marufuku ya mifuko ya plastiki.

"Katika utekelezaji wa sheria hii mpya inayoanza Juni Mosi, mwaka huu, hatutegemei kuona watu wanaendelea kubeba mifuko, lakini pia hatutegemei kuona kinamama wanapigwa virungu na mgambo kisa wamebeba mifuko na wala hatutegemei kuona watu kuporwa mali zao," alisema Makamba.

Alieleza katika utekelezaji wa sheria hiyo, watendaji watakaosimamia kazi hiyo hawapaswi kuingia kwenye ofisi, maduka na kufungua magari ya watu kutafuta mizigo ya mifuko ya plastiki.

"Tunatarajia hakuna mwananchi ambaye atatumia mifuko ya plastiki kuanzia Juni Mosi, lakini watendaji wanaosimamia kazi hii, hatutarajii kuona wanapita kwenye ofisi, maduka na kufungua magari ya watu kutafuta mizigo ya mifuko hili hatulitarajii kabisa," alisema Makamba.

Alisema katika utekelezaji wa jambo hilo, mwananchi ambaye atakutwa amebeba au mfanyabiashara anayeuza mifuko ya plastiki ndiye atawajibishwa kwa mujibu wa sheria.

Kadhalika, alisema mpango huo unaenda sambamba na kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu udhibiti wa matumizi ya mifuko hiyo.

"Tutatumia muda mrefu kuendelea kuelimishana na kuelekezana kuhusu kuacha matumizi ya mifuko hii ya plastiki, hivyo utekelezaji wake hatutegemei ukitumika kuwanyanyasa watu na kupora mali zao," alisema Makamba.

Makamba alisema pia faini zitakazotozwa kwa wananchi watakaokutwa wamekiuka sheria hiyo, zitatumika katika halmashauri husika hadi hapo wizara itakapotoa mwongozo mwingine.

Alishauri maofisa mazingira kwenye mitaa husika kuwa wasimamizi wa kazi hiyo badala ya kila mtendaji kuwa mtekelezaji jambo ambalo alisema litaleta usumbufu kwa jamii.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-Tamisemi), Mwita Waitara, alisema utekelezaji wa agizo hilo utaenda sambamba na utoaji wa elimu zaidi kwa jamii.

Alisema utekelezaji wa sheria hiyo hautahusika kutumia nguvu ya vyombo vya dola isipokuwa watafanya hivyo endapo ikibidi.

Naye Mwanasheria Mkuu wa Baraza la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (Nemc), Heche Suguta, alisema utekelezaji wa sheria hiyo si kwa ajili ya kuwaonea wananchi bali kusaidia kudhibiti uharibifu wa mazingira nchini.

Hata hivyo, alisema siyo mifuko yote ya plastiki itakayozuiliwa matumizi yake, bali kuna baadhi ya vifungashio vya plastiki vitaendelea kutumika kama vile vya dawa za binadamu, pembejeo za kilimo, vya kiwandani, vya ujenzi na vya maziwa.

Hivi karibuni serikali ilipiga marufuku uzalishaji, uingizaji, usafirishaji nje ya nchi, usambazaji, uuzaji na matumizi ya mifuko aina ya plastiki, maarufu kama 'rambo', inayotumika kubebea bidhaa.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 21/05/2019.

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **ALHAMIS tarehe 23 /05/2019 kampuni ya S.S.F Co.LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **KAGERA** kuelekea MTIBWA gari hilo lenye namba za usajili:

**T 794 DFQ /T 243 DCT.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 18.50 |
| Upana | - | mita | 3.24 |
| Kimo | - | mita | 5.20 |

3. NJia itakayotumika **KAGERA hadi MTIBWA kupitia MWENDAKULIMA** gari litasafiri muda wa mchana tu(kuanzia saa **12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215241101


# Zitto ambana Lugola ubakaji wajane

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

BUNGE limemtaka Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, kwenda Kigoma kutatua changamoto ya ubakaji na ukatili dhidi ya wanawake, hasa wajane inayodaiwa kushika kasi katika mkoa huo.

Agizo hilo lilitolewa bungeni jijini Dodoma jana na Mwenyekiti wa Bunge, Najima Murtaza Giga, baada ya Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe (ACT-Wazalendo), kumbana waziri huyo kuhusu kuchukua hatua dhidi ya wanaofanya ukatili dhidi ya wanawake mkoani Kigoma.

Akiwasilisha hoja bungeni jana asubuhi, Zitto alihoji sababu za kile alichokiita kufumbia macho vitendo viovu vya uhalifu licha ya kuwa wizara kupokea taarifa kutoka kwa viongozi na wananchi.

Hata hivyo, Lugola alizitisha taasisi zisizokuwa za kiserikali zinazofanya utafiti wa masuala ya ukatili na

INAENDELEA UK 26

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, January Makamba, akizungumza na viongozi na watendaji wa mkoa wa Dar es Salaam jana, kuhusu kupiga marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki nchini. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Mpina atangaza neema 2019/20

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amesema wizara yake itaajiri watumishi wapya 295 katika mwaka ujao wa fedha.

Vilevile, amesema serikali pia imepanga kufuta tozo 10 ambazo imebaini ni kero kwa wafugaji na maendeleo ya sekta ya mifugo.

Pia, waziri huyo ametaja mambo 10 yatakayopewa kipaumbele na wizara yake katika mwaka ujao wa fedha ili kuhakikisha sekta za uvuvi na mifugo zinachangia kikamilifu katika kuifikisha nchi kwenye uchumi wa viwanda.

Akiwasilisha hotuba bungeni jijini Dodoma jana kuhusu makadirio ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Mpina alisema wizara yake itaajiri watumishi wapya 295 wakiwamo 176 wa sekta ya mifugo na 119 uvuvi na watumishi 10 watathibitishwa kazini.

Alisema wizara pia itaendelea kufanya uhakiki wa watumishi 824 na kuwezesha vikao vinne vikiwamo - viwili vya Kamati ya Ajira na viwili Baraza la Wafanyakazi.

Mpina aliongeza kuwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inafanya tathmini ili kutambua maeneo yenye upungufu na ziada ya watumishi (wageni) kwa lengo la kuwahamishia watumishi kwenye maeneo yenye uhitaji mkubwa.

**TOZO 10 KUFUTWA**

Waziri Mpina alisema kumekuwapo na mwingiliano wa majukumu, sheria, kanuni na tozo kati ya wizara hiyo na nyingine.

Alisema hali hiyo imesababisha urasimu katika utoaji vibali na leseni katika ujenzi wa viwanda na uzalishaji wa biashara.

Alibainisha kuwa utitiri wa kodi na tozo umesababisha ongezeko la gharama za uwekezaji na uendeshaji wa biashara na hivyo kuwapo kwa malalamiko makubwa kutoka kwa wawekezaji na wafanyabiashara.

Alisema utatuzi wa changamoto hizo utapunguza urasimu wa upatikanaji wa vibali, leseni, kupunguza gharama za uwekezaji na uendeshaji biashara, kuvutia uwekezaji na kupanuka kwa sekta binafsi, ajira na ukuaji wa uchumi nchini.

Waziri Mpina alisema wamepitia orodha ya tozo na ada inazotozwa na wizara yake, taasisi zake na wizara nyingine chini ya sheria mbalimbali za mifugo na kubaini baadhi ya tozo na ada hizo kuwa ni kero kwa wafugaji na maendeleo ya sekta ya mifugo kwa ujumla.

Alisema wizara imetoa mapendekezo ya kuziboresha ili kuondoa usumbufu kwa waf-

INAENDELEA UK 8

## Mkuu wa shule mbaroni tuhuma kuhonga wasimamizi mtihani

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), mkoani Ruvuma, imewafikisha Mahakama ya Wilaya ya Namtumbo Mkuu wa Shule ya Sekondari Nanungu pamoja na Mohamed Ngonyani ambaye alikuwa msimamizi mkuu wa mitihani ya kidato cha sita, Vitusi Matembo, kwa tuhuma za kuwashawishi na kutaka kuwahonga wasimamizi watano wa mtihani.

Watuhumiwa hao wanadaiwa kutaka kuwashawishi ili wawape hongo ya Sh. 100,000 ili walegeze masharti ya usimamizi wa mitihani hiyo.

Akizungumza na vyombo vya habari jana, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Ruvuma, Christina Chagaka, alisema, ofisi ya Takukuru Songea mjini ili pokea taarifa kutoka chanzo cha siri ikimtuhumu mkuu wa shule hiyo kwa makosa ya kuwashawishi wasimamizi wa mitihani katika shule hiyo, kwa kutaka kuwapatia hongo ya Sh. 100,000 ili walegeze masharti ya usimamizi wa mitihani kwa wanafunzi wa kidato cha sita wanaofanya mitihani.

Alisema, baada ya kupokea taarifa hiyo, walianza uchunguzi, na kuthibitika kuwa watuhumiwa hao wawili walishirikiana kufanya kitendo cha rushwa.

Kwa mujibu wa Lamanda Chagaka, Matembo anadaiwa alishawishika na kupokea fedha hizo ili agawane na wenzake, lakini wenzake walikataa.

Alisema watuhumiwa hao wanakabiliwa na makosa ya rushwa kinyume na kifungu cha 15 cha sheria ya kupambana na rushwa Na. 11/2007.

Alisema watuhumiwa hao wanatarajiwa kufikishwa mahakamani leo kujibu tuhuma zinazowakabili.

Aliwapongeza wasimamizi wote wa mitihani waliokataa vishawishi hivyo vya rushwa na kusimamia mitihani hiyo kwa uadilifu kama inavyotakiwa.

Alisema Baraza la Mitihani la Taifa (Necta), limekuwa likipambana na udanganyifu kwenye mitihani ya taifa ya darasa la nne, saba, kidato cha nne na sita ili kukomesha vitendo, na kwamba Takukuru ilitoa elimu kwa wasimamizi wote ili kujiepusha na madhara ya rushwa.

## Askofu wa Tanzanite afariki dunia

**Na Waandishi Wetu, ARUSHA**

MFANYABIASHARA maarufu wa madini mkoani Arusha, Thomas Mollel maarufu kama 'Askofu', amefariki dunia ghafla jijini Dodoma.

Askofu alikuwa jijini Dodoma kwa ajili ya kushuhudia kuapiswa kwa mbunge mteule wa jimbo la Arumeru Mashariki, Dk. John Pallangyo, ambaye aliapishwa jana bungeni.


Katibu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) wilaya ya Meru, Shaaban Mdoe ambaye ni miongoni mwa ujumbe wa mbunge mteule Dk. Pallangyo uliosafiri kwenda Dodoma, jana alithibitisha kutokea kwa kifo hicho.

Mdoe ambaye pia ni katibu mwenezi wa CCM mkoa wa Arusha, alisema walipokea taarifa ya kuugua kwa Askofu muda mfupi baada ya kuachana naye na kurejea katika hoteli aliyofikia baada ya wote kupata chakula cha jioni.

"Tulikuja wote juzi yeye akiwa katika gari lake binafsi na sisi katika usafiri wetu mwingine kumsindikiza mbunge mpya wa jimbo la Arumeru Mashariki, Dk. Pallangyo Bungeni tushuhudie akiapishwa leo, ambayo mwenzetu katangulia kabla ya siku hiyo,"alisema.

Alisema waliongozana naye akiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Siasa Wilaya Meru na Mei 20 majira ya saa 3:00 usiku walikuwa pamoja kwenye hotel moja jijini

INAENDELEA UK 8

# Wakazi Kidodi wachachamaa kunyanyaswa

**Na Hellen Mwango, KILOMBERO**

WAKAZI wa Kijiji cha Kidodi, wilayani Kilombero mkoani Morogoro, wameiomba serikali kumhamisha mtu waliyedai kuwasumbua wanakijiji hao na kumtuhumu kuwabugudhi wananchi kwa kuwapiga na kuwajeruhi na kuwafanya waishi maisha ya hofu kwenye nchi yao.

Aidha, wamemtuhumu kumjeruhi Mwenyekiti wa Kitongoji cha Ngwila, Extery Sanane (59) na kusababisha jicho lake kuathirika.

Wakazi hao walimtaja mtuhumiwa huyo kuwa ni Amosi Maboga maarufu kama Marekani.

Walitoa madai hayo katika mkutano wao ulioitishwa na Mkuu wa Kituo cha Polisi, Ruhembe, Mrakibu Msaidizi wa Polisi (ASP), Deogratus Mwambigili, baada ya tukio la kupigwa na kujeruhiwa kwa mwenyekiti huyo sehemu mbalimbali za mwili ikiwamo kunusurika kutolewa jicho lake la kulia.

Katika nyakati tofauti wakazi hao walimlalamikia mtuhumiwa huyo kujichukulia sheria mkononi kwa kuwapiga wananchi na kuwajeruhi bila sababu za msingi.

Malalamiko hayo waliyatoa baada ya ASP Mwambigili kutoa nafasi ya kutoa kero zao ili aweze kuzitatua.

Akitoa kero yake mmoja wa wakazi hao, Joseph Kasasa, alisema mtuhumiwa anatumia kipato chake kuwanyanyasa wananchi na kudai kuwa baadhi ya askari polisi kumlinda.

Alidai kuwa mtuhumiwa anapofanya matukio ya kupiga au kujeruhi anatumia jeshi hilo kumsweka mahabusu mlalamikaji badala ya kuchukuliwa hatua yeye (mtuhumiwa).

"Aliwahi kumpiga bibi kizee mmoja kwa sababu alipita na kuni karibu na eneo analodai ni mali yake, polisi badala ya kumkamata mtuhumiwa walimlaza mahabusu bibi huyo mpaka leo analalamika shingo


INAENDELEA UK 26



Mchuuzi wa balaghashia akisaka wateja katika eneo la Ilala Mchikichini, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**


RADIO One

POPOTE ULIPO SIKILIZA RADIO ONE KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.radioone.co.tz @RadioOneStereo @RadioOneStereo @radioonetz


# Usajili simu sasa hadi mnadani

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) zimeamua kuwafuata wananchi katika mikusanyiko kutoa elimu na kuwapatia huduma za usajili wa laini za simu kupitia mfumo wa alama za vidole.

Elimu ya usajili wa simu kwa mfumo wa alama za vidole inatolewa kwenye minada mbalimbali inayofanyika katika wilaya na mikoa. Tayari mikoa mitano ya Morogoro, Mbeya, Kigoma, Mwanza na Zanzibar imeshapata elimu na huduma hiyo.

Akizungumza katika mnada wa soko la Sabasaba Manispaa ya Morogoro ambao unafanyika kila Jumapili, Mkuu wa Huduma na Bidhaa za Mawasilino Tanzania, Thadayo Ringo, alisema hatua za kushirikisha NIDA inatokana na kiu ya wananchi ya kutaka kupata vitambulisho vya taifa ili kusajili laini zao.

"Tunakwenda katika maeneo ambayo wako wananchi tukiwa pamoja na NIDA, polisi kitengo cha kudhibiti uhalifu mitandaoni na kampuni za huduma za mawasilino. Lengo ni kuwasaidia wananchi na kutatua changamoto zao ili wanufaike na huduma za TCRA," alisema Ringo. Naye Mkuu wa Kanda ya Mashariki wa TCRA, Mhandisi Lawe Odiero, alisema wameshatoa huduma kwenye minada ya Nyandila, Mkuyuni, Dakawa na Sabasaba mkoani Morogoro na mwitikio wa watu umekuwa mkubwa.

Naye Ofisa Usajili wa NIDA, James Malimo, alisema wapo kwa ajili ya kuwasaidia wananchi jinsi ya kupata vitambulisho vya taifa baada ya kukamilisha nyaraka mbalimbali vikiwamo vyeti vya kuzaliwa.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha kudhibiti Uhalifu Mitandaoni kutoka Jeshi la Polisi Mkoa wa Morogoro, David Kamugisha, aliwataka wananchi wanaopatwa na matatizo ya kuibiwa simu na uhalifu mitandaoni kufika katika kitengo hicho ili kutoa taarifa.

# Matatani tuhuma kukutwa meno tembo ya mil. 69/-

**Na Hellen Mwango**

WATU watatu akiwamo mfanyabiashara, Godlisten Mtui na wenzake wawili wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na tuhuma za uhujumu uchumi ikiwamo kukamatwa na meno ya tembo ya thamani ya zaidi ya Sh. milioni 69.

Washtakiwa wengine ni Frank Lucas na Mhando Shomary.

Wote kwa pamoja walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Maira Kasonde.

Wakili wa Serikali Candid Nasua, Mei 7, mwaka huu, eneo la Mbezi Luis jijini Dar es Salaam, washtakiwa walikutwa na nyara hizo za serikali bila kibali.

Ilidaiwa kwamba, washtakiwa hao walikuwa eneo hilo walikutwa na vipande vinne vya meno ya tembo vyenye thamani ya Sh. 69,025,000 bila kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Shtaka lingine ilidaiwa kuwa wanadaiwa kumiliki vipande hivyo vya meno ya tembo huku wakijua vimetokana na kosa la uwindaji haramu na kwamba ni utakatishaji.

Hakimu alisema mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo na washtakiwa hao hawatakiwi kujibu chochote hadi Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP), atakavyotoa kibali.

Washtakiwa wote walirudishwa rumande hadi Juni 4, mwaka huu, kesi hiyo itakapotajwa kwa kuwa shtaka la utakatishaji linalowakabili halina dhamana.

## HABARI KITAIFA

# Wakili aomba mahakama washtakiwa warudishiwe kadi zao za benki

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa utetezi katika kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili Mkurugenzi wa uthaminishaji wa madini ya almasi na vito nchini (Tansort), Archard Kalugendo na wenzake, umeomba washtakiwa hao warudishiwe kadi zao za benki ili familia zao ziweze kujikimu.

Wakili wa utetezi Nehemia Nkoko, alitoa ombi hilo jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakati kesi hiyo ilipotajwa.

Mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, wakili huyo alidai kadi za washtakiwa hao zimeshikiliwa na polisi uwanja wa ndege, tangu walipokamatwa.

"Tunaomba washtakiwa wapewe access (haki) ya kupata mishahara yao, warudishiwe kadi zao za benki ili familia zao ziweze kujikimu na hasa tukizingatia hali ngumu ya maisha," alidai Nkoko.

Baada ya kutoa maombi hayo, hakimu alimtaka wakili huyo awasilishe ombi hilo rasmi kwa njia ya barua ili liweze kushughulikiwa.

Awali wakili wa serikali, Wankyo Symon, alidai kuwa, kesi hiyo ililetwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba faili la kesi hiyo limesharudi polisi lilipokuwa likifanyiwa upelelezi zaidi.

Alidai tarehe ijayo ya kesi, itabainika kama kesi hiyo itasikilizwa mahakamani hapo au la.

Baada ya maelezo hayo, hakimu aliahirisha kesi hiyo hadi Juni 3, mwaka huu itakapotajwa, washtakiwa wote wamerudishwa rumande.

Mshtakiwa mwingine katika kesi hiyo ni Mthamini wa Madini ya Almasi wa Serikali, Edward Rweyemamu.

Kalugendo na Rweyema ambao ni watumishi kutoka Wizara ya Madini, kwa mara ya kwanza walifikishwa mahakamani hapo, Septemba 15, 2017, wakikabiliwa na shtaka moja la kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 2.4.

Katika hati ya mashtaka, washtakiwa hao wanadaiwa kutenda kosa hilo Agosti 25 na 31, 2017 katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam na Mkoa wa Shinyanga.

Kwa pamoja wakiwa wathaminishaji wa almasi wa serikali na waajiriwa wa Wizara ya Nishati na Madini, waliisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani 1,118,291.43 ambazo ni sawa na Sh. bilioni 2.4.



Mwenyekiti wa Wakala wa Kudhibiti Ushindani nchini Kenya, Flora Mutahi (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu ushirikiano na Tanzania katika udhibiti wa bidhaa bandia zinazoingia sokoni. Katikati ni Mwenyekiti wa Tume ya Ushindani nchini (FCC), Prof. Emmanuel Mushi na Kamishna wa tume hiyo, Prof. Marcellina Chijoriga. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Mwanafunzi matatani tuhuma za kumpa mwenzake ujauzito

**Na Gurian Adolf, NKASI**

MWANAFUNZI wa kidato cha pili Shule ya Sekondari ya Kirando wilayani Nkasi mkoani Rukwa, Venance Kasolo (17), anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kumpa mimba mwanafunzi mwenzie wa kidato cha kwanza wa shule hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa makamu mkuu wa shule hiyo, Godwin Ndalama, mwanafunzi huyo alikamatwa jana asubuhi shuleni hapo na kupelekwa kituo kidogo cha Polisi Kirando kwa mahojiano.

Alisema kuwa wao kama shule hawakujua lolote juu ya ujauzito wa mwanafunzi huyo na kuwa baada ya kukamatwa uongozi wa shule ulikwenda polisi kujua ukweli wa jambo hilo.

Alisema kuwa polisi waliueleza uongozi wa shule hiyo kuwa mwanafunzi huyo anatuhumiwa kumpa mimba mwanafunzi mwenzie wa kidato cha kwanza na kuwa mahojiano yakikamilika, atapelekwa mahakamani kujibu tuhuma zitakazomkabili.

Hata hivyo, kwa mujibu wa makamu mkuu huyo wa shule, katika mahojiano na mwanafunzi huyo alikiri kumpa ujauzito mwanafunzi huyo na kudai kuwa wamekuwa wakifanya mapenzi. Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya ya Nkasi, John Lupenza, alikiri kupokea taarifa hizo na kumtaka mkuu wa shule hiyo, Eleneo Mgina, kumpelekea taarifa ya maandishi kuhusiana na tukio hilo na kuwa mkurugenzi mtendaji wa wilaya amejulishwa juu ya tukio hilo.

# Majaliwa ataka Askofu Mmole aenziwe kwa matendo yake

**Na Mwandishi Wetu, MTWARA**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa, amewataka Watanzania kumuenzi Askofu Mstaafu Gaberiel Mmole (80) wa Jimbo Katoliki Mtwara kwa wema, upole na utumishi mwema aliouonyesha wakati wote wa maisha yake.

Majaliwa alitoa wito huo jana wakati wa mazishi ya Askofu Mmole yaliyofanyika katika Kanisa Kuu la Katoliki Mtwara na kuhudhuriwa na viongozi, waumini wa kanisa hilo na wakazi wa mkoa wa Mtwara.

Ibada ya mazishi imeongozwa na Askofu Mkuu wa Jimbo la Songea, Mhashamu Askofu Damian Dallu ambaye alitumia muda huo kuwaasa Watanzania kuishi katika maadili mema na kuheshimiana.

Waziri Mkuu amesema enzi za uhai wake, Askofu Mmole alitoa kipaumbele katika masuala muhimu ya maendeleo ya jamii ikiwamo elimu na alisaidia sana watawa waliomaliza darasa la saba kujiunga na shule za sekondari.

"Hata uanzishwaji wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Stella Maris (Stemmuco) ambacho ni tawi la Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine (Saut) hapa Mtwara ni moja ya jitihada zake alizozifanya kuhakikisha anawapa elimu bora vijana na jamii.

Kifo chake ni pigo kubwa kwa Taifa kwa sababu tumepoteza kiongozi wa kiroho aliyesimamia kwa uadilifu ustawi wa jamii ya Kitanzania," alisema.

Naye Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Mhashamu Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga wa Jimbo Kuu la Mbeya alisema wamepata simanzi kubwa kufuatia kifo cha Askofu Mmole kwa kuwa walitegemea hekima zake katika baraza hilo.

Aliongeza kuwa Askofu Mmole alikuwa kielelezo cha dhamira njema na alilitumikia kanisa katika hali yoyote, hivyo yatupasa kumuombea apumzike kwa amani. Mazishi ya Askofu Mmole yalihudhuriwa na maelfu ya wananchi, maaskofu wa majimbo mbalimbali nchini, Rais mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa na mkewe Mama Anna Mkapa, na Waziri wa Nchi Ofisi ya rais R-Utumishi na Utawala Bora, George Mkuchika.


International School of Tanganyika
Challenge | Support | Inspire

**Invitation for Bids**

Bids are invited from interested registered, competent, reliable and licensed suppliers/dealers to provide the under listed goods and services for the year ending 31st July 2020.

| S/N | Category No. | Description |
|---|---|---|
| 1. | Category 01 | Maintenance Materials |
| 2. | Category 02 | Consumables and Cleaning Materials |
| 3. | Category 03 | Office Stationery |
| 4. | Category 04 | Staff Welfare Supplies (Sugar, Tea, Coffee & Milk Powder) |
| 5. | Category 05 | Timber |
| 6. | Category 06 | Supply and Servicing of Fire Extinguishers |
| 7. | Category 07 | Fumigation |
| 8. | Category 08 | Supply and Distribution of Clean Water |
| 9. | Category 09 | Cesspit Emptying |
| 10. | Category 10 | Appliances (Fridges, Cookers & Air-conditions) |
| 11. | Category 11 | Motor Vehicle Spare Parts |

**Conditions:**

- Bid document(s) will be emailed to the bidders on payment of **TZS 50,000/=** payable per bid category. Payments should be made to the Billing Department located in the Administration Building (Gate #5), off United Nations Road, Upanga, between 10.00 am to 1.00 pm Monday to Friday. Bidders will need to provide the School with their **email ID** at the time of making payment. Once payment has been received, bid documents will be emailed by the following working day.
- Bids should be emailed to **bids@istafrica.com** latest by **2 p.m. on Friday, May 31, 2019**. No bids will be accepted after this time. In addition, bidders should attach scanned copies of certificates of registration, business license, TIN/VAT certificates and User Identification Number certificate (for VAT registered suppliers). On submission of the information, the bidders would receive a confirmation that their bids have been successfully received by IST.
- The School is not bound to accept the lowest or any bid and reserves the right to reject all or any of the bids received.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Jambo jema kupaa uwazi mikataba ya manunuzi

**TAARIFA** kwamba Tanzania imeshika nafasi ya tisa kwenye uwazi wa mikataba ya manunuzi ya umma kati ya nchi 25 duniani, zinabeba ujumbe kwamba kuna jitihada zimefanyika.

Katika toleo letu la jana, tulichapisha habari zikiinukuu ripoti iliyotolewa na Shirika Lisilo la Kiserikali la Maendeleo Hivos, kwamba katika eneo la uwapo wa sheria zinazosaidia utekelezaji wa manunuzi ni asilimia 100.

Ripoti hiyo imeonyesha kuwa kwenye ufanisi wa manunuzi ya umma, Tanzania imepata asilimia 90.

Aidha, kwenye eneo la uwajibikaji Tanzania imepata asilimia 71.43, huku kwenye eneo la ushindani imepata asilimia 89.5.

Aidha, ripoti hiyo imebainisha kuwa mfumo wa kushughulikia manunuzi kielektroniki umesaidia kuwezesha utaratibu wa manunuzi kufanyika kirahisi.

Ripoti hiyo imebainisha kuwa mifumo iliyojengwa kwenye utaratibu wa manunuzi, ikiwamo kutangaza zabuni na kuwezesha wahusika kuzijaza kirahisi zaidi.

Kadhalika, kwenye eneo la kutoa zabuni Tanzania imepata asilimia 80.

Haya ni mambo ya kujivunia, na ni ishara kuwa katika suala zima la utawala bora na uwajibikaji, taasisi za serikali zimeanza kufanya vizuri sana.

Tunakumbuka huko nyuma jinsi suala la manunuzi katika wizara, idara, taasisi na wakala wa serikali zilivyokuwa zikifanya madudu katika manunuzi.

Kutokana na hali hiyo, sekta ya manunuzi ilionekana kuwa kichaka cha udanganyifu, matumizi mabaya ya fedha za umma, rushwa na ufisadi.

Mara kwa mara hali hiyo ilikuwa ikibainishwa na ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Serikali za Mitaa (LAAC).

Kimsingi, ni jambo la kufurahisha kusikia kuwa kuwa uwapo wa sheria zinazosaidia utekelezaji wa manunuzi ni asilimia 100.

Vile vile, ni jambo la kujivunia kuwa kwenye ufanisi wa manunuzi ya umma, Tanzania imepata asilimia 90 bila kusahau kwamba kwenye eneo la uwajibikaji Tanzania imepata asilimia 71.43, huku kwenye eneo la ushindani ikipata asilimia 89.5.

Kilichosababisha matokeo haya chanya bila shaka ni hatua zinazochukuliwa na serikali kwa sasa za kupambana na vitendo vya rushwa na ufisadi katika sekta ya umma.

Sekta ya manunuzi ni nyeti kwa kuwa zinatumika fedha nyingi za umma, hivyo unapokosekana udhibiti, nchi inaweza kujikuta ikipoteza fedha nyingi ambazo zingeweza kutumika kwa ajili ya maendeleo.

Kwa mfano, kuna miradi kadhaa mikubwa ambayo huko nyuma tulishuhudia iliiingiza taifa hasara kubwa kutokana na kukiukwa kwa sheria za manunuzi. Hali hiyo ilichangiwa na kukosekana sheria madhubuti za manunuzi pamoja na udhibiti wa sekta ya manunuzi.


Kwa hiyo hatua za serikali za kuziba mianya ya rushwa na ufisadi imechangia kwa kiwango kikubwa katika mafanikio haya, hususan udhibiti katika manunuzi ya umma.

Mbali na kupongeza hatua zilizochukuliwa, tunaishauri serikali iendelee kuweka udhibiti katika manunuzi ya umma ikiwamo kuhakikisha kwamba kunakuwapo na uwazi.

Pale inapoonekana kuwa baadhi ya sheria zina udhaifu, basi ziboreshwe na wakati mwingine kutungwa mpya, kwa lengo la kuhakikisha kuwa sekta ya manunuzi haitumiki kama kichaka cha kuhujumu uchumi wa taifa letu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Marufuku mifuko ya plastiki jamii isome ishara za nyakati

Na Sabato Kasika

MWISHO wa matumizi ya mifuko ya plastiki ni Juni Mosi mwaka huu, na serikali imeshatangaza kuwa haitarudi nyuma katika hilo na kuwataka watu wote kuzingatia tarehe hiyo.

Hata hivyo, kumekuwapo na upotoshaji wa mitaani ambapo baadhi ya watu wamekuwa wakijifariji kuwa ni masuala ya kisiasa tu na kwamba mifuko hiyo itaendelea kuuzwa kama kawaida.

Watu wa aina hiyo wanapaswa kupuuzwa kwani wanaweza kusababisha wenzao wakaingia kwenye matatizo kwa kutozwa faini watakapokutwa na mifuko hiyo, baada ya muda ulioweka kumalizika.

Msimamo wa serikali ni kwamba haina mpango wa kuongeza muda kwa wamiliki wa viwanda vinavyozalisha mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku, hilo ndilo jambo la msingi la kuzingatia.

Ni vyema watu wakasoma ishara za nyakati na kutambua kwamba serikali hii hailembi, kwa kuwa ikishaamua, kinachofuata ni utekelezaji tu, hivyo ni muhimu Watanzania kuzingatia hilo.

Itashangaza iwapo Juni 2 mwaka huu kutakuwa na watu ambao watakutwa na mifuko hiyo, wakiamini kwamba serikali imetangaza na kisha italegeza msimamo au itaongeza muda.

Siyo vyema kukumbana na hali hiyo kwasababu tu ya uzembe na hasa kwa kuzingatia kwamba zimebaki siku chache ule muda uliowekwa na serikali wa kupiga marufuku mifuko hiyo utumie.

Yale ambayo yamekuwa yakiwakuta baadhi ya watu kwa uzembe wa kutozingatia muda, hayapaswi kufanywa kwenye suala hili la marufuku ya mifuko ya plastiki ambalo lina faini yake.

Kwa mfano wakati uandikishaji wa vitambulisho vya taifa unaanza, baadhi walikosa, kutokana na mtindo wao wa kusubiri hadi siku ya mwisho na kukuta msururu mrefu wa watu na hivyo wakakwama kuhudumiwa.

Siyo vitambulisho tu bali hata kuhama kwenda kwenye televisheni za ving'amuzi, wengine walizembea na kushindwa kubadilisha zao kwa wakati na kujikuta zikizimwa.

Mimi ninaamini kwamba mtu atakayekutwa na mifuko hiyo kuanzia Juni 2 mwaka huu, basi atakuwa ni mzembe au atakuwa miongoni mwa wale wanaosikiliza maneno ya mitaani.

> **Msimamo wa serikali ni kwamba haina mpango wa kuongeza muda kwa wamiliki wa viwanda vinavyozalisha mifuko ya plastiki iliyopigwa mafuruku, hilo ndilo jambo la msingi la kuzingatia.**

Wakumbuke kuwa kwa sasa kuna matangazo ya mara kwa mara kwenye vyombo vya habari na hata ujumbe unaotumwa katika simu ukisisitiza kwamba mifuko hiyo ni marufuku ifikapo Juni Mosi.

Kwa maana hiyo sidhani kuna mtu atakayejitetea kwamba hajui marufuku hiyo, kwani atakuwa hana ujanja wa kujitetea, kwa sababu kumekuwapo na njia nyingi za kufikisha ujumbe kuhusu suala hilo.

Kama hana TV, redio au simu, basi atakuwa amepata ujumbe kupitia kwa ndugu, rafiki au jirani, vinginevyo atakuwa ni miongoni mwa wale wanaosubiri hadi dakika ya mwisho ili 'waibipu' serikali.

Kila mmoja aepuke kutozwa faini ambayo imetangazwa kuwa ni Sh. 30,000 kwa yule atakayekutwa akitumia mifuko hiyo baada ya kumalizika kwa muda uliowekwa na serikali.

Wakati serikali ikiweka faini hiyo, Baraza la Madiwani Manispaa ya Moshi limepitisha sheria ndogo itakayodhibiti mifuko hiyo.

Kwamba kwa wale watakaokamatwa nayo, watalipa faini ya Sh. 50,000.

Bado wapo wafanyabiashara wa maduka ya jumla na rejareja, ambao wanataka jamii ipewe elimu kuhusu mifuko hiyo, lakini sidhani kama haijawahi kutolewa tangu serikali ilipotangaza marufuku miaka kadhaa iliyopita.

Nakumbuka siyo mara ya kwanza serikali kupiga marufuku mifuko hiyo, kwani miaka kadhaa iliyopita ilifanya hivyo lakini ikawa inaishia njiani na sasa imeamua kufanya kweli na ndio maana kumekuwapo na matangazo ya mara kwa mara yakisisitiza kuwa Juni Mosi ni mwisho.

Hatua hivyo inatosha kuwafanya Watanzania wajue kuwa imedhamiria kukomesha mifuko hiyo nchini, na kinachotakiwa ni jamii kutii.

MAKALA

# Nuru mpya sekta mifugo, uvuvi

## • Makusanyo yote yavuka lengo



Shughuli zikiendelea katika Soko la Samaki Feri, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA.**

**Na John Mapepele**

LEO, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, anahitimisha Mapendekezo ya Bajeti ya Wizara yake bungeni kwa mwaka ujao wa fedha, 2019/20. Hiyo ni hotuba yake ya pili ya bajeti tangu alipokabidhiwa wizara hiyo, akiwa na Naibu wake, Abdallah Ulega.

Ni hotuba iliyosheheni ripoti za mafanikio makubwa, baada mikakati iliyotekelezwa katika kipindi kilichopo, yaani Julai 2018 hadi sasa, Mei 2019. Baadhi ya mafanikio hayo makubwa, yamo katika sekta ya Uvuvi.

Anasema kwa mara ya kwanza katika kipindi cha zaidi ya miaka 40, wizara imeifumua Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009 na kuzaliwa; Sheria ya Uvuvi na Sheria ya Ukuzaji Viumbe Maji.

Anaongeza, katika mwaka 2018/2019, wizara imefanya marekebisho ya dharura kwa baadhi ya Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009, kuliwezesha Taifa kunufaika na rasilimali uvuvi.

Hayo yanajumuisha: Kuruhusu matumizi ya nyavu milimita nane, badala ya kumi 10 kwa uvuvi wa dagaa katika ukanda wa bahari; matumizi ya nyavu za makila zenye ukubwa wa macho ya kuanzia inchi saba, badala ya inchi sita.

Mengine ni: Uvunaji wa Kaa kutoka gramu 500 hadi gramu 450; Kuondoa Ukomo wa Urefu wa Sentimita 85 kwa samaki aina ya Sangara; na Matumizi ya Leseni Moja kwa kila eneo la Maji ya Uvuvi, badala ya kila halmashauri kutoa leseni yake. Marekebisho hayo ni ya Mei 10 ya mwaka 2019

Marekebisho hayo yatarajiwa kuwezesha wananchi wa Ukanda wa Pwani kuvua dagaa mchele kwa kutumia nyavu za milimita nane, waliokuwa hawawezi kuvuliwa kwa kutumia nyavu za milimita 10 zilizokuwepo kwa mujibu wa Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009.

Pia, inahusu kuwezesha kuvua samaki sangara wenye urefu zaidi ya sentimita 85 na kuondoa ukataji leseni, ikiwa na manufaa ya kuongeza kipato cha wavuvi, malighafi ya viwanda, kuvutia uwekezaji mpya, kudhibiti utoroshaji mazao ya uvuvi na kuongeza mapato ya serikali.

**MAGEUZI ZIWA VICTORIA**

Kuhusu kuongezeka samaki wa Ziwa Victoria, Waziri anasema kwa kutumia teknolojia iitwayo'Hydro-acoustic survey' Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), kwa kushirikiana na Taasisi za Kenya Marine and Fisheries Research Institute (KMFRI-Kenya ) na National Fisheries Resources Research Institute (NaFIRRI-Uganda), zilifanya utafiti kati ya mwezi Septemba hadi Oktoba, mwaka jana na kubaini kuwapo tani 2,210,000 za aina mbalimbali za samaki.

Ni utafiti ulioonyesha mafanikio: Sangara walioongezeka kutoka tani 417,936 mwaka 2016 hadi kufikia tani 553,770 mwaka 2018.

Pia, sangara wa chini ya sentimita 50 wamepungua kutoka asilimia 96.6 mwaka 2017 hadi asilimia 62.8 mwaka jana; sangara kuanzia sentimita 50 hadi 85, wameongezeka kutoka asilimia 3.3 mwaka 2017 hadi asilimia 32.0 mwaka jana.

Samaki aina hiyo wenye urefu unaozidi sentimenta 85, wameongezeka kutoka asilimia 0.4 mwaka 2017 hadi asilimia 5.2 mwaka 2018, huku wastani wa urefu wa sangara umeongezeka kutoka sentimeta 16 mwaka 2017 hadi kufikia sentimeta 25.2 mwaka jana.

**VIWANDA SAMAKI**

Takwimu zinaonyesha katika mwaka wa fedha unaoisha, kuna viwanda vikubwa 12 vilichakata mazao yenye viwango vya kuuzwa katika soko la nje, hususan Umoja wa Ulaya (EU), vikiwemo viwanda vinane vya Ziwa Victoria na vinne Ukanda wa Pwani.

Vilevile, viwanda vya kati vinne vilichakata mazao ya uvuvi yaliyouzwa katika soko la kikanda nchi zingine, zikiwemo Bara Asia na Marekani; na kuna viwanda vidogo 34 vya kupokea samaki hai na maghala 52 kwa ajili ya mazao ya uvuvi yaliyokaushwa.

Kwa mujibu wa Waziri Mpina, doria na operesheni zinazoendelea nchini, zimeongeza upatikanaji wa samaki hususan sangara, kuimarika viwanda na kuongeza uzalishaji. Hivi sasa, kuna wastani wa tani 180 zinazochakatwa kwa siku, ikilinganishwa na tani 165 katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Kingine anachokitaja ni hadi Machi mwaka huu, jumla ya tani 389,459.40 za samaki zenye thamani ya Sh.trilioni 1.83 zilivunwa, ikilinganishwa na tani 376,352.72 zenye thamani ya Sh. trilioni 1.77 zilizovunwa katika kipindi kama hiki mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia tatu.

Katibu Mkuu

Katibu Mkuu wa wizara hiyo yenye dhamana na uvuvi, Dk. Rashid Tamatama, anasema udhibiti wa rasilimali za uvuvi, wizara imeanzisha kanda kuu tatu za usimamizi na udhibiti wa rasimali za uvuvi: Ziwa Victoria; Tanganyika; na Ukanda wa Pwani.

Dk. Tamatama anasema, wizara imeanzisha kanda ndogo mbili ambazo ni Ukerewe na Sengerema na imeimarisha vituo 27 vya kusimamia rasilimali za uvuvi nchini.

Anasema, wizara ilifanya 'Operesheni Sangara' katika maziwa yote makubwa nchini na ikafanikiwa kukamata zana haramu mbalimbali, zikiwemo nyavu za makila (168,708); makokoro (3,715); na nyavu za timba (15,915); nyavu za dagaa (9,068); na kamba za kokoro zenye urefu wa mita 525,784; ndoano (568,958); mitumbwi/boti 2,291.

Katibu Mkuu anataja operesheni hiyo ilikamatwa samaki wazazi kilo 8,958; wachanga/kayabo kilo 110,181p; na mabondo kilo 634.01.

Anasema kulikuwapo watuhumiwa 4,713 wanaojumuishwa na viongozi 17 kati yao, waliotumia magari 4,489, pikipiki 374 na mitungi ya gesi 236 kufaikisha azma yao.

**UHARAMIA KIMATAIFA**

Dk. Tamatama anasema, walikamata tani 15.53 za samaki walioingizwa nchini bila nyaraka, leseni na vibali. Hao walipatikana kuwa na viambata vya sumu, baada ya kufanyiwa uchunguzi na wote waliteketezwa kwa kutokukidhi viwango vya ubora na usalama.

Hiyo iliendana na raia wa kigeni 203 walikamatwa wakijihusisha na uvuvi na biashara za mazao ya uvuvi kinyume cha sheria.

Katika mwaka 2018/2019, kuna vifaranga 17,301,076 (samaki 6,221,076 na kambamiti 11,080,000) vimezalishwa katika vituo vya serikali na sekta binafsi ikilinganishwa na vifaranga 15,119,757 vilivyozalishwa mwaka 2017/2018.

Pia, mabwawa ya samaki yameongezeka kutoka 24,302 katika mwaka 2017/2018 hadi 26,445 wa sasa. Wizara inaendelea kuhamasisha uwekezaji na matumizi ya teknolojia stahiki kuzalishia viumbe maji.

Hiyo inahusu matumizi ya vizimba (fish cage), hadi sasa kuna vizimba 408, kwa mgawannyiko: Ziwa Victoria (346); Ziwa Tanganyika (9); na malambo (53).

**MAKUSANYO**

Waziri Mpina anasema kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Uvuvi ilitarajia kukusanya Sh. 21,534,305,600.00. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 kiasi cha Sh. 30,330,063,743.25 sawa na asilimia 140.8 ya lengo zilikusanywa kutoka Sekta ya Uvuvi.

Katika mifugo, anasema katika mwaka huo wa fedha, Wizara ilitarajia kukusanya Sh. 18,467,945,100. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 kiasi cha Sh. 33,853,050,919 kilikusanywa kutoka Sekta ya Mifugo, sawa na asilimia 183.31 ya lengo.

Ongezeko linatokana na wizara kuimarisha udhibiti wa upotevu wa mapato, pamoja na marekebisho katika ada na tozo katika Sekta ya Mifugo.

Katika bajeti ijayo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inaomba Bunge, kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sh. 64,901,756,551. Ipo katika mgawanyo; Sekta Mifugo Sh. 31,774,378,000; Sekta Uvuvi, Sh.33,127,378,551.00.

*• Mwandishi wa makala hii ni Katibu wa Waziri wa Mifugo na Uvuvi anapatikana kwa mawasiliano ya baruapepe; jmapepele1@gmail.com au simu (+255) 0784441180.*

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



# JPM awaagiza mawaziri kutumia laini za TTCL

INATOKA UK 2

lemani Kakoso, alisema TTCL inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo kuzidai taasisi nyingi za serikali zaidi ya Sh. bilioni 28, pamoja na madai ya fedha kutokana na Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa.

Naye Msajili wa Hazina, Dk. Athumani Mbuttuka, alisema kwa kipindi cha miezi mitatu gawio limeongezeka kutoka Sh. bilioni 119.2 kwa mwaka 2015/16 hadi Sh. bilioni 339 kwa mwaka 2017/18.

AGIZO KUTOA GAWIO

Pia Magufuli aliyaagiza mashirika na taasisi za serikali 253 zilipo kisheria kuhakikisha zinatoa gawio kwa serikali ifikapo Julai mwaka huu, vinginevyo watachukulia sheria kali, ikiwamo kufutwa.

Alimwagiza Msajili wa Hazina, Dk. Athumani Mbuttuka, kuyaandikia barua mashirika na taasisi hizo kuhusu agizo hilo, na nakala kwenda kwa Katibu Kiongozi.

Aliyataka mashirika na taasisi zingine za serikali yenye wajibu kisheria wa kutoa gawio kufanya hivyo haraka.

"Mashirika ambayo yanapaswa kutoa gawio nayaagiza ifikapo Julai mwaka huu yawe yameshatoa, vinginevyo tutatumia sheria ikiwezekana kuyafuta, haiwezekani shirika kila mwaka liwe linapata hasara lakini halifungwi," alisema na kuongeza.

"Msajili wa hazina yaandikie barua mashirika hayo yote na nakala iende kwa Katibu Kiongozi, haiwezekani taasisi kama Jeshi la Wananchi linatoa gawio halafu mengine yasitoe," alisema Rais Magufuli.

Rais Magufuli alisema fedha za gawio ndizo zinatumika kujenga shule, hospitali, miundombinu ya barabara, na huduma zingine za kijamii nchini.

Alisema kwa mwaka 2017/18 ni mashirika 40 tu yaliyotoa gawio kwa serikali yenye thamani ya Sh. bilioni 717.56, hivyo kwa mwaka 2018/19 anatarajia idadi ya mashirika itaongezeka.

Kadhalika, Rais Magufuli aliutaka uongozi wa TTCL kuhakikisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unafika katika maeneo yote nchini, ambapo kwa sasa kati ya wilaya 149 ni wilaya 40 tu zilizofikiwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Aidha, aliitaka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhakikisha inaisaidia TTCL katika kupata minara yake, na kuacha tabia ya kukodi minara ya kampuni zingine za simu.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, Waziri Kindamba alisema sababu iliyochochea kupatikana kwa gawio hilo ni ongezeko la mapato kutoka Sh. bilioni 119 hadi 167.

"Kwa kipindi cha miaka mitatu tumeweza kuboresha vituo vya wateja, tumeongeza uwezo wa teknolojia na miundombinu, tumeendelea kuwa wasimamizi wa Mkongo wa Taifa na Kituo cha Taarifa," alisema Kindamba.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya TTCL, Omary Nundu, alisema endapo TTCL ikiwezeshwa inaweza kutoa gawio kubwa zaidi ya hilo walilotoa.



Mwenyekiti wa Bunge, Najma Giga; Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa Tanzania, Godfrey Mungereza; Mbunge wa Bahi, Omar Badwel; Mbunge wa Chemba, Juma Nkamia; Mbunge wa Mpwapwa, George Lubeleje; Mbunge wa Viti Maalum Dodoma, Fatma Taufiq, Raisi wa Shirikisho la Sanaa Tafca pamoja na wawakilishi wa Kampuni ya Data vision International wakiwa kwenye uzinduzi wa semina ya mafunzo yaliyo andaliwa na Tacip jijini Dodoma juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Mpina atangaza neema 2019/20

INATOKA UK 3

ugaji katika mwaka ujao wa fedha na hivyo kuongeza mapato katika sekta ya mifugo na kutoa huduma za mifugo kwa wafugaji.

"Jumla ya tozo 10 zimependekezwa kufutwa ikiwa ni pamoja na tozo nne za maziwa, tano za nyama na moja ya kuku," Mpina alisema.

Tozo zilizopendekezwa kufutwa ni pamoja na vibali vya vyombo vya kusafirisha maziwa chini ya lita 51, usajili wa vituo vya kukusanya maziwa chini ya lita 201, usajili wa wazalishaji maziwa chini ya lita 51, usajili wa wasambazaji wa pembejeo za maziwa na usajili wa wafugaji wa mifugo ya nyama wadogo, wa kati na wakubwa.

Tozo zingine zilizopendekezwa kufutwa ni usajili wa wasimamizi wa minada ya awali, upili na mpakani, usajili wa minada ya awali, upili na mpakani, vibali vya kusafirisha kuku ndani ya nchi, usajili wa wafanyabiashara wa mifugo katika minada ya awali, upili na mpakani na usajili wa wafanyabiashara wa nyama na bidhaa za nje ya nchi.

**VIPAUMBELE 10**

Mpina alitaja maeneo 10 ambayo wizara yake imepanga kuyatilia mkazo kwa kushirikiana na wadau kuwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi, udhibiti na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na kutunza mazingira.

Alisema vipaumbele vingine ni kudhibiti upotevu wa mapato ya serikali yatokanayo na sekta ya uvuvi, kuimarisha usimamizi wa rasilimali katika ukanda wa uchumi wa bahari na bahari kuu na kuimarisha usimamizi na udhibiti wa ubora, usalama na viwango vya samaki na mazao ya uvuvi.

Vinginevyo ni kuimarisha miundombinu na kukuza biashara ya mazao ya uvuvi, kuboresha upatikanaji wa taarifa sahihi za uvuvi na kuboresha upatikanaji wa taarifa sahihi za uvuvi. Waziri Mpina alisema wizara yake pia itaongeza upatikanaji wa vifaranga vya samaki, kuandaa kanda za ufugaji wa samaki na kuimarisha utafiti wa huduma za ugani na mafunzo ya uvuvi.

Ili kutekeleza majukumu yake, Mpina aliliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 64.9 kwa ajili ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha. Kati yake, Sh. bilioni 31.7 ni kwa ajili ya sekta ya mifugo na Sh. bilioni 33.2 kwa ajili ya sekta ya uvuvi.

**MAONI YA UPINZANI**

Akiwasilisha hotuba yake bungeni jana kuhusu makadirio ya bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka ujao wa fedha, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi katika wizara hiyo, Dk. Sware Semesi, alibainisha mambo nane muhimu yanayopaswa kufanyiwa kazi na serikali kwa maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi.

Aliyataja mambo hayo kuwa ni pamoja na kuimarisha utafiti katika kupata mbegu na vyakula bora na utengenezaji wa vifaa vya uvuvi, ujenzi wa bandari za uvuvi na bandari kavu.

Dk. Sware alisema jambo la pili ni serikali kuweka mikakati mapema ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya nchi badala ya kusubiri hadi kutokee janga la usalama wa chakula.

Upinzani pia ulishauri kuwapo na uwekezaji mahususi kwa wajasiriamali wa uvuvi hasa katika ufugaji wa samaki, kaa, lulu, ukulima wa mwani na uzalishaji wa vyakula, mbegu na vifaranga vya samaki.

Dk. Sware alisema jambo la nne ambalo upinzani unaishuri serikali ni kuweka mazingira rafiki ili kuwekeza zaidi katika ufugaji wa samaki kwenye vizimba vya maziwa na mwambao wa bahari. Waziri kivuli huyo alisema jambo lingine linalopaswa kufanyiwa kazi na serikali ni kufanya upya tathmini ya kodi, tozo na ushuru mbalimbali katika sekta hizo mbili, akitolea mfano kuondoa tozo ya asilimia 10 kwa usafirishaji wa ngozi.

Alisema serikali pia inapaswa kuwekeza katika uzalishaji zaidi wa samaki ili kukabiliana na changamoto ya kuagiza samaki toka nje kwa fedha za kigeni kunakosababisha kupungua kwa akiba ya fedha za kigeni nchini.

"Serikali itafute suluhisho la kudumu kuhusu nyavu za kuvulia na kutafuta njia mbadala ambazo ni rafiki kwa mazingira katika kuteketeza nyavu haramu za uvuvi," alisema.

Dk. Sware aliongeza: "Ni bora serikali ikapitia sera ya Chadema kuhusu sekta ya uvuvi ili kubuni na kuboresha shughuli za biashara za masuala ya uvuvi ambazo zitalenga kuhakikisha kuna usambazaji wa kutosha wa samaki na bidhaa nyingine za baharini kwa ajili ya matumizi ya wananchi na viwanda."

# Askofu wa Tanzanite afariki dunia

INATOKA UK 3

humo walikula chakula pamoja akiwa hana shida yeyote.

"Tulikaa pale na aliagiza soda Club Soda tu na alipomaliza saa nne usiku huo aliondoka na kwenda hoteli alipofikia lakini kufika saa tano usiku nilipokea simu toka kwa Mwenyekiti wa wazazi wilayani kwangu, akinitaarifu Askofu ameanguka hotelini anakimbizwa hospitalini," alisema.

"Tulipigiwa simu na mkewe kwamba amezidiwa baada ya kuteleza akitoka kuoga, lakini tulipofika hospitali Mkoa wa Dodoma muda mfupi baadaye tulijulishwa kwamba amefariki," alisema Mdoe. Askofu alikuwa miongoni mwa wachimbaji wachache wa madini waliofanikiwa na akaendelea kuishi katika kijiji alichozaliwa cha Mbuguni wilayani Arumeru, kilometa chache kutoka ilipo migodi ya madini ya Tanzanite katika eneo la Mirerani.

Alikuwa mjumbe wa kamati ya siasa ya CCM Wilaya ya Meru na pia mjumbe wa Halmashauri kuu ya CCM katika wilaya hiyo. Kati ya mwaka 2010 na 2015 alikuwa diwani wa kata ya Mbuguni Askofu atakumbukwa zaidi kwa tukio la mwaka 1995 baada ya kupata madini ya Tanzanite aligawa fedha kwa kuzirusha akiwa ghorofani katika jengo lake la Hoteli ya Pallsons iliyopo katikati ya Jiji la Arusha.

Akizungumzia kifo hicho, mchimbaji wa madini ya Tanzanite huko Mererani, Rahim Massawe, alisema kimewagusa wengi kwa kuwa alisaidia watu wengi kufanikiwa kuingia kwenye uchimbaji wa madini.

Mbali na kuwa mchimbaji wa madini na mwanasiasa, Askofu pia alikuwa mwana michezo ambaye alifanikiwa kuanzisha timu ya soka ya Pallson iliyofanikiwa kucheza ligi kuu ya soka ikiwa na makazi yake katika kijiji cha Mbuguni. Afisa habari wa shirikisho la wachimbaji wa Madini nchini (Femata), Dk. Bernard Joseph alisema wachimbaji wamempoteza rafiki, mpambanaji na mtu muhimu kwenye sekta hiyo.

"Wakati wa uhai wake alikuwa na mapenzi mema na vijana kwani alianzisha timu ya mpira wa miguu ya Pallsons ambayo ilifikia hatua kubwa kwenye soka," alisema Dk. Joseph.

Naye, mmiliki wa mgodi wa madini ya Tanzanite, Fatuma Kikuyu, alisema wachimbaji madini wamepata pigo kubwa kwani Mollel alikuwa anasaidia wachimbaji wenzake ambao hawakuzalisha madini.

Alisema ni pengo kubwa wamepata wachimbaji madini ya Tanzanite kwani watu kama Mollel wapo wachache kutokana na kuwajali wachimbaji wenzao.

Mchimbaji wa madini ya Tanzanite, Haji Msham Ngokwe, alisema sekta ya madini imepoteza mtu muhimu kwani Mollel ni miongoni mwa matajiri wa mwanzo mwanzo kupata madini ya Tanzanite.

"Huyu alikuwa na roho nzuri hadi watu wakamuita Askofu badala ya Mollel. Alisababisha wengine waione Sh.milioni moja kutokana na kuwa na roho ya utoaji," alisema Ngokwe.

***Imeandikwa na Novatus Makunga na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA***

HABARI KITAIFA

# Ndugu wa mtoto majeruhi wapatikana

Na Beatrice Moses

HATIMAYE ndugu na baba mzazi wa mtoto aliyekuwa amelazwa katika Hospitali ya Rufani ya jijini Mbeya, baada ya kunusurika kwenye ajali ya pikipiki iliyoua mama yake mzazi wamepatikana.

Watu kadhaa waligubikwa na huzuni, huku wengine wakiandika maneno ya kumuombea kwa Mungu, baada ya kusoma ujumbe uliotumwa juzi mitandao ya jamii na hospitali hiyo ambao uliambatanishwa na picha ya mtoto huyo akiwa amelala kitandani hospitalini hapo, huku ikibainishwa kuwatafuta ndugu zake.

"Huyu mtoto yuko hospitali ya rufani mjini wodi namba 8, ni mtoto wa mama aliyegonjwa Alhamisi ya Mei 17, 2019 na kufariki katika mteremko wa Iwambi kuelekea Mbalizi, hakuna aliyejitokeza kumchukua... tunaomba share kwenye makundi mengine ili ndugu wa karibu wamchukue," ilielezwa katika ujumbe huo ambao iliwekwa na namba ya simu ya msimamizi wa hospitali hiyo kwa mawasiliano na ndugu husika.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alithibitisha kupatikana kwa ndugu wa mtoto huyo, akibainisha pia wamekwenda kuutambua mwili wa ndugu yao, aliyetambulika kwa jina la Victoria Anthony, aliyekuwa akiishi Mbalizi jijini Mbeya.

"Baba yake amejitokeza jina lake kwa hapa sina, ila baada ya kukamilisha taratibu husika atakabidhiwa mtoto wake," alisema Kamanda Mtei.

Imeelezwa kuwa katika ajali hiyo licha ya kifo cha mama huyo, dereva aliyekuwa akiendesha pikipiki hiyo naye alikufa.

Msemaji wa Hospitali hiyo, Acard Mosha, alisema mtoto huyo alifikishwa baada ya kupewa rufani kutoka katika Hospitali ya Isisi Mbeya kwa matibabu, ambapo pia mwili wa mama yake ulihifadhiwa.

"Baada ya kumpokea alikuwa na majeraha kiasi katika mwili wake, madaktari walimchunguza na kumpatia matibabu anayostahili, kwa sasa anaendelea vizuri kabisa," alisema Mosha.

Pia alisema uongozi wa hospitali hiyo licha ya kutangaza kutafuta ndugu wa mtoto huyo, wapo makini kuhakikisha usalama wake, hivyo watakabidhi kwa wale watakaothibitishwa na polisi kuwa ni ndugu halisi na siyo vinginevyo.




Ofisa huduma kwa wateja wa kampuni ya Tigo, Pendo Stephen (kushoto), akimsajilia laini ya simu mmoja wa wateja ambaye ni mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani, jijini Dar es Salaam jana, kwa kutumia utaratibu mpya wa usajili kwa alama za vidole. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kikosikazi kukabiliana na ukatili Dar

Na Sabato Kasika

BAADHI ya mashirika ya kiraia jijini Dar es Salaam yameunda kikosikazi ambacho kitakuwa na jukumu la kukabiliana na ukatili wa kijinsia kwa makundi yaliyo pembezoni.

Mwenyekiti wa asasi ya kiraia ya Mpakani Tunaweza, Assia Khalifa, aliliambia gazeti hili kuwa kikosikazi hicho kiliundwa juzi katika mkutano maalum ulioshirikisha mashirika kadhaa ya kiraia.

Alisema asasi yake ndio iliyoratibu mkutano huo ulioshirikisha mashirika ya Zawode, Huba Foundation na Toto's ambayo ni yanaunda Mtandao wa Tanzania Women Coalition.

Mwenyekiti huyo alisema mashirika hayo yanaendesha mradi wa kuzuia ukatili wa kijinsia kwa makundi yaliyo pembezoni kwa ufadhili wa OSIEA, na kwamba yamefikia hatua hiyo ili kusaidia na serikali kupambana na ukatili.

Alisema kikosikazi hicho kilichoundwa kinahusisha watu watatu kutoka katika kila wilaya nne za Temeke, Ubungo, Kinondoni na Ilala, jijini Dar es Salaam.

"Kikosikazi hicho kitashirikisha waratibu wa maofisa maendeleo ya jamii na waratibu wa Ukimwi wa manispaa husika ili kuhakikisha vitendo hivyo vinakomeshwa ndani ya jamii," alisema Assia.

Alisema kila baada ya ziara ya kutembelea waathirika watakuwa wanaketi na kuchambua taarifa na kisha wataweka mikakati na kutafuta jinsi ya kuitekeleza ili kuwasaidia waathirika wa ukatili wa kijinsia.

"Kwa kuanzia wamepanga kutembelea waathirika wa matukio ya ukatili waliopo katika maeneo yao ili kujua changamoto zinazowakabili na namna zinavyoweza kutatuliwa kwa kutumia rasilimali zilizopo," alisema.

Alisema jukumu la kukabiliana na vitendo vya ukatili na Watanzania wote, siyo la serikali pekee yake, ndio maana wameamua kuunda kikosikazi hicho ili kiweze kutoa mchango katika kazi hiyo.

## Mradi Tacip wazinduliwa

Na Paul Mabeja, DODOMA

MRADI wa utambuzi wa wasanii wa sanaa za ufundi Tanzania ujulikanao kama Tacip umezinduliwa rasmi katika Wilaya ya Dodoma Mjini, huku ukiungwa mkono na wabunge wa Mkoa wa Dodoma.

Wabunge hao wakiambatana na Rais wa Shirikisho la Sanaa za Ufundi Tanzania (TAFCA), Adrian Nyangamalle, pamoja na Mtendaji wa Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA), Godfrey Mungereza.

Akimwakilisha Spika wa Bunge, Mwenyekiti wa Bunge, Najma Giga, alisema: "Tumeupokea mradi huu wa Tacip kwa faraja kubwa katika jiji letu na makao makuu ya nchi, ni jambo jema kwamba mradi huu uliobuniwa na Kampuni ya DataVision International ikishirikiana na Shirikisho la Sanaa za Ufundi nchini chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kupitia Basata unadhamira ya kuwajengea mazingira wezeshi wasanii wa sanaa za ufundi kutumia ujuzi na ubunifu wao kujikwamua na umaskini, huku wakiongeza mchango katika pato la taifa."

"Hivyo natoa wito kwa serikali mkoa wa Dodoma kuwapa ushirikiano wa kutosha kwa kusaidia katika kutoa wito kwa jamii na hata katika kutatua changamoto watakazokutanazo wakifanya shughuli zao jijini hapa," aliongeza Giga.

Naye Mratibu wa TACIP, Sauli Mpocke, alielezea azma ya mradi wa TACIP katika kuwafikia wasanii wote nchini wa tasnia ya sanaa za ufundi kwa lengo kuu la kupata taarifa za wasanii kwa kuwabaini na kuwatambua ili kuwaunganisha katika fursa mbalimbali na kusaidia kutatua changamoto zinazowakabili.

"Zoezi hili la kutambua na kuwasajili wasanii lilianza rasmi jijini Dar es Salaam, ambapo tumetembelea na tunaendelea kutembelea wilaya zote za jiji hilo, na kwa sasa tumeingia rasmi mkoani Dodoma tukiwa na dhamira ile ile ya kupita mtaa kwa mtaa kwa nia ya kutimiza lengo la kumfikia kila msanii kwenye wilaya zote na nchi nzima kwa ujumla," alisema Mpocke.

Mkutano huo pia uliolenga kutoa mafunzo ya usajili kwa watumishi wa serikali ya mkoa wa Dodoma wakiwamo watendaji kata na mitaa, ofisa utamaduni wa wilaya pamoja na kuhudhuriwa na wabunge kadhaa wa Dodoma kama Mbunge wa Bahi, Omary Badwel; Mbunge wa Chemba, Juma Nkamia; Mbunge wa Mpwapwa, George Lubeleje; Mbunge wa Viti Maalum Dodoma, Fatma Taufiq, wawakilishi wa kampuni ya DataVision International na timu nzima ya TACIP.

# Mashine 60 za kusafisha figo kumwagwa hospitali za mikoa

BUNGE limeelezwa kuwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inatarajia kupata zaidi ya mashine 60 za kusafishia damu kwenye figo kutoka Saudi Arabia ambazo zitawekwa baadhi ya hospitali za rufani za mikoa.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Waziri wa Wizara hiyo, Ummy Mwalimu, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Kilolo (CCM), Venance Mwamoto.

Mbunge huyo alisema wagonjwa wa kisukari wameongezeka kwa kasi na mashine za kusafishia figo ziko maeneo machache ikiwamo Hospitali ya KCMC, Dodoma na Dar es Salaam, hivyo kusababisha wagonjwa kupata adha ya kusafiri umbali mrefu kwenda kusafisha figo.

"Je, serikali haioni kwamba umefika muda wa kila hospitali ya rufani ya mkoa kuwa na mashine ya kusafishia figo?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Ummy alikiri kuwa kuna ongezeko la magonjwa yasiyo ya kuambukiza ikiwamo ya kisukari, moyo na saratani.

"Kuhusu kuweka huduma za kusafisha damu kwenye hospitali za rufani za mikoa nakubaliana. Tunatarajia kupata zaidi ya mashine 60 kutoka Saudi Arabia ambazo tutaziweka baadhi ya hospitali za rufani za mikoa," alisema.

Hata hivyo, alisema changamoto iliyopo ni kupata wataalamu wanaotakiwa kutoa huduma hiyo.

"Lakini tunazungumza na serikali ya Saudi Arabia ikiwezekana tuwe na mpango wa haraka wa kupeleka wataalamu katika hospitali zao na hospitali zingine kwa mfano KCMC, Muhimbili, JKCI na Bugando ili kuongeza ujuzi," alisema.

Alisema hawataanza na hospitali zote isipokuwa wataangalia maeneo ambayo hayafikiki.

"Tutaangalia kwa mfano Katavi, hatutegemei mtu atoke Katavi hadi Mbeya, tutaangalia maeneo ambayo hayafikiki kwa mfano Katavi, Ruvuma, Rukwa, Lindi, tumebainisha hospitali tano za kuanza nazo," alisema.


Waziri huyo alisisitiza wananchi kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza kwa kufanya mazoezi pamoja na kupunguza matumizi ya tumbaku.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Kinondoni (CCM), Maulid Mtulia, alihoji ni lini serikali itanunua mashine ya CT-Scan na MRI kwa ajili ya Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala ili kupunguza msongamano katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na kuongeza ufanisi.

Akijibu swali hilo, Mwalimu alisema kutokana na mwongozo uliokuwapo, huduma za CT-Scan na MRI hazikuwapo kwenye hospitali za rufani za mikoa.

Hata hivyo, alisema kutokana na mabadiliko ya kiuchumi na uhitaji wa huduma hizo kwa wananchi, wizara ilifanya mabadiliko ya mwongozo kwa kutengeneza mwongozo wa vifaa vya radiolojia nchini mwaka jana.

Alifafanua kuwa pamoja na mengineyo huduma za CT-Scan sasa zitapatikana katika ngazi ya hospitali za rufani za mikoa na huduma za MRI zitapatikana katika ngazi za rufani za kanda na taifa. Aidha, alisema kutokana na mabadiliko hayo, serikali inakusudia kufunga CT-Scan katika hospitali ya rufani ya mkoa ya Mwananyamala na utekelezaji wake umeshaanza.



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, akitoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizotolewa na wabunge wakati wa mjadala wa hotuba ya bajeti ya wizara yake jijini Dodoma juzi. **MPIGAPICHA WETU**

## Ardhi yakumbwa na uhaba watumishi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI kupitia Bodi ya Mfuko wa Barabara inaendelea na uhakiki wa mtandao wa barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura), ili kuishauri serikali kuhusu mgawo wa fedha za Mfuko wa Barabara.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alisema hayo jana bungeni jijini hapa alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mpanda Mjini (CCM), Sebastian Kapufi.

Katika swali lake, Kapufi alisema katika bajeti ya mwaka 2018/19, Mkoa wa Katavi ulitengewa kiasi kidogo cha fedha kuliko mikoa yote.

"Je, serikali iko tayari kuongeza mgawo wa fedha kwa mkoa wa Katavi kwa kuzingatia jiografia na kilomita za mtandao wa barabara?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Waziri Jafo alisema hatua hiyo inalenga kuishauri serikali kufanya mapitio ya mgawo huo na kuhakikisha barabara zinazohudumiwa na Tarura zinatengewa bajeti ya kutosha kwa ajili ya matengenezo. Aidha, alisema katika kupanga bajeti kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya barabara kwenye mamlaka za serikali za mitaa, serikali inazingatia vigezo mbalimbali kikiwamo kigezo cha mtandao wa barabara uliosajiliwa.

"Mkoa wa Katavi katika mwaka wa fedha 2018/19 uliidhinishiwa Sh. bilioni 3.62 kwa kuzingatia mtandao wa barabara uliopo ambao ni kilometa 1,441.3," alisema.

Pamoja na hayo, alisema vigezo vingine vinavyozingatiwa ni pamoja na tabaka la barabara, hali ya mtandao wa barabara na idadi ya magari yanayotumia barabara na idadi ya watu wanaohudumiwa na barabara husika.

# Wachimbaji watozwa kodi zilizofutwa

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amekiri kupata malalamiko kutoka baadhi ya watu hasa mkoa wa Arusha na maeneo mengine kuwa wachimbaji wadogo bado wanatozwa kodi licha ya kufutwa.

Kutokana na hali hiyo, Biteko amepiga marufuku maofisa wanaohusika na utozaji wa kodi kwenye sekta ya madini kuacha kutoza kodi zilizofutwa na Bunge na itakapobainika hatua zitachukuliwa dhidi yao.

Biteko alisema hayo bungeni jijini hapa jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Momba (Chadema), David Silinde, ambaye alisema moja ya kero kubwa kwa wachimbaji hao ilikuwa sheria iliyopitishwa bungeni kodi ya zuio ya asilimia tano kwa bei ya kuuzia madini kwa wachimbaji wadogo.

"Bunge lako Februari lilibadilisha sheria na kuondoa zuio, utekelezaji baada ya kuondoa hiyo sheria umefikia wapi kwa sababu ilikuwa inasababisha madini mengi kutoroshwa?" Alihoji.


Akijibu swali hilo, Waziri Biteko alisema pamoja na kodi ya zuio na ile ya ongezeko la thamani (VAT) kufutwa kwa wachimbaji wadogo, bado kuna watu wanawatoza.

"Natoa maelekezo rasmi kwa watu wote wanaohusika kwenye utozaji wa kodi na kodi mbalimbali kwenye sekta ya madini, kodi ambazo zimefutwa na bunge hili hakuna mtu yeyote anayetakiwa kuzitoza," alisema.

"Ninasema hili na iwe marufuku kwa mtu yeyote na nikipata taarifa kwa mtu yeyote ambaye anaendelea kutoza kodi hiyo, hatua kali zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria," aliongeza.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Rhoda Kunchela, alihoji kama serikali iko tayari kutatua kero kwa wachimbaji wadogo na vibarua ambao wananyanyasika katika migodi mbalimbali nchini.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Stanslaus Nyongo, alisema wizara kupitia Tume ya Madini imeendelea kuweka mikakati ya kuwatambua wachimbaji wadogo kwa kuwapa leseni za uchimbaji.




Habari na Augusta Njoji

"Pia tunahamasisha Watanzania kote nchini kujiunga katika vikundi kwa mujibu wa sheria ya viwanda vya ushirika ili iweze kupatiwa elimu kirahisi kuhusu uchimbaji salama, utunzaji kumbukumbu za uzalishaji na namna ya kupata mikopo ya riba nafuu," alisema.

Nyongo alisema wizara imedhamiria kuondoa kero kwa wachimbaji wadogo hasa za maeneo ya kuchimba ili kuwawezesha kujiajiri katika sekta ya madini.

Aliagiza Tume ya Madini kuhakikisha wamiliki wote wa leseni za utafiti ambazo hazifanyiwi kazi zinafutwa ili maeneo hayo wamilikishwe wachimbaji wadogo wenye lengo la kuviendeleza ili kuongeza mchango wa sekta ya madini katika pato la taifa na kujenga uchumi wa viwanda.

"Migodi yote nchini inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria za Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017 na kuzingatia kanuni za uchimbaji, usalama, mazingira na afya kwa wafanyakazi," alisema.

Kuhusu unyanyasaji, Nyongo alisema unyanyasaji wa aina yoyote haukubaliki na mmiliki yeyote anayefanya hivyo atakuwa anavunja sheria ya madini na sheria za kazi mahali pa kazi.

## Viongozi wa dini wapatiwa mafunzo ya udereva

**Na Woinde Shizza, ARUSHA**

VIONGOZI wa dini kutoka makanisa mbalimbali Mkoa wa Arusha, wamehitimu mafunzo ya udereva na usalama barabarani, yaliyotolewa na Chuo cha Wide Institute of Driving, lengo ikiwa ni kudhibiti ajali zinazosababisha vifo na majeruhi.

Mkufunzi wa chuo hicho, Faustine Matina, alisema mafunzo hayo yalifanyika kwa umakini mkubwa kwa viongozi hao, ili waweze kuwa mabalozi wa usalama barabarani na kuokoa maisha ya watu.

Matina alisema kuwa viongozi hao wamehitimu mafunzo yao na kupatiwa vyeti, hivyo kukidhi matakwa ya serikali ya kuwataka madereva kuwa na vyeti vya shule ya udereva, pamoja na leseni kama vigezo muhimu kwa madereva.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Arusha, Joseph Bukombe, aliwataka viongozi hao wa dini kuhubiri masuala ya usalama barabarani, katika makanisa yao ili kuokoa maisha ya waumini wao ambao wengi ni madereva.

"Nawaomba msikae kimya mkazungumze huko makanisani, badala ya kusema nendeni kwa amani muwaambie kuwa wasisahau kufunga mkanda wanapokuwa kwenye magari yao, kwa kufanya hivyo tutaokoa maisha yao," alisema Bukombe.

Mwakilishi wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha ambaye ni Mrakibu wa Polisi Makao Makuu ya Polisi Arusha, Namsemba Mwakatobe, alisema jeshi hilo litashirikiana na viongozi wa dini katika kutatua changamoto za usalama barabarani pamoja na kutoa elimu kwa wananchi.

Mwenyekiti wa Umoja wa Makanisa mkoani Arusha, Askofu Stanley Hotay, alisema mafunzo hayo yatawasaidia viongozi wa dini, kuwa na uelewa mkubwa na kujifunza vitu vingi ambavyo walikuwa hawavijui kuhusu usalama barabarani.

# IFAD yasaidia miradi ya bil. 1.6/- Arumeru

**Na Novatus Makunga, ARUSHA**

HALMASHAURI ya Meru wilayani Arumeru, imetekeleza miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 1.6, kupitia Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), kwa ushirikiano na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB).

Akitoa taarifa kwa Rais wa IFAD, Gilbert Haungbo, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, alisema miradi hiyo imetekelezwa kufuatia taasisi hizo za kimataifa, kuingia ubia na Serikali ya Tanzania mwaka 2011.

Miradi hiyo imetekelezwa kupitia programu ya miundombinu ya masoko, uongezaji thamani na huduma za fedha vijijini (MIVARF).

Akiwa katika kiwanda cha kusindika maziwa cha The Grand Deman, kilichopo Leganga eneo la Usa River wilayani Arumeru, Rais huyo wa IFAD, alielezwa na Muro kuwa, miradi hiyo imetekelezwa kwa lengo la kuimarisha uchumi wa nchi.

Muro alisema kufanikiwa katika utekelezaji kwa miradi hiyo, kunaiingiza Tanzania katika dhamira yake ya sasa ya uchumi wa viwanda kupitia sekta binafsi.

Alikitaja Kiwanda cha The Grand Deman kama moja ya mfano wa viwanda vinavyosimamiwa na sekta binafsi, ambacho kimetekeleza kwa vitendo sera ya serikali kwa viwanda.

Alisema maendeleo ya uchumi yanategemea sekta binafsi kikiwamo kiwanda hicho katika ujenzi wa uchumi na pia kiwanda kimesaidia kutengeneza ajira kwa Watanzania.

Muro alisema kiwanda kinatoa huduma kwa wananchi waliounganishwa na kiwanda, hususani wafugaji kwa lengo la kuwaongezea kipato na kuwawezesha kuondokana na umaskini.

Alitaja miradi iliyotekelezwa katika halmashauri hiyo kwa ufadhili wa programu ya MIVARF ni pamoja na ukarabati wa ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 300 katika Kijiji cha King'ori.

Aidha, alisema MIVARF wamejenga ghala jipya katika Kijiji cha Muungano lenye uwezo wa kuhifadhi tani 1000 za mahindi, ukabarati wa barabara yenye urefu wa kilomita 18.1, inayounganisha kijiji cha Malula na King'ori.

Alisema MIVARF kupitia ufadhili wa IFAD na AFDB wamefanikiwa kuwajengea uwezo wakulima pamoja na kuwaunganisha na masoko na kuwapatia mafunzo.

Alisema programu hiyo pia ilikiwezesha kiwanda hicho kwa mitambo ya kisasa kwa ajili ya usindikaji na kupoozea maziwa.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda hicho, Dk. Deo Temba, alisema mbali na kutoa ajira, pia kinazalisha bidhaa mbalimbali zikiwamo mtindi, jibini, maziwa na siagi.

Dk. Temba alisema kiwanda hivi sasa kinasindika kati ya lita 4,131 hadi 5,000 za maziwa kwa siku.

"Kiwanda kimeuwaunganisha wakulima kutoka katika vikundi zaidi ya 15, wa halmashauri za Siha, Meru na Arusha," alisema.

Alisema hivi sasa kinapokea kati ya lita 2,150 hadi 3,131 kwa siku za maziwa.

Aidha, alisema kiwanda hicho kimeunganishwa na wakulima kati ya 200 hadi 600 ambao wanapeleka maziwa katika kiwanda hicho.

Kwa upande wake Rais wa IFAD, Haungbo, aliipongeza Serikali ya Tanzania kwa kubuni miradi inayolenga kuwakomboa wananchi wenye uchumi wa chini, hususani wanawake wa vijijini.

Alisema, asilimia kubwa ya wazalishaji mali vijijini na ambao ndiyo wanaoendesha familia ni wanawake.



Diwani wa Kata ya Babati mkoani Manyara, Mohamed Kibiki (kulia), akiongoza kikao cha tathmini ya ujenzi wa vyumba vya madarasa ya Shule ya Sekondari Kwaraa, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Ukame wakwamisha wananchi kufunga ndoa

**Na Asraji Mvungi, ARUSHA**

WANANCHI wanaoishi vijiji vilivyoko pembezoni mwa wilaya za Mbulu mkoani Manyara na Karatu mkoani Arusha, wamelalamikia kuendelea kukabiliwa na umaskini wa kipato unaotokana na kuandamwa na ukame, unaowaathiri kukaa bila kufunga ndoa.

Wananchi hao waliyasema hayo wakati wa ibada maalumu ya kuadhimisha Siku ya Familia, iliyoandaliwa na Kanisa Katoliki Parokia ya Kitete, iliyoko Wilaya ya Karatu mkoani Arusha na waamini zaidi ya 240 kujitokeza kupata huduma ya kufunga ndoa baada ya kanisa hilo kuwalipia gharama za stakabadhi za ndoa.

Wakizungumzia ukubwa wa tatizo hilo, wananchi hao walisema kutokana na kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo, ambayo ndio tegemeo lao kwa chakula na biashara, uwezo wao wa kutekeleza majukumu muhimu yakiwamo ya kuhudumia familia na maendeleo yamekuwa yakipungua siku hadi siku.

Mmoja wa wananchi hao, Antony Simion, mkazi wa Kijiji cha Kitete, Tarafa ya Mbulumbulu wilayani Karatu, alisema athari ni kubwa zaidi kwa wanawake na vijana, hasa wa kike ambao licha ya kuathirika kiuchumi, pia wanakabiliwa na tatizo kubwa la migogoro ya kifamilia, ambayo huchangiwa na baadhi yao kujihusisha na vitendo vya ulevi.


"Hali inapokuwa ngumu mambo mengi yanakwenda nje ya utaratibu na kiasi kidogo kinachopatikana kimekuwa kikitumika kwa mambo muhimu pekee, mfano kwa sasa wananchi wengi hawataki kufunga ndoa kutokana na fedha kidogo wanayopata kuitumia kwenye mahitaji ya chakula, elimu kwa watoto wao na matibabu na ni masuala ambayo pia ni ya muhimu," alisema mzee Simion.

Akizungumzia tatizo la watu wengi kuishi bila kufunga ndoa, Paroko wa Parokia hiyo, Sebastian Mwilinga, alisema kwa upande wao wameanzisha utaratibu wa kuzitembelea familia zilizoathirika na kuzipatia elimu na ushauri nasaha, unaolenga kuwawezesha kudumisha upendo katika familia zao.

Sebastian alisema katika harakati hizo pia walibaini kuwapo kwa tatizo kubwa la watu wengi kuishi kama mume na mke bila kuwa na ndoa, utaratibu ambao umekuwa chanzo cha wanawake na watoto kutekelezwa hasa wakati huu, ambao shughuli za kiuchumi zimeyumba kutokana na ukame.

"Baada ya kuona tatizo hilo tulianza kampeni ya kutoa elimu maalumu ya umuhimu wa kufunga ndoa, ambayo licha ya wengi wao kuelewa, bado waliendelea kusingizia kuwa hawafungi ndoa kutokana na ukosefu wa fedha za gharama za ndoa," alisema Paroko Sebastian.

Alisema katika kutatua tatizo hilo, uongozi wa parokia hiyo ulilazimika kuwaondolea wananchi hao gharama za hati za ndoa na kutangaza siku maalumu ya kufunga ndoa, bila malipo ambayo wananchi zaidi 240 walijitokeza. Tukio hilo liliongozwa na Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Mbulu, Mhasham Antony Gasper, ambaye licha ya kuwapongeza wananndoa hao, pia aliwasifu viongozi wa parokia hiyo kwa ubunifu ambao ni mfano wa kuigwa maeneo mengine.





# Wataka miradi chini ya uongozi wa mpito

**Na Godfrey Mushi, SAME**

WANANCHI wa Kijiji cha Vunta katika uwanda wa juu wa milima ya Upare ambao walipiga kura ya kumng'oa madarakani mwenyekiti wa serikali ya kijiji hicho, wamemwomba Mkuu wa Wilaya ya Same, kuagiza miradi yote ya maendeleo iliyokuwa chini ya kiongozi huyo itekelezwe na kamati maalum ya mpito.

Mkuu wa wilaya hiyo, Rosemary Senyamule, amethibitisha taarifa za kung'olewa madarakani kwa mwenyekiti wa kijiji hicho, baada ya wananchi wake kupiga kura ya kumkataa.

"Hao wananchi wa Kijiji cha Vunta ni kweli wamepiga kura za kumkataa Mwenyekiti wa Kijiji baada ya kutokuwa na imani naye, kwa kumtetea mtu aliyejimilikisha ardhi ya kijiji bila wananchi kuridhia," alisema.

"Unajua pamoja na mambo mengine pia hao wananchi wana madai yao ya msingi kwamba serikali iliyoondolewa madarakani kwa kura, ilikuwa haiwasomei taarifa za kijiji kwa muda mrefu na makosa mengine ya kiuongozi."

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Wilaya, mwenyekiti aliyeondolewa madarakani ni Joseph Makengo ambaye hakujitetea alipopewa nafasi.

Aidha, tukio hilo lilienda sambamba na wananchi wa Kitongoji cha Hemwambo pia kupiga kura za kutokuwa na imani na mwenyekiti wao ambaye ndiye aliyejinyakulia eneo hilo la kijiji.

Kutokana na ombi hilo la wananchi wa Vunta, Mkuu huyo wa Wilaya ya Same, amemwagiza Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho kuchagua uongozi wa muda ndani ya wiki moja ili kuendelea na shughuli za maendeleo.

Katika hatua nyingine, wananchi wa eneo hilo wameiomba serikali wilayani humo kuupeleka mwenge wa Uhuru katika eneo hilo, kwa kuwa tangu nchi ipate uhuru wameuona mara moja tu.

Wilaya ya Same, zaidi ya nusu ya wananchi wake wanaishi milimani.

**"Unajua pamoja na mambo mengine pia hao wananchi wana madai yao ya msingi kwamba serikali iliyoondolewa madarakani kwa kura, ilikuwa haiwasomei taarifa za kijiji kwa muda mrefu na makosa mengine ya kiuongozi.**

# Wabeba wagonjwa, maiti kwa machela

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

UBOVU wa miundombinu ya barabara katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, unadaiwa kusababisha baadhi ya wananchi hasa wanaotoka kwenye maeneo ya ukanda wa tambarare kupata adha kubwa ikiwamo kusafirisha wagonjwa.

Hayo yalisemwa jana na madiwani wa halmashauri hiyo, muda mfupi baada ya kuwasilishwa katika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani taarifa ya Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (Tarura).

Diwani wa Kata ya Kirua Vunjo Magharibi, Joseph Mawere, alisema ubovu wa miundombinu ya barabara umesababisha wananchi katika baadhi ya maeneo kubeba maiti na wagonjwa kwa kutumia machela, huku wakipata adha kubwa kufikia huduma mbalimbali za kijamii.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya madiwani wameeleza masikitiko yao kuwa wananchi wao wanavyopata adha kutokana na kata nyingi kukabiliwa na changamoto kubwa ya uharibifu wa mawasiliano ya barabara hasa katika kipindi hiki cha mvua za masika zinazoendelea kunyesha.

"Kwa sasa wananchi wa vijiji vingi, barabara zinapitika kwa shida ikiwamo wanafunzi na walimu kushindwa kwenda shule nyakati za mvua, zahanati, vituo vya afya na hospitali kushindwa kupata vifaa tiba kutokana na magari kushindwa kupita na mengine kukwama wakati yakipeleka vifaa hivyo kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi maeneo ya vijijini," alisema Diwani wa Marangu Magharibi, Filbert Shayo.

Aidha, Shayo akichangia mjadala huo kuhusu hali ya barabara, alisema: "Tuna tatizo ambalo lazima litatuliwe na sisi viongozi wa vijiji na kata tuache kutegeana na tuondoe dhana ya kukwepa kushiriki katika ujenzi wa miundombinu ya barabara.

"Tushirikiane na wananchi wetu pale ambapo Tarura wamechelewa kufanya kazi yao ili tusiwe sehemu ya kuchangia wananchi kukwama kupata huduma za jamii na kufanya shughuli za maendeleo."

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Michael Kilawila, aliitaka Tarura katika wilaya hiyo kuwasilisha kwao taarifa ya utekelezaji wa miradi ya barabara zilizokuwa zimetengewa bajeti katika mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, mwaka huu.

Kilawila pia aliitaka Tarura kushirikisha viongozi wa vijiji, kata na wananchi katika miradi inayotekelezwa ili kumaliza malalamiko ya wananchi dhidi ya makandarasi wanaodaiwa kujenga chini ya kiwango miradi ya barabara.

Akijibu hoja za madiwani hao, Mhandisi wa Barabara wa Tarura katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Loisheyi Mollel, alisema amezipokea kero hizo na anakwenda kuzifanyia kazi.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Tarura itatumia zaidi ya Sh. bilioni 1.1 katika ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 674.52 ikiwamo ahadi ya Rais John Magufuli ya ujenzi wa barabara yenye urefu kilomita 20.

Barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami kuanzia eneo la Geti Fonga kwenda Mabogini hadi Mhekereni kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 22.



Mchuuzi wa sendozi akizitembeza kutafuta wateja katika eneo la Tandika, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Maonyesho Kili Fair kufanyika Arusha

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MAONYESHO ya Kimataifa ya Biashara ya 'Karibu Kili Fair' yanayotangaza utajiri wa vivutio vya utalii wa Tanzania, kwa mwaka huu yamepangwa kufanyika kwa mara ya kwanza katika Jiji la Arusha.

Karibu Kili Fair inayobeba maudhui na utajiri wa Tanzania unaotokana na sekta ya utalii ilikuwa ikifanyika mfululizo katika mji wa Moshi kwa miaka kadhaa, lakini sasa yanafanyika kwa miji hiyo kupokezana uandaaji wake. Kwa mwaka huu yatafanyika Juni 7 hadi 9 eneo la Friedkin Recreation Center jijini Arusha, zamani ukijulikana kama viwanja vya TGT.

Akizungumzia maandalizi ya maonyesho hayo jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Kili Fair Promotion Ltd, Tom Kunkler, alisema washiriki wa maonyesho hayo kutoka nchi mbalimbali duniani, wanafikia 450.

Alisema kampuni za utalii zipatazo 450 na mashirika ya ndege ya kimataifa yamethibitisha ushiriki wao na kwamba maonyesho hayo yatavutia zaidi ya watu 5,000 watakaokwenda kuyatembelea.

Kivutio kipya mwaka huu ni pamoja na kuitangaza Hifadhi ya Taifa ya Ruaha yenye ukubwa wa kilomita za mraba 20,226 na maili 7,800.

Kwa sasa, Ruaha ndiyo hifadhi kubwa kuliko zote nchini Tanzania, ikiwa inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya tembo kuliko hifadhi nyingine yoyote iliyoko katika nchi za Afrika Mashariki.

Kingine ni uwekezaji wa kampuni ya kimataifa ya utafutaji na uokozi ya Kilimanjaro SAR iliyowekeza Dola za Marekani milioni tatu, kuanzisha kliniki maalumu ya kwanza ya tiba barani Afrika ambayo kwa siku moja inafanya safari zisizopungua nane.

Kliniki hiyo ina madaktari wasio na mipaka na inatoa msaada wa uokozi na matibabu kwa watalii wanaopata ajali na kuathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro na Mlima Meru ulioko ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Arusha.

Awali, akizungumzia maandalizi ya maonyesho hayo, Mkurugenzi Mwenza wa Kili Fair Promotion Ltd, Dominic Shoo, alisema maonyesho ya utalii ya Karibu Fair na Kili Fair yameunganishwa na kuwa kitu kimoja.

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,
# WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI



WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI,
MHE. LUHAGA JOELSON MPINA

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI, MHE. ABDALLAH ULEGA

KATIBU MKUU SEKTA YA MIFUGO,
PROF. ELISANTE OLE GABRIEL

KATIBU MKUU SEKTA YA UVUVI,
DKT. RASHID TAMATAMAH

# HOTUBA YA WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2019/2020

# HOTUBA YA WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2019/2020

## A: UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji iliyochambua bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99 – Mifugo na Fungu 64 – Uvuvi) Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019. Aidha, naliomba pia Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa namshukuru sana **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kushika wadhifa huu. Pia, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuiongoza nchi yetu kwa uhodari na umahiri mkubwa katika kipindi kifupi tangu aingie madarakani. Katika kipindi cha miaka minne (4) tumeshuhudia mageuzi makubwa ya uchumi na maendeleo na amekuwa Kiongozi wa mfano na wakuigwa Afrika na Dunia. Utendaji wake umewaridhisha wananchi, viongozi na hata taasisi kubwa zinazoaminika kimataifa. Mhe. Rais pamoja na kuwepo na kauli za kukatishwa tamaa zinazotolewa na baadhi ya watu, **"endeleza mapambano ya kusaka maendeleo ya watanzania na sisi wasaidizi wako tupo imara na tutaendelea kufanya kazi usiku na mchana ili matarajio ya watanzania kwa Serikali ya awamu ya tano yafikiwe".**

3. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, nawapongeza Mheshimiwa **Dkt. Ally Mohamed Shein**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa **Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.),** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiongoza vema nchi yetu kwa hekima na busara.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza, Mheshimiwa **Kassim Majaliwa Majaliwa,** Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango (Mb**) Waziri wa Fedha na Mipango, kwa hotuba zao ambazo zimefafanua vizuri mipango na mikakati ya Serikali katika mwaka wa fedha 2019/2020 yenye lengo la kuimarisha na kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii nchini.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza vizuri Bunge letu Tukufu. Ni imani yangu kuwa, mtaendelea kuliongoza Bunge hili kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo stahiki ili Bunge liweze kuisimamia na kuishauri Serikali.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake **Mhe. Mahamoud Hassan Mgimwa**, Mbunge wa Mufindi Kaskazini na Makamu wake **Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma**, Mbunge wa Viti Maalum Morogoro kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri waliotoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, napenda kuwapongeza **Mhe. Abdallah Ally Mtolea**, Mbunge wa Temeke, **Mhe. Said Maulid Mtulia**, Mbunge wa Kinondoni, **Mhe. James Ole Milya**, Mbunge wa Simanjiro, **Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara** Mbunge wa Ukonga, **Mhe. Julius Kalanga Laizer** Mbunge wa Monduli, **Mhe. Pauline Philipo Gekul**, Mbunge wa Babati Mjini, **Mhe. Ryoba Chacha Marwa,** Mbunge wa Serengeti, **Mhe. Joseph Michael Mkundi**, Mbunge wa Ukerewe, **Mhe. Mhandisi Christopher Kajolo Chiza** Mbunge wa Buyungu, **Mhe. Timotheo Paul Mnzava** Mbunge wa Korogwe Vijijini, **Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka** Mbunge wa Liwale kwa kuchaguliwa na kisha kuapishwa na Bunge lako Tukufu ili wawatumikie wananchi waliowachagua.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Mbunge wa Korogwe Vijijini; Marehemu Steven Ngonyani Mbunge mwenzetu. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya marehemu, ndugu na wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijijini. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi Amina. Aidha, naomba pia, nitumie fursa hii kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge waliopata ajali mbalimbali na waliougua katika kipindi cha Mwaka 2018/2019.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** pia nichukue nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi **Mhe. Abdallah Hamis Ulega**, Mbunge wa Mkuranga pamoja na Makatibu wakuu **Prof. Elisante Ole Gabriel** (Mifugo) na **Dkt. Rashid Adam Tamatamah** (Uvuvi) kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika kuiongoza Wizara.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kwa mara nyingine tena niwapongeze na kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kisesa kwa kunichagua na kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha na kuwatumikia katika Bunge hili Tukufu.

## B: SEKTA YA MIFUGO

### HALI YA SEKTA YA MIFUGO

10. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2018/2019 idadi ya mifugo hapa nchini inakadiriwa kuongezeka ikilinganishwa na mwaka 2017/2018 ambapo idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka **milioni 30.5** hadi **milioni 32.2,** mbuzi kutoka **milioni 18.8** hadi **milioni 20** na kondoo kutoka **milioni 5.3** hadi **milioni 5.5**. Aidha, kuku wameongezeka kutoka **milioni 74.8** hadi **milioni 79.1** ikiwa kuku wa asili wameongezeka kutoka **milioni 38.2** hadi **milioni 38.5**, kuku wa kisasa wameongezeka kutoka **milioni 36.6** hadi **milioni 40.6**, nguruwe kutoka **milioni 1.9** hadi **milioni 2** na punda kutoka **595,160** hadi **636,997** (Chanzo: Mpango Kabambe wa Mifugo Tanzania). Aidha, Sekta ya Mifugo katika mwaka 2018 ilikua kwa asilimia **4.9** na kuchangia asilimia **7.6** katika Pato la Taifa.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa maziwa hapa nchini umeongezeka kutoka lita **bilioni 2.4** mwaka 2017/2018 na kufikia lita **bilioni 2.7** hadi mwezi Aprili Mwaka 2018/2019 **(Kiambatisho Na.1)** ikiwa ni ongezeko la asilimia **12.5**. Ongezeko la uzalishaji limetokana na kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji katika tasnia ya maziwa nchini ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa kiwango cha tozo kutoka shilingi **150** hadi shilingi **2,000** kwa lita/kilo ya maziwa yanayoingizwa nchini.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka hadi kufikia **tani 690,629** mwaka 2018/2019 (Machi, 2019) ikilinganishwa na **tani 679,992** mwaka 2017/2018 (**Kiambatisho Na.1**), ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia **1.6.** Aidha, jumla ya **tani 516.63** za nyama zenye thamani ya Dola za Marekani **2,160,974.33** ziliingizwa nchini mwaka 2018/2019 (Machi, 2019) ikilinganishwa na **tani 1,401.96** za nyama zenye thamani ya Dola za Marekani **4,368,858.07** zilizoingizwa nchini mwaka 2017/2018 sawa na upungufu wa **asilimia 63.15**. Upungufu huu umechangiwa na uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji, kuongezeka kwa uzalishaji katika viwanda vya ndani na udhibiti wa uingizaji holela wa nyama kutoka nje ya nchi. Pia, uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai **bilioni 3.2** mwaka 2017/2018 hadi mayai **bilioni 3.6** mwaka 2018/2019 (**Kiambatisho Na. 1**).

13. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **tani 16,012** za ngozi za ng'ombe, mbuzi na kondoo zenye thamani ya shilingi **bilioni 22.8** zimezalishwa hadi mwezi Aprili Mwaka 2018/2019, ikilinganishwa na **tani 15,389** zenye thamani ya shilingi **bilioni 22** zilizozalishwa katika Mwaka 2017/2018**.**

14. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya marobota ya hei **550,919** yenye wastani wa uzito wa kilo **10** kila moja yalizalishwa mwaka 2018/2019 kutoka kwenye mashamba ya Serikali ikilinganishwa na marobota **482,246.4** yaliyozalishwa mwaka 2017/2018. Ongezeko hilo la asilimia **14.2** limetokana uboreshaji wa mashamba. Vilevile, jumla ya tani **12.1** za mbegu bora za malisho zilizalishwa kutoka katika mashamba ya Serikali mwaka 2018/2019 ikilinganishwa na tani **10** zilizozalishwa mwaka 2017/2018.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa na kutekeleza Mkakati wa Kutafuta Ufumbuzi wa Kudumu wa Migogoro ya Wafugaji na Watumiaji Wengine wa Ardhi ambapo Wizara imefanikiwa kutatua migogoro **27** kati ya migogoro **43,** sawa na asilimia **62.8** katika Mikoa Mitano (**5**) ya Kigoma, Katavi, Mbeya, Rukwa na Pwani.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti magonjwa 11 ya kimkakati kwa kutumia chanjo. Mahitaji ya chanjo kwa magonjwa hayo ni jumla ya dozi **milioni 41.6** kwa ng'ombe, dozi **milioni 30.6** kwa mbuzi na kondoo, dozi **milioni 4** kwa mbwa na paka, dozi **milioni 112.5** kwa kuku wa asili na dozi **milioni 121.8** kwa kuku wa kisasa. Aidha, jumla ya chanjo dozi **301,593,730** ziliingia sokoni kwa ajili ya kukabiliana na magonjwa mbalimbali. Kati ya hizo dozi **39,548,500** zilizalishwa nchini zenye thamani ya **shilingi 1,599,143,000** na dozi **222,496,730** ziliingizwa nchini zenye thamani ya **shilingi 16,350,945,000** ziliagizwa kutoka nje ya nchi. Chanjo zilizozalishwa nchini ni dozi **38,245,800** za Mdondo (I2), dozi **1,114,850** za Kimeta na dozi **187,850** za Chambavu. Kiwango cha chanjo zilizoagizwa nchini ni dozi **26,840,000** za Homa ya Mapafu ya ngómbe (CBPP), dozi **182,000** za Homa ya Mapafu ya Mbuzi (CCPP), dozi **1,074,230** za Kichaa cha Mbwa (Rabies), dozi **122,505,000** za Mdondo, dozi **2,500** za Kutupa Mimba (Brucellosis), dozi **457,000** za Sotoka ya Mbuzi (PPR), dozi **103,984,500** za *Gumboro* na dozi **7,000,000** za *Mareks*.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa taarifa ya utafiti uliofanywa na Wizara mwaka 2006 na mwaka 2007 ulibaini kuwa, Magonjwa yaenezwayo na kupe yasipodhibitiwa huchangia asilimia **71.4** ya vifo vyote vya ng'ombe. Magonjwa hayo na asilimia ya uchangiaji kwenye vifo ni Ndigana Kali (**43.5**), Ndigana Baridi (**16.5**), Maji Moyo (**6.3**) na Mkojo Mwekundu (**5.1**). Hasara itokanayo na magonjwa hayo ni takriban Dola za Marekani **milioni 364** sawa na shilingi za Kitanzania **bilioni 815.36** kwa mwaka. Hasara nyingine ni kupungua kwa uzalishaji, kushuka kwa thamani ya ngozi, kupoteza wanyama kazi na udumavu wa ndama.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** magonjwa yaenezwayo na kupe hudhibitiwa kwa kutumia dawa *(acaricides)* hususan kwa njia ya kuogesha mifugo kwa kutumia majosho, kunyunyiza au kupaka. Uogeshaji huo umekuwa ukizorota kutokana na gharama kubwa ya dawa na usimamizi usioridhisha wa uendeshaji wa majosho na kusababisha magonjwa hayo kuendelea kuwepo na hivyo kuwa tishio kwa mifugo mingi nchini. Wizara inaendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kampeni ya uogeshaji. Kabla ya uzinduzi wa kampeni, kiwango cha uogeshaji kwa mwaka kilikuwa ni **asilimia 10** (Taarifa ya Mtaalamu Mwelekezi: Ujenzi wa Majosho na Matumizi ya dawa za ruzuku-PAPAC, 2017). Baada ya uzinduzi wa Kampeni ya uogeshaji mifugo mwezi Desemba, 2018, wastani wa uogeshaji umefikia jumla ya michovyo **10,145,457** kwa mwezi. Michovyo hiyo ni ya ng'ombe **5,600,042**, Mbuzi **3,209,079** na Kondoo **1,278,917.** Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 uogeshaji mifugo umefikia **asilimia 25** kwa mwezi ambalo ni ongezeko la **asilimia 15**.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi 2019, kuna jumla ya majosho **2,533** nchini ambapo kati ya hayo yanayofanya kazi ni **1,486** na mabovu **1,047**. Mahitaji ya awali ya majosho nchini ni **3,788** na hivyo kufanya upungufu kuwa **1,255.** Hata hivyo, Wizara inaendelea kufanya tathmini ya mahitaji halisi ya majosho nchini ambapo tathmini hiyo inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2019.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 jumla ya **lita 518,406** za dawa vimiminika za kuogesha mifugo zenye thamani ya **shilingi 15,939,982,800.00** ziliingizwa kutoka nje ya nchi na nyingine kuzalishwa nchini. Kati ya hizo, **lita 327,530.5** zenye thamani ya **shilingi 8,544,009,500.00** ziliagizwa kutoka nje ya nchi na **lita 190,875.5** zenye thamani ya **shilingi 6,388,580,800.00** zilizalishwa nchini. Aidha, dawa za unga jumla ya **kilo 67,159.5** zenye thamani ya **shilingi 1,007,392,500.00** zinazoua wadudu wasumbufu kwa mifugo zilizalishwa nchini.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019 biashara ya mifugo nchini imeendelea kuimarika ambapo jumla ya shilingi **trilioni 1.4** zilipatikana kutokana na mauzo ya mifugo katika minada mbalimbali hapa nchini, ikiwa ni mapato ya ng'ombe **2,253,100**, mbuzi **2,003,200** na kondoo **385,500** waliuzwa ikilinganishwa na ng'ombe **1,614,321** mbuzi **1,340,222** na kondoo **315,636** kwa shilingi **trilioni 1.1** waliouzwa katika mwaka 2017/2018.

### MAPITIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2018/2019

**Makusanyo ya Maduhuli**

22. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi **18,467,945,100.** Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 kiasi cha shilingi **33,853,050,919** kimekusanywa na Wizara kutoka Sekta ya Mifugo sawa na asilimia **183.31** ya lengo la makusanyo. Ongezeko hili linatokana na Wizara kuendelea kuimarisha udhibiti wa upotevu wa mapato, marekebisho katika ada na tozo mbalimbali zin-

## HOTUBA YA WIZARA YA UFUGAJI NA UVUVI

azotozwa katika Sekta ya Mifugo.

**23.** *Mheshimiwa Spika,* Vyanzo vikuu vya fedha hizo ni pamoja na:- Leseni za kusafirisha wanyama na mazao yake nje ya nchi *(export duty license fees);* Ada ya kutoa vibali vya kusafirisha wanyama, nyama, ngozi na mazao mengine nje ya nchi; Ada ya huduma ya vibali vya kusafirisha mifugo ndani ya nchi *(Movement Permits)*; Ushuru wa soko *(Market fee);* Faini: na Mauzo ya chanjo za mifugo, mifugo, mitamba na mazao ya mifugo (**Kiambatisho Na.2).** Mchango wa kila chanzo kwa mwaka 2018/19 ni kama inavyoonekana hapa chini:




**24.** *Mheshimiwa Spika;* Wizara imefanya tathmini ya utekelezaji wa Waraka wa Rais Na.1 wa Mwaka 2002 unaozitaka Halmashauri zote nchini kuchangia asilimia isiyopungua 15 kwa mapato yatokanayo na mifugo nchini katika mwaka 2017/2018. Tathmini hiyo inaonesha kuwa, Halmashauri **130** kati ya **185** zenye rasilimali ya mifugo nchini zilikusanya kiasi cha shilingi **17,461,690,975.86** ambapo kiasi cha shilingi **1,373,287,346.85** kilitengwa kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Mifugo ambacho ni sawa na asilimia **7.9** ya makusanyo yote. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa Wakuu wa mikoa ya Tabora, Iringa, Mwanza na Shinyanga kwa kusimamia zoezi hili kwa kiwango cha juu. Vilevile, Wizara yangu imewaandikia barua ya pongezi Wakuu wa Mikoa na Halmashauri zilizofanya vizuri ambazo ni Tarime DC, Magu DC, Kiteto DC, Moshi DC, Same DC, Chato DC, Simanjiro DC na Mbeya Mji. Hata hivyo, baadhi ya Halmashauri hazikufanya vizuri zikiwemo Chunya DC, Njombe DC, Kaliua DC, Morogoro Manispaa, Uvinza DC na Sikonge DC **(Kiambatisho Na.3 ).**

**25.** *Mheshimiwa Spika,* Wizara imefanya tathmini na mapitio ya orodha ya kodi, tozo na ada zinazotozwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Taasisi zake na Wizara nyingine chini ya Sheria mbalimbali za mifugo na kubaini baadhi ya kodi, tozo na ada hizo ni kero kwa wafugaji na maendeleo ya Sekta ya Mifugo kwa ujumla. Katika mwaka 2019/2020 Wizara imetoa mapendekezo ya kuziboresha ili kuondoa usumbufu wa kodi, tozo na ada kwa wafugaji na hivyo kuongeza mapato katika Sekta ya Mifugo na kutoa huduma za mifugo kwa wafugaji. Jumla ya Tozo **10** zimependekezwa kufutwa ikiwa ni pamoja na tozo (**4**) za Maziwa, (**5**) za Nyama na Kuku (**1**) **(Kiambatisho Na. 4).**

**Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

**26.** *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Sekta ya Mifugo ilitengewa jumla ya shilingi **35,362,663,000.** Kati ya Fedha hizo, shilingi **30,362,663,000.00** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi **5,000,000,000.00** ni fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi **20,458,552,489.00** ni mishahara na shilingi **9,904,110,511.00** ni Matumizi Mengine. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2019, jumla ya shilingi **23,291,626,966.48** zilikuwa zimetolewa, ambazo ni sawa na asilimia **76.7** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, shilingi **13,285,693,400.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara (PE) na shilingi **7,832,745,480.48** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**27.** *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Sekta ya Mifugo ilitengewa jumla ya **shilingi 5,000,000,000** za Matumizi ya Maendeleo zikiwa ni fedha za ndani. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 kiasi cha shilingi **2,173,188,086.00** (sawa na asilimia **43**) kilikuwa kimetolewa na Wizara ya Fedha na Mipango.

**Maeneo ya Vipaumbele katika Mpango na Bajeti 2018/2019**

**28.** *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2018/2019 Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Sekta ya Mifugo nchini, iliainisha na kutekeleza maeneo ya vipaumbele yaliyohusu utekelezaji wa Sekta ya Mifugo. Maeneo hayo ni pamoja na:-

(i)
(i) Kuimarisha mashamba ya kuzalisha mitamba na vituo vya uhimilishaji mifugo na kuhamasisha, kusimamia matumizi ya zana, mitambo na teknolojia sahihi katika uzalishaji wa mifugo yenye tija;
(ii) Kuimarisha miundombinu ya uzalishaji mifugo na masoko (minada, majosho na malambo) na kuongeza thamani ya mazao ya mifugo;
(iii) Kudhibiti magonjwa ya milipuko na magonjwa ya kipaumbele;
(iv) Kuongeza upatikanaji na matumizi ya pembejeo na zana za mifugo;
(v) Kuainisha, kupima, kutenga, kumilikisha na kuhamasisha utengaji wa maeneo ya malisho kwa ajili ya mifugo ili kupunguza migogoro ya ardhi kati ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi na rasilimali zingine;
(vi) Kuimarisha utafiti, mafunzo na ugani wa mifugo kwa kujenga na kukarabati miundombinu ya vituo vya utafiti na vyuo vya mafunzo ya mifugo kuvipatia watumishi na vitendea kazi;
(vii) Kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya mazao ya mifugo na pembejeo pamoja na kuvifufua viwanda vya zamani;
(viii) Kuhamasisha na kusimamia matumizi ya zana na mitambo na teknolojia sahihi katika uzalishaji wa mifugo yenye tija;
(ix) Kuhamsisha, kuimarisha na kujenga ushirika wa vyama vya wafugaji; na
(x) Kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya kukuza uwekezaji wa sekta binafsi katika sekta ya mifugo.

**Sera, Mikakati na Programu**

**29.** *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2018/2019 Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 na Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo wa mwaka 2010. Jumla ya wadau **4,800** walipata elimu hiyo kupitia Maonesho ya Sabasaba, Nanenane na Siku ya Chakula Duniani. Aidha, Wizara imesambaza nakala **350** za Sera ya Taifa ya Mifugo na nakala **100** za Fursa za Uwekezaji kwa wadau katika Sekta ya Mifugo.

**30.** *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2018/2019 Wizara ilikamilisha na kuzindua Mpango Kabambe wa Mifugo Tanzania *(Tanzania Livestock Master Plan – TLMP)* hapo tarehe 10 Machi, 2019. Mpango huu umeainisha mahitaji ya jumla ya shilingi **trilioni 1.4** zinahitajika katika utekelezaji wa Mpango ambapo asilimia **64** ya fedha hizi zinatarajiwa zitokane na Sekta binafsi na asilimia **36** zitokane na Serikali. Kupitia Mpango huu, Wizara imeweza kujua hali halisi ya uzalishaji na mahitaji ya mazao yatokanayo na mifugo kwa kuzingatia ongezeko la idadi ya watu, ukuaji wa miji na kipato. Kwa namna ya pekee sana napenda kuwashukuru Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo *(International Livestock Research Institute)* kwa ufadhili wa Taasisi ya Bill & Melinda Gates Foundation (BMGF) tulioshirikiana nao katika kuandaa Mpango. Aidha, Mpango huu umeainisha kanda tatu za mifugo nchini kama ifuatavyo:-

(i) Kanda ya Nyanda za Juu ikijumuisha Kanda ya Kaskasini (Arusha na Kilimanjaro) na Kanda ya Kusini (Iringa, Katavi, Mbeya, Njombe, Rukwa na Songwe), Kanda hii imeainishwa kwa ajili ya uwekezaji na uzalishaji wa maziwa kama zao kuu;
(ii) Kanda ya Kati (Dodoma, Manyara, Morogoro, Simiyu, Singida, Tabora na Shinyanga). Kanda hii imeainishwa kwa ajili ya uwekezaji wa uzalishaji wa nyama; na
(iii) Kanda ya Pwani (Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Pwani na Tanga) na Kanda ya Ziwa (Geita, Kagera, Kigoma, Mara na Mwanza), Kanda ya Pwani na ziwa ni kwa ajili ya uwekezaji na uzalishaji wa nyama na maziwa kwa upande wa ng'ombe, mbuzi na kondoo.

**31.** *Mheshimiwa Spika,* katika Mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Mifugo Tanzania kupitia mfumo wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *(Agriculture Sector Development Programme – ASDP II)*. Aidha, Wizara itafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 ili kuboresha mazingira ya biashara.

**32.** *Mheshimiwa Spika,* katika Mwaka 2018/2019 Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Sekta ya Kilimo pamoja na wadau wengine imeanza kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini Awamu ya Pili (ASDP II). Uzinduzi wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II), ulizinduliwa na **Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 4 Juni, 2018. Lengo la ASDP II ni kufanya mageuzi ya Sekta ya Kilimo (mazao, mifugo na uvuvi) ili kuongeza uzalishaji na tija kwa ajili ya uhakika wa chakula, kuongeza kipato kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na Taifa kwa ujumla.

**Sheria na Kanuni**

**33.** *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2018/2019 Wizara imeandaa Waraka wa Mbari za Wanyama *(Animal Breeding Cabinet Paper)* ambao upo katika ngazi ya Sekretariati ya Baraza la Mawaziri. Aidha, Wizara inafanya mapitio ya Sheria Na. 13 ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama ya Mwaka 2010 ili kukidhi mahitaji ya sasa.

**34.** *Mheshimiwa Spika,* Wizara imekamilisha kuandaa Kanuni za Fedha na Utumishi za Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania, 2017 ambazo zimeidhinishwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali GN No. 27 la Mwaka 2018. Pia, Kanuni zifuatazo za Tasnia ya Mifugo zimeandaliwa na tayari zimeshatangazwa katika Gazeti la Serikali. Kanuni hizo ni:-

(i) *The Animal Diseases (Animals and Animal Products Movement Control) (Amendment) Regulations, 2018 GN No. 475* ambayo imebadilisha viwango vya tozo;
(ii) *The Animal Diseases (Livestock Markets), 2018 GN No. 478;* na
(iii) *The Animal Diseases (Animals and Animal Products Movement Control)*, 2019 GN No. 25.

**35.** *Mheshimiwa Spika,* Wizara pia, imefanya maandalizi ya Kanuni sita (6) ambazo zitatolewa baada ya marejeo ya Sheria Na. 13 ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama ya Mwaka 2010 kukamilika. Kanuni hizo ni:-

(i) *Import and Export of Animal Feed Resources Regulation;*
(ii) *Detention, Treatment, Disposal and Distruction of Animal Feed Resources, Regulation;*
(iii)
(iv) *Packing, Branding, Labeling and Sealing of Animal Feed Resources Regulation;*
(v)
(vi) *Animal Feed Resources Product Registration Regulation;*
(vii)
(viii) *Fees and Charges of Animal Feed Resources Regulation; na*
(ix)
(x) *Varietal Purity Certification of Pasture Seeds Regulation.*

**36.** *Mheshimiwa Spika,* Wizara inaandaa kanuni chini ya Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na.17 ya Mwaka 2003 na Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na.19 ya Mwaka 2008. Kanuni zinazoandaliwa ni pamoja na:-

(i) **Kanuni ya Uogeshaji Mifugo.**

Wizara inatunga Kanuni hii ili kukabiliana na kuenea kwa magonjwa yaenezwayo na kupe na wadudu wengine; kukabiliana na tatizo la uogeshaji mifugo usioratibiwa/holela, gharama kubwa za uogeshaji; kutokuwepo kwa takwimu/tarifa za matumizi ya dawa za kuogesha mifugo; kutofanyika kwa upimaji wa nguvu ya dawa za kuogesha mifugo na maji ya josho; kutokuwepo kwa usajili na ukaguzi wa majosho; kutokuwepo kwa mgawanyo wa dawa kwa maeneo yenye usugu; umiliki usioeleweka wa majosho na hatari ya kuchukuliwa ardhi iliyotengwa kwa ajili ya majosho.

(ii) **Kanuni ya Uzalishaji, Uingizaji, Usambazaji na Uchanjaji wa mifugo**

Wizara inatunga Kanuni hii ili kuondoa changamoto za uzalishaji, uingizaji, usambazaji na utoaji wa chanjo nchini. Kasoro hizo ni kama gharama kubwa za utoaji chanjo; Mwingiliano katika usimamizi; Utunzaji hafifu wa taarifa na takwimu; kiwango kidogo cha uchanjaji na usiofikia maeneo yote kwa magonjwa ya kipaumbele; kutokuwepo kwa udhibiti wa uchanjaji wa mifugo nchini; na utunzaji wa chanjo.

(iii) **Kanuni ya Uhimilishaji, uhawilishaji kiinitete na matumizi ya madume bora.**

Wizara inatunga Kanuni hii ili kutatua changamoto zilizopo katika uzalishaji wa mifugo. Mfano, gharama kubwa ya uhimilishaji na uhawilishaji, Matumizi holela ya madume na mbegu; mapungufu katika utunzaji wa kumbukumbu; mapungufu katika mipango ya utambuzi na uhifadhi wa vinasaba vya mifugo bora; na kutokuwa na vyanzo vya uhakika vya utunzaji wa vinasaba.

(iv) **Kanuni ya Vitotoleshi na Kuku Wazazi *(Hatcheries and Breeding Flock Farms)***

Wizara inatunga Kanuni hii ili kuondoa mwingiliano wa majukumu ya wadau mbalimbali, kuweka bayana mamlaka, vigezo na viwango vya vitotoleshi vya vifaranga; kuweka utaratibu wa uanzishwaji wa vitotoleshi vya vifaranga; mashamba ya kuku wazazi, utunzaji wa mayai, vifaranga vya siku moja *(old day chicks)* na ufuatiliaji wa magonjwa. Pia, kuzingatia viwango vya afya ya wanyama na kuhuisha utoaji wa vibali sawa na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE); na kuweka viwango tofauti vya teknolojia ya uanzishaji wa vitotoleshi vya vifaranga na mashamba ya kuku wazazi.

(v) **Kanuni ya Ukamataji wa Mifugo**

Wizara inafanya mapitio ya Kanuni za ukamataji mifugo ili kuzuia ukamataji holela wa mifugo. Imejitokeza tabia ya baadhi ya wananchi na watendaji wa Serikali kukamata mifugo bila kuzingatia haki za mifugo ambazo zimeainishwa katika Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya Mwaka 2008 na Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya Mwaka 2003 pamoja na Kanuni zake. Ukiukwaji huu wa Sheria umeleta mateso makubwa kwa wanyama kwa kukosa huduma muhimu kama malisho, dawa, chanjo, na maji. Hali hii inasababisha mifugo mingi kufa ikiwa imeshikiliwa.

**37.** *Mheshimiwa Spika,* katika Mwaka 2019/2020 Wizara itaendelea kukamilisha Sheria na Kanuni zote za Mifugo ili kuboresha huduma za mifugo na mazao yake. Lengo kubwa ni kuhakikisha kuwa chanjo za mifugo zinapatikana kwa bei

nzuri kwa ajili ya wafugaji; kuondoa tatizo la dawa zilizoisha muda wake kuendelea kutumika; na kuzuia ukamataji holela wa mifugo.

**UZALISHAJI WA MIFUGO NA MAZAO YAKE**

**Uzalishaji na Usindikaji wa Zao la Maziwa**

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mifugo na mazao yake hapa nchini umeendelea kuongezeka ambapo idadi ya ng'ombe wa maziwa imeongezeka kutoka **1,100,000** mwaka 2017/2018 hadi **1,294,882** mwaka 2018/2019**.** Pia, katika kipindi cha mwaka 2018/2019, jumla ya mitamba ya ng'ombe wa maziwa **15,097** ilizalishwa na kusambazwa. Kati ya mitamba hiyo, **637** ilizalishwa kutoka katika mashamba ya Serikali **(Kiambatisho Na. 5)** na **14,460** kutoka Sekta binafsi ikilinganishwa na mitamba **13,735 (**Ikiwa ya Serikali **590** na Binafsi **13,145)** iliyozalishwa na kusambazwa mwaka 2017/2018**.**

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeanza kutekeleza mkakati wa miaka mitatu (**3**) kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2020/21 unaolenga kuzalisha mitamba **1,000,000** kwa mwaka kutokana na kuhimilisha ng'ombe wa asili **milioni 3** ili kuongeza uzalishaji wa maziwa. Mkakati huu ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Mifugo Tanzania (TLMP) ambao umeainisha kuwa ifikapo mwaka 2021/2022 idadi ya ng'ombe wa maziwa wanatarajiwa kuongezeka mara **3.8** kutoka **789,000** mpaka **2,985,000**.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mkakati huo, Wizara imeendelea kuimarisha kituo cha Uhimilishaji cha Taifa (NAIC) Usa River - Arusha kupitia Mradi wa Ushirikano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika kuboresha Uhimilishaji *(Public Private Partnership for Artificial Insermination Delivery - PAID)* kwa ufadhili wa taasisi ya Bill & Melinda Gates Foundation. Katika mwaka 2018/2019, kituo cha NAIC kimeendelea kuimarishwa kwa kupatiwa kichambuzi cha mbegu (*semen analyzer - CASA)* na madume bora matatu **(3)** aina ya Boran. Pia, mradi wa EU-IBAR umefadhili madume matatu (3) ya Sahiwal na hivyo kufikia madume **31**. Aidha, katika kutekeleza mkakati wa kuzalisha mitamba **1,000,000** kwa njia ya uhimilishaji mradi umenunua mitungi **71** ya kuhifadhi kimiminika cha naitrojeni (lita **35**), pikipiki **46** na vifaa vingine vya uhimilishaji.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019 Wizara ilitoa mafunzo kwa wataalam **389** wa uhimilishaji ikilinganishwa na Wataalam **204** waliopatiwa mafunzo hayo mwaka 2017/2018, ambalo ni ongezeko la asilimia **90.7.** Aidha, mauzo ya mbegu bora za ng'ombe *(semen)* yameongezeka kutoka shilingi **152,545,250** mwaka 2017/2018 hadi kufikia shilingi **350,218,560** mwaka 2018/2019, sawa na asilimia **129.6.**

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara itaendelea kuimarisha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji cha NAIC kwa kununua vitendea kazi ikiwa ni pamoja na kukarabati mabanda ya madume, kutengeneza mtambo wa kuzalisha kimiminika cha naitrojeni na kutoa mafunzo kwa wahimilishaji **600** kutoka mikoa ya Lindi, Mtwara, Dodoma, Singida, Simiyu, Shinyanga, Tabora, Kigoma, Katavi, Mwanza na Geita. Pia, Wizara itatoa mafunzo rejea kwa wahimilishaji **50** na waendesha mitambo saba (**7**). Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha vituo sita vya Kanda vya kuzalisha kimiminika cha Nitrojeni katika Mikoa ya Dodoma, Pwani, Lindi, Mbeya, Mwanza na Katavi kwa kufanya matengenezo na ukarabati wa mitambo.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu Mradi wa Uendelezaji wa Sekta ya Maziwa Afrika Mashariki (East Africa Dairy Development - EADD II) unaotekelezwa na Shirika la Heifer International. Mradi umetoa mafunzo ya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa katika nyanja za uzalishaji mifugo, ulishaji, afya ya mifugo na elimu ya ushirika kwa wafugaji **40,498** kutoka katika Mikoa ya Iringa, Mbeya na Njombe. Aidha, mradi umewezesha wafugaji wa Halmashauri za Rungwe, Busokelo, Iringa na Njombe kuunda na kuimarisha vyama vya Msingi vya Ushirika **35.** Kati ya hivyo, vyama **23** vya kutoka Rungwe vimeunda Chama Kikuu cha Ushirika kiitwacho Maziwa Cooperative Union (MCU). Vilevile, mradi umevijengea uwezo vyama vya Msingi vya Ushirika **26** kutoka Mkoa wa Songwe vinavyounda mtandao *(Songwe Dairy Cooperative Joint Entreprises).*

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa EADD II umeendelea kutekeleza Programu ya miaka mitano (2014 hadi 2019) ya Unywaji Maziwa Shuleni (*School Milk Feeding Program*) kwa lengo la kuwafikia wanafunzi **15,000** wa shule za awali na msingi ili kuboresha lishe na afya, kupunguza utoro, kuongeza ufaulu na kujenga utamaduni wa unywaji wa maziwa. Hadi kufikia Machi 2019, wanafunzi **16,849** kutoka katika shule **25** za Wilaya za Njombe, Mbeya na Wanging'ombe wanakunywa maziwa kwa ujazo wa mililita **200** kwa mtoto kwa siku kwa siku nne **(4)** za wiki. Program hii imechangia kuongeza udahili na mahudhurio ya wanafunzi katika shule husika yameongezeka kutoka asilimia **89.04** mwaka 2017/2018 hadi kufikia asilimia **95.6** mwezi Machi, 2019. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia **6.56**.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020 Wizara kwa kushirikina na mradi wa EADD II itaendelea kupanua wigo wa masoko ya maziwa kwa kuanzisha na kuendeleza vituo **10** vya ukusanyaji wa maziwa vyenye uwezo wa lita **34,000** kwa siku ili kusogeza soko la maziwa karibu na wafugaji wengi zaidi. Pia, mradi utaendelea kutekeleza program ya unywaji maziwa shuleni kwa kuongeza shule ili kuwafikia wanafunzi wengi zaidi katika maeneo ya mradi.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu uzalishaji wa maziwa hapa nchini ambapo katika mwaka 2018/2019 kiasi cha lita **bilioni 2.7** kimezalishwa ikilinganishwa na lita **bilioni 2.4** zilizozalishwa mwaka 2017/2018 sawa na ongezeko la asilimia **12.5**. Kati ya hizo, lita **bilioni 1.8** zilitokana na ng'ombe wa asili na lita **milioni 900** zilitokana na ng'ombe wa kisasa. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa idadi ya ng'ombe wa maziwa kutoka **1,100,000** hadi kufikia ng'ombe **1,294,882,** matumizi ya uhimilishaji na hali nzuri ya upatikanaji wa malisho na maji.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania imeendelea kuratibu na kusimamia usindikaji na biashara ya maziwa nchini. Katika Mwaka 2018/2019 usindikaji umeongezeka kutoka lita **milioni 56** Mwaka 2017/2018 hadi lita **milioni 66.9** Mwaka 2018/2019, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia **19.4.** Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa uwekezaji wa Sekta binafsi katika ujenzi wa viwanda vya kusindika maziwa ambapo viwanda vipya **14** vya Maziwa vimejengwa na kufanya jumla ya viwanda vya kusindika maziwa vinavyofanya kazi kote nchini kuwa **91** (**Kiambatisho Na.6**) ikilinganishwa na viwanda **76** vilivyokuwa vinafanya kazi Mwaka 2017/2018. Pia, vituo vya kukusanyia maziwa vimeongezeka kutoka vituo **184** mwaka 2017/2018 hadi vituo **195** mwaka 2018/2019.

**48.** ***Mheshimiwa Spika*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuhamasisha Sekta binafsi kuimarisha ukusanyaji na usindikaji wa maziwa kufikia **lita 284,500** kutoka **lita 154,100** kwa siku. Aidha, Wizara imeingia makubaliano (MoU) ya uwekezaji katika usindikaji kupitia Dawati la Sekta binafsi ili kuongeza usindikaji wa maziwa nchini.

**Uzalishaji na Usindikaji wa Zao la Nyama na Mayai**

**49.** *Mheshimiwa Spika,* Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia tasnia ya nyama nchini. Katika Mwaka 2018/2019, uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kutoka tani **679,992** mwaka 2017/2018 hadi kufikia tani **690,629** Mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la asilimia **1.54**. Aidha, katika Mwaka 2018/2019 ng'ombe **449,120** wamenenepeshwa ikilinganishwa na ng'ombe **322,030** walionenepeshwa Mwaka 2017/2018 ikiwa ni ongezeko la asilimia **39.47**. Ongezeko hilo limetokana na Wizara kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu unenepeshaji ili kutoa nyama nyingi na bora inayokidhi mahitaji ya soko. Hadi mwezi Machi, 2019 wafugaji **86** kutoka katika Halmashauri **17** za Wilaya mwaka 2018/2019 wamepatiwa mafunzo ya unenepeshaji.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuhamasisha wadau wa tasnia ya nyama kupitia mashamba darasa ya unenepeshaji ili kuwekeza kwenye ufugaji wa kisasa ukiwemo wa ranchi na unenepeshaji wa mifugo ili kufikia ng'ombe **550,000** kwa mwaka.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Nyama Tanzania imeendelea kufuatilia biashara ya nyama ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 jumla ya **tani 1,759.12** za nyama zenye thamani ya **Shilingi 9,498,468,816 (Dola za Marekani 3,957,695.34)** ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na kiasi cha **tani 2,608.93** zenye thamani ya **Dola za Marekani 5,679,217.28** zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2017/2018 ikiwa ni pungufu kwa asilimia **48.3**.

**52.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/2019, jumla ya **tani 516.63** za nyama zenye thamani ya Dola za Marekani **2,160,974.33** ziliingizwa kutoka nje ya nchi ikilinganishwa na **tani 1,401.96** za nyama zenye thamani ya Dola za Marekani **4,368,858.07** zilizoingizwa nchini katika Mwaka 2017/2018 sawa na upungufu wa **asilimia 63.15**. Upungufu huu umetokana na sababu mbalimbali ikiwemo Wizara kubadilisha Kanuni na Taratibu za usimamizi wa uingizaji na uuzaji wa bidhaa za mifugo kutoka nje ya nchi ili kuweka uwiano wa ushindani katika soko. Kiasi hicho cha nyama kiliingizwa kutoka nchini Kenya, Afrika Kusini, Ubelgiji na Uingereza. Katika mwaka 2019/20, Wizara itaendelea kusimamia Sheria, Kanuni na Miongozo ili wawekezaji waweze kuzalisha nyama yenye ubora wa kukidhi viwango na mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara imejenga na kukarabati minada kwa kujenga ukuta katika Mnada wa Mpakani wa Kirumi ulioko Butiama uliofunguliwa rasmi tarehe 16 Oktoba, 2018. Aidha, ujenzi wa jengo la ofisi ya mnada wa Kirumi litakalokuwa na huduma za kibenki unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2019. Kazi ya ujenzi wa sakafu katika mnada wa mpakani uliopo Wilaya ya Longido unaendelea na upo katika hatua za mwisho. Vilevile, ujenzi wa kituo cha Polisi na uzio katika mnada wa mpakani wa Buhigwe na uzio katika minada ya Kasesya na Nyamatala unaendelea na utakamilika mwezi Mei, 2019.

**Operesheni Nzagamba II**

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Mambo ya Ndani, Viwanda na Biashara (TBS), Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee, Walemavu na Watoto (TFDA), Ofisi ya Rais (TISS) na TAMISEMI imeendesha doria maalum (Operesheni Nzagamba Awamu ya II) ikiwa na lengo la:-

(i) Kudhibiti ukwepaji wa kulipa maduhuli ya Serikali kwenye biashara ya mifugo na mazao yake unaofanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu;

(ii) Kulinda viwanda vya ndani kwa kudhibiti uingizaji holela wa bidhaa mbalimbali zinazoingizwa nchini kinyume cha Sheria, Kanuni na Taratibu; na

(iii) Kuwalinda wananchi/walaji kwa kudhibiti uuzwaji wa bidhaa zisizokidhi viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango Tanzania na TFDA.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuelimisha wananchi, Operesheni Nzagamba Awamu ya II, 2018 imekuwa na mafanikio makubwa katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kudhibiti utoroshaji wa Mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi;
(ii) Kulinda afya ya watumiaji wa mazao ya mifugo na bidhaa zake;
(iii) Kuongeza Pato la Taifa (kutokana na utii wa kibiashara);
(iv) Kulinda ajira za watanzania;
(v) Kuvutia wawekezaji kwenye Sekta ya Mifugo; na
(vi) Kulinda raslimali za nchi.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika awamu hii, zoezi lililenga maeneo ya viwandani, minadani, mipakani, *supermarkets,* maeneo ya kupumzishia mifugo na vituo vya ukaguzi wa mifugo na maeneo mengine ya kimkakati. Operesheni hii ilifanyika nchi nzima kuanzia tarehe 9 Oktoba, 2018 hadi Machi, 2019. Aidha, ufuatiliaji huu umekuwa na mafanikio yafuatayo:-

(i) Jumla ya ngómbe **207,906,** mbuzi/kondoo **268,048**, nguruwe **1,356**, ngamia **10**, farasi **9**, punda **193** na sungura **102**; ngozi vipande **162** na mbwa **5** walikaguliwa na wamiliki kubainika kuwa na makosa mbalimbali (**Kiambatisho Na. 7**);

(ii) Jumla ya ngómbe **40,944**, mbuzi na kondoo **165,115** walikamatwa wakiwa wanatoroshwa kwenda nje ya nchi bila kulipiwa vibali na ushuru stahiki. Aidha, tani **26.3** za nyama na maziwa zilikamatwa zikiwa zimeingizwa nchini bila vibali, zilizokwisha muda wa matumizi na kuwa na ubora hafifu ambapo zote ziliteketezwa. Vilevile, vifaranga **27,600** na mayai **21,500** vilivyoingizwa nchini bila vibali vilikamatwa na kuharibiwa kwa mujibu wa Sheria;

(iii) Tani **12,555** za mashudu, tani **2,223** za pumba na tani **45** za dagaa (malighafi ya chakula cha mifugo) zilikaguliwa zikisafirishwa kwenda nje ya nchi kwa kupitia maeneo mbalimbali. Aidha, tani **25,425** za vyakula vya mifugo zilikamatwa zikisafirishwa kwenda nje ya nchi bila vibali. Pia, jumla ya katoni **118** za madawa ya mifugo zilikamatwa zikiuzwa katika maeneo yasiyosajiliwa na bila kuzingatia utaalam katika mikoa ya Kigoma, Tabora na Arusha zikiuzwa katika maeneo yasiyosajiliwa na bila kuzingatia utaalam.

**57.** ***Mheshimiwa Spika***, kabla ya Operesheni Nzagamba II makusanyo ya Wizara kwa mwezi Julai hadi Septemba, 2018 yalikuwa ni wastani wa shilingi **1,147,592,640.47** kwa mwezi. Aidha, wakati wa kipindi cha Operesheni, mwezi Oktoba hadi Desemba, 2018 mapato yaliongezeka na kufikia wastani wa shilingi **3,139,309,528** kwa mwezi. Hii ina maana kuwa bila udhibiti huu, Serikali inapoteza wastani wa shilingi **bilioni 2** kwa mwezi**.**

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** faida za operesheni Nzagamba ni kuongezeka kwa mapato ya Serikali, kulinda viwanda na wazalishaji wa ndani na kuleta ushindani ulio sawa, kulinda afya za walaji, kuchochea uwekezaji katika Sekta ya Mifugo ambapo viwanda vingi hivi sasa vinajengwa, upatikanaji wa bei nzuri, soko la uhakika, kuongezeka kwa uelewa na utii wa Sheria bila shuruti.

**59.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kusimamia na kudhibiti uingizaji holela wa mazao na pembejeo za mifugo kutoka nje ya nchi, kuelimisha wafanyabiashara kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za uendeshaji wa biashara ya mazao ya mifugo, kudhibiti matumizi ya bidhaa zisizokuwa na ubora, kuzuia utoroshaji wa malighafi za mifugo, kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali na kuweka mifumo thabiti ya kusimamia biashara ya mifugo na mazao yake.

**Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)**

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) imetekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kutunza jumla ya ng'ombe **14,590**, mbuzi **2,829**, kondoo **2,477**, nguruwe **144** na farasi **27**. Aidha, Kampuni ilizalisha na kukuza ndama **4,606** kutokana na ng'ombe wazazi **5,703** ikilinganishwa na ndama **4,269** waliozalishwa na kukuzwa mwaka 2017/2018.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** NARCO imenunua ng'ombe **1,343**


HOTUBA YA WIZARA YA UFUGAJI NA UVUVI

wenye thamani ya shilingi **bilioni 1.05** kati ya hao ng'ombe **313** ni wazazi walionunuliwa kutoka Mzalishaji wa nyama 'Overland' na kupelekwa West Kilimanjaro na ng'ombe **1,030** kwa ajili ya kunenepesha kwa kutumia vyakula vya ziada kwa ajili ya nyama bora na hivyo kuwa sehemu ya soko la uhakika kwa wafugaji nchini ikilinganishwa na ng'ombe **1,175** walionunuliwa mwaka 2017/2018.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, NARCO imeuza ng'ombe **3,598** wenye thamani ya shilingi **bilioni 2.572** ikilinganishwa na ng'ombe **3,149** wenye thamani ya shilingi **bilioni 2.078** waliouzwa katika mwaka 2017/2018. Vilevile, uuzaji wa nyama bora (Kongwa Beef) kiasi cha **Tani 305.097** umefanyika hivyo kujipatia mapato ya jumla ya shilingi **1,983,135,170.**

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni imetoa ushauri wa kitaalam kwa wafugaji **439** katika vijiji **52** vinavyozunguka ranchi za Kampuni katika ranchi za Kongwa (vijiji **10**), Ruvu (vijiji **12**), West Kilimanjaro (vijiji **7**), Kagoma (vijiji **6**), Kalambo (vijiji **8**), Missenyi (vijiji **7**) na Mkata (vijiji **2**).

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kupunguza changamoto ya upatikanaji wa malisho na kuboresha uhusiano kati ya Kampuni na jamii za wafugaji wanaozunguka maeneo ya ranchi, Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) imetenga vitalu **122** vyenye ukubwa wa hekta **59,290** vitakavyopangishwa kwa muda mfupi**.** Hadi kufikia Aprili, 2019 vitalu **92** vimeshapangishwa ambapo ng'ombe **31,356** wanalishwa. Aidha, Kampuni inawakaribisha wafugaji kupangisha vitalu **30** vilivyobaki vyenye uwezo wa kulisha ng'ombe **8,780**.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza azma ya kuendeleza ufugaji wenye tija, Kampuni ilitangaza vitalu **122** kwa ajili ya uwekezaji wa mifugo wa muda mrefu. Vitalu hivi vina jumla ya hekta **59,290.** Hadi sasa, jumla ya vitalu **92** vyenye **ng'ombe 31,356** vimepangishwa kwa muda mfupi. Aidha, jumla ya vitalu **30** bado havijapata wawekezaji (**Kiambatisho Na. 8**).

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Kampuni imetenga jumla ya shilingi **95,000,000** kwa ajili ya kuchangia huduma za kijamii katika vijiji vinavyozunguka ranchi. Kati ya fedha hizo shilingi **50,000,000** zitajenga na kukarabati majosho na shilingi **45,000,000** zitajenga miundombinu ya maji katika maeneo hayo. Katika mwaka 2019/2020, Kampuni ya NARCO imepanga kuzalisha ng'ombe **4,791** na mbuzi/kondoo **1,399** na kuzalisha na kuuza nyama tani **323.6**.

**Uzalishaji wa Kuku**

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuratibu na kusimamia uzalishaji wa nyama na mayai kutokana na kuku wa asili na wa kisasa, ambapo vituo vya kutotolesha vifaranga vimeongezeka kutoka vituo **10** mwaka 2017/2018 hadi kufikia vituo **19** mwezi Aprili, 2019. Vituo hivyo **19** viko katika mikoa ya Dar es Salaam (**4**), Iringa (**2**), Njombe (**1**), Pwani (**6**), Kilimanjaro (**3**), Arusha (**1**) na Mwanza (**2**). Aidha, mashamba ya kuku wazazi nchini yameongezeka kutoka **6** hadi **16** katika kipindi hicho yenye uwezo wa kutunza zaidi ya kuku wazazi **1,000,000**. Katika mwaka 2018/2019, jumla ya vifaranga **50,928,000** vimezalishwa na kusambazwa nchini, ambapo vifaranga **47,328,000** ni wa nyama, vifaranga **1,896,000** ni vya kuku chotara hususan *Sasso* na *Kroiler* na vifaranga **1,704,000** ni vya kuku wa mayai. Aidha, Wizara ilitoa vibali maalum kwa Kampuni **13** kuingiza vifaranga vya kuku wazazi **556,616** wa nyama na mayai kutoka nchi za Uholanzi, Uingereza, Ufaransa, Zambia na India. Pia, jumla ya mayai ya kutotolesha vifaranga vya nyama **360,000** yaliingizwa nchini kutoka Zambia. Katika mwaka 2019/2020 Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia uzalishaji wa kuku vifaranga na mayai.

**Uzalishaji wa Nguruwe**

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019 Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ufugaji na biashara ya nguruwe. Hadi mwezi Aprili, 2019 jumla ya tani **37,773** za nyama ya nguruwe zimezalishwa ikilinganishwa na tani **37,191** zilizozalishwa mwaka 2017/2018. Ongezeko hilo limetokana na kukua kwa soko na wafugaji kuendelea kuwekeza katika ufugaji wa nguruwe.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji, usindikaji na biashara ya nguruwe. Aidha, Wizara itahimiza sekta binafsi kuzalisha na kusambaza mbegu bora za nguruwe kwa wafugaji ili kuongeza uzalishaji wa nguruwe na bidhaa zake. Pia, Wizara itaendelea kuimarisha Chama cha Wazalishaji Nguruwe nchini TAPIFA kwa lengo la kuboresha kosaafu za nguruwe. Vilevile, Wizara itaendelea kuimarisha shamba lake la nguruwe la Ngerengere ili liweze kuendelea kuzalisha mbegu bora za nguruwe.

**Zao la Ngozi**

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia uendelezaji wa tasnia ya ngozi hapa nchini. Katika mwaka 2018/19 jumla ya kilo **5,384,735.79** za ngozi **ghafi,** zilizosindikwa kufikia hatua ya kati (*wet blue*) na bidhaa za ngozi zenye thamani ya **shilingi 8,165,356,495.28** zimesafirishwa kwenda katika nchi za Ethiopia, China, Pakistani, Kenya na India. Kati ya hizo, **kilo 935,286.50** zilizosindikwa (wet blue) zenye thamani ya **shilingi 1,808,412,620.41** ni za ngozi ya ng'ombe, **kilo 386,135** zilizosindikwa (wet blue) zenye thamani ya **shilingi 788,964,283.46** ni ngozi za mbuzi na kondoo kilo 16,594.00 ni ngozi zilizochakatwa (crust leather) zenye thamani ya shilingi **40,185,479** na kilo **20,985.54** ni bidhaa za ngozi zenye thamani ya shilingi **146,177,818.00** zilizosafirishwa kwenda nje ya nchi.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, ngozi ghafi za ngo'mbe zenye uzito wa kilo **3,636,700.06** zikiwa na thamani ya shilingi **4,687,562,544.21** na mbuzi/kondoo **kilo 274,234.96** zenye thamani ya shilingi **535,552,749.70** zimeuzwa katika nchi za Nigeria na Ghana Pia, jumla ya **kilo 114,800** za ngozi zilizosindikwa za punda zenye thamani ya shilingi **157,201,000** zimeuzwa China na Vietnam**.** (**Kiambatisho Na. 9a).**

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini inaonesha kuwa uwezo wa uzalishaji wa viatu vya ngozi nchini ni takriban **jozi 1,200,000** kwa mwaka kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 9c** ukilinganisha na mahitaji ya viatu takriban jozi **milioni 54.2** kwa sasa. Kutokana na takwimu hizo uwekezaji mkubwa unahitajika katika tasnia ya ngozi kwa kuwa kuna fursa nyingi. Hata hivyo, tasnia hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

(i) Ubora hafifu wa ngozi ghafi zinazozalishwa nchini;
(ii) Ushindani wa soko la ndani kwa bidhaa za ngozi zinazozalishwa nchini unaotokana na wingi wa uingizwaji wa bidhaa za ngozi zinazozalishwa nje ya nchi kama mitumba na ngozighushi *(synthetic leather);*
(iii) Utoroshwaji wa ngozi ghafi kwenda nje ya nchi kupitia njia zisizo halali;
(iv) Udanganyifu wa thamani halisi ya ngozi ghafi na zilizosindikwa *(Wet Blue)* unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu; na
(v) Uhaba wa wataalam katika sekta ya ngozi hivyo kuathiri usindikaji na ubora wa bidhaa za ngozi.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019 Wizara kupitia mfuko wa ngozi (LDF) imetekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Ngozi (*Leather Sector Development Strategy 2016 - 2020)* kwa kufanya kikao cha wadau **25** wa tasnia ya ngozi kujadili changamoto zinazoikabili tasnia ya ngozi. Pia, Wizara imeendesha mafunzo ya ubora wa ngozi kwa wakaguzi wa ngozi **26** kutoka mikoa yote ya Tanzania bara.

**MATUMIZI YA RASILIMALI ZA ARDHI, MAJI NA MALISHO KWA MIFUGO**

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa mkakati wa upatikanaji wa uhakika wa malisho na maji na inakamilisha maandalizi ya miongozo ya usimamizi wa rasilimali hizo. Aidha, Wizara inaendelea kuhamasisha na kuwezesha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji. Katika mwaka 2018/2019 Wizara inaendelea kukamilisha ujenzi wa bwawa la Mbangala (Songwe), lambo katika Kijiji cha Chamakweza (Bagamoyo) na Visima virefu katika Vijiji vya Mpapa (Manyoni) na Nsolanga-Ismani (Iringa). Pia, Wizara imekamilisha ukarabati wa bwawa la Nyakanga (Butiama) na inaendelea na ukarabati wa lambo katika Kijiji cha Wami -Dakawa (Mvomero) na hivyo kufanya idadi ya mabwawa/malambo kufikia **1,384** na visima virefu **103.**

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuimarisha upatikanaji wa maji kwa mifugo kwa kufanya ukarabati wa malambo sita (6) katika mikoa ya Manyara, Pwani, Simiyu, Arusha, Geita na Tabora na kuchimba visima virefu 50.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha lishe na upatikanaji wa uhakika wa malisho, Wizara inaendelea kutoa elimu kwa wafugaji na wadau wengine kuhusu uzalishaji na uhifadhi wa malisho. Katika mwaka 2018/2019, jumla ya marobota **550,919** ya hei yalizalishwa kutoka katika mashamba ya Serikali ikilinganishwa na marobota **482,246** yaliyozalishwa mwaka 2017/2018 (**Kiambatisho Na. 10**). Ongezeko hilo la asilimia **14.2** limetokana na uboreshaji wa mashamba.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019 jumla ya tani **12.1** za mbegu bora za malisho zilizalishwa kutoka katika mashamba ya Serikali ikilinganishwa na tani **10** zilizozalishwa mwaka 2017/2018. Aidha, jumla ya hekta **730** za mbegu za nyasi na hekta **245** za mbegu za mikunde kutoka mashamba ya TALIRI, LMUs – Sao Hill na Mabuki zimestawishwa; Mashamba ya Malisho Vikuge na Langwira pia yameimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi. Aidha, wafugaji na wawekezaji wenye mashamba binafsi wamehamasishwa na wamestawisha hekta **197** za nyasi na hekta **35** za mikunde katika mashamba yao. Vilevile, mashamba ya malisho **208** yameendelezwa katika Halmashauri **32**. Katika mwaka 2018/2019, mashamba darasa ya malisho **67** yamestawishwa kwa kupanda malisho aina ya nyasi ekari **72,** mikunde ekari **16** na malisho mchanganyiko ekari **48** katika Halmashauri 17 za Mpanda, Nsimbo, Nkasi, Tunduru, Mbarali, Lushoto, Maswa, Itilima, Meatu, Chato, Muleba, Butiama, Bunda, Morogoro, Rungwe, Njombe na Mufindi, ambapo wafugaji **1,756** wamefikiwa na kupatiwa mafunzo.

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaongeza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za malisho kwa kuimarisha na kupanua mashamba saba **(7**) ya Serikali. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa mbegu bora za malisho na kusimamia urasimishaji wa mbegu aina tano (5) kupitia vituo vya Utafiti na Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu *(Tanzania Official Seed Certification Institute – TOSCI).* Mbegu hizo ni Buffel, Rhodes, Lucerne, Lablab na Blue pea.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara ilifanya ukaguzi wa maeneo ya kuzalisha, kuhifadhi na kuuza vyakula vya mifugo ambapo viwanda **22** vilikidhi vigezo na kusajiliwa hivyo kufanya viwanda vilivyosajiliwa kote nchini kuongezeka kutoka **72** mwaka 2017/2018 hadi viwanda **94 (Kiambatisho Na. 11).** Katika kipindi hicho, wakaguzi **15** kutoka Mikoa ya Mwanza, Simiyu na Mara walijengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ya ukaguzi wa vyakula vya mifugo. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kusimamia na kudhibiti ubora wa vyakula vya mifugo kwa kufanya ukaguzi wa viwanda, maeneo ya kuuzia na kutoa mafunzo kwa wakaguzi **50** na watengenezaji **20.** Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu uzalishaji na uhifadhi wa vyakula vya mifugo.

**Utatuzi wa Migogoro baina ya Wafugaji na Watumiaji wengine wa Ardhi**

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** migogoro baina ya wafugaji na wakulima, wafugaji na wahifadhi, wafugaji na mashamba ya Serikali na watumiaji wengine wa ardhi imekuwepo kwa muda mrefu katika mikoa mbalimbali hapa nchini. Migogoro hiyo imekuwa ikisababisha madhara mbalimbali ikiwemo vifo vya binadamu na mifugo, uharibifu wa mali na uvunjifu wa amani, wafugaji kukamatwa na wakati mwingine mifugo yao kutaifishwa na kuuzwa. Hadi kufikia Oktoba, 2017 kulikuwa na migogoro **428** iliyowahusisha wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi katika mikoa mbalimbali hapa nchini**.**

**81.** *Mheshimiwa Spika,* katika kutatua migogoro hiyo, Wizara yangu imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

(i) Kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Kutafuta Ufumbuzi wa Kudumu wa Migogoro ya Wafugaji na Watumiaji wengine wa Ardhi,

(ii) Kuunda timu ya Wataalam kutoka OR-TAMISEMI; OR – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Wizara za Mambo ya Ndani; Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na Chama cha Wafugaji Tanzania kwa lengo la kutatua migogoro katika mikoa mbalimbali nchini. Timu ilifanya kazi katika Mikoa mitano (5) katika Wilaya za Uvinza, Kasulu na Kibondo (Kigoma); Tanganyika na Mlele (Katavi); Kalambo, Nkasi na Sumbawanga (Rukwa); Chunya na Mbarali (Mbeya); na Mkuranga, Kibiti, Rufiji na Kisarawe (Pwani), ambapo migogoro **27** kati ya **43** sawa na asilimia **59.26** ilitatuliwa. Kazi hii inaendelea katika maeneo mengine yaliyobainika kuwa na migogoro.

(iii) Kutafuta na kuainisha maeneo kwa ajili ya malisho ya mifugo ambapo Wizara imetenga jumla ya hekta **373,076.05 (Kiambatisho Na. 12)** kutoka katika maeneo yake ya vituo vya kupumzishia mifugo, Ranchi za Taifa, Mashamba ya TALIRI na Mashamba ya Kuzalisha Mifugo (LMUs) ili yatumiwe na wafugaji kwa utaratibu maalum. Pia, Halmashauri tano (**5**) za Tunduru, Mpanda, Biharamulo, Muleba na Kyerwa zimetenga jumla ya hekta **199,827.3 (Kiambatisho Na. 13)** kwa ajili ya malisho ya mifugo na hivyo kupunguza migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini.

(iv) Wizara pia imeanzisha Kurugenzi kwa lengo la kuendeleza na kusimamia maeneo ya malisho, vyanzo vya maji kwa mifugo na rasilimali za vyakula vya mifugo na hivyo kusaidia katika utatuzi wa migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa Ardhi.

**82.** *Mheshimiwa Spika,* Wizara yangu inatoa shukrani za dhati kwa **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Agizo alilolitoa tarehe 15 Januari, 2019 kwa Mawaziri nane (8). Agizo hilo lilihusisha OR – TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mifugo na Uvuvi; Kilimo; Maliasili na Utalii; Maji; na Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kushirikiana kwa pamoja kufuatilia migogoro iliyopo na kuitafutia ufumbuzi.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Asasi zisizo za Kiserikali kwa kutoa elimu ya uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Wizara kupitia mradi wa Usimamizi Endelevu wa Nyanda za Malisho *(Sustainable Range Management Project-SRMP)* imetenga hekta **172,218.87** za maeneo ya malisho ya pamoja *(Joint Village Land Use Plans)* katika Halmashauri za

# HOTUBA YA WIZARA YA UFUGAJI NA UVUVI

Chemba, Kiteto na Chalinze. Aidha, katika Mwaka 2018/2019 jumla ya Vijiji **42** vimetenga hekta **80,823.26** kwa ajili ya malisho katika Wilaya **9 (Kiambatisho Na. 14).** Hadi sasa Vijiji **1,852** vimeandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kati ya Vijiji **12,545** vilivyopo nchini ambapo maeneo ya malisho hekta **2,788,901.17** yametengwa kwa ajili ya ufugaji katika Mikoa **22.**

**84.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, wadau na Mamlaka nyingine za Serikali kuendelea kutenga na kupima maeneo ya malisho. Pia, itaandaa miongozo ya utumiaji na usimamizi wa maeneo hayo.

**UDHIBITI WA MAGONJWA YA MIFUGO**

**85.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara iliandaa na kuanza kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti Magonjwa ya Mifugo, Matumizi ya Dawa, Chanjo na Viuatilifu vya Mifugo nchini. Ili kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe nchini Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutoa elimu na hamasa. Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili 2019, jumla ya michovyo **40,352,228** imefanyika. Kati ya michovyo hiyo, ng'ombe ni **22,400,170**, Mbuzi ni **12,836,389** na Kondoo ni **5,115,669**. Ili kuchochea zoezi la uogeshaji nchini Wizara ilitoa dawa lita **8,823.53 aina ya Paranex (Alphacypermethrin) yenye thamani ya shilingi 300,000,000 na kuzigawa katika majosho 1,486** yanayofanya kazi katika Mikoa **24**. Vilevile, ili kudhibiti ubora wa dawa za kuogeshea nchini Wizara kupitia TVLA imenunua kifaa cha kupima ubora wa dawa ya kuogeshea mifugo (HPLC) kwa shilingi **120,000,000.** Katika Mwaka 2019/2020 Wizara **itaendelea kuhamasisha uogeshaji na kutoa dawa ya kuogesha mifugo kwa majosho yote yatakayokuwa yanafanya kazi kila baada ya miezi sita.**

**86.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019 Wizara inakarabati majosho **161** kwa gharama ya shilingi **235,113,200** katika mikoa 21 nchini **(Kiambatisho Na.15a)**. Aidha, Wizara imehamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kukarabati majosho ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 jumla ya majosho **151** yalikuwa yamekarabatiwa. Pia, Wizara inazitaka Halmashauri zote nchini kutekeleza **Agizo la Chato** la kukarabati majosho yote nchini ifikapo mwezi Juni, 2019. Halmashauri zote nchini ambazo hazitatekeleza agizo hili zitanyang'anywa mamlaka ya kukusanya mapato yatokanayo na mifugo na mazao yake (**Kiambatisho Na. 15b**). Vilevile, jumla ya Kamati **847** za kusimamia majosho zimeundwa na kufungua akaunti za uendeshaji (**Kiambatisho Na.15c**). Katika mwaka 2019/2020 Wizara itaendelea kuhamasisha uogeshaji na kutoa dawa yenye ruzuku ya kuogesha mifugo kwa majosho yote yatakayokuwa yanafanya kazi kila baada ya miezi sita **(6)** kuanzia Desemba, 2018.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa kutokomeza magonjwa mbalimbali yenye athari kijamii na kiuchumi. Magonjwa hayo ni pamoja na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo, Homa ya Mapafu ya Ng'ombe, Mafua Makali ya Ndege, Mdondo, Homa ya Nguruwe, Chambavu, magonjwa yaenezwayo na Kupe (Ndigana Kali, Ndigana Baridi, Maji Moyo na Mkojo Mwekundu), Kimeta, Ugonjwa wa Kutupa Mimba na ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa. Aidha, kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, Sekta binafsi na Washirika wa Maendeleo Wizara inahamasisha na kutekeleza uchanjaji wa mifugo. Kwa kipindi cha mwaka 2018/2019 jumla ya ng'ombe **milioni 3.9 (9.6%)**, mbuzi **milioni 2.3 (7.8%)** na mbwa **milioni 0.3 (7.5%)** wamechanjwa dhidi ya magonjwa mbalimbali. Vilevile, dozi **milioni 46.9 (41.7%)** zilitolewa kwa kuku wa asili dhidi ya mdondo na kuku wa kisasa dozi **milioni 121.8** dhidi ya Mdondo, **milioni 75 (57%)** Gumboro na **milioni 1.8 (100%)** Mareks **(Kiambatisho Na.**16). Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuhamasisha, kuratibu na kusimamia uchanjaji wa mifugo dhidi ya magonjwa mbalimbali.

**88.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Washirika wa Maendeleo imeendelea kutekeleza Mikakati ya kutokomeza magonjwa yanayoambukiza binadamu kutoka kwa wanyama kwa dhana ya Afya Moja. Magonjwa hayo ni pamoja na Malale, Mafua Makali ya Ndege, Kimeta, Ugonjwa wa Kutupa Mimba, Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa na Homa ya Bonde la Ufa. Aidha, kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, Sekta binafsi na Washirika wa Maendeleo Wizara inahamasisha na kutekeleza uchanjaji wa mifugo.

**89.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaweka utaratibu wa manunuzi ya pamoja ya chanjo pamoja na dawa za kuogesha mifugo ili kupunguza gharama za manunuzi. Pia, itakijengea uwezo Kiwanda cha Chanjo za Mifugo cha Serikali kilichopo Kibaha (Tanzania Vaccine Institute - TVI) ili kiweze kuzalisha aina saba **(7)** za chanjo za magonjwa kutoka aina tano **(5)** za chanjo zinazozalishwa. Aina saba za chanjo ni pamoja na M*dondo (New Casttle Disease)*, Kimeta (*Anthrax*), Chambavu *(Black Quarter)*, Ugonjwa wa Kutupa Mimba *(Brucellosis)*, Homa ya Mapafu ya Ng'ombe *(CBPP)*, Homa ya Mapafu ya Mbuzi *(CCPP)* na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo *(PPR)*. Vilevile, Wizara itaendelea kusimamia na kufuatilia Usalama wa Chakula ili kulinda afya za walaji wa mazao ya mifugo na kukuza biashara ya mazao ya mifugo Kimataifa. Aidha, ili kurahisisha biashara hii, Wizara imekusudia kutengeneza mfumo wa kuomba vibali kwa njia ya kielektroniki na kuhuisha Sheria na Kanuni za ukaguzi na usafirishaji wa mifugo na mazao yake nchini na nje ya nchi.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) imezalisha dozi **39,548,000** za chanjo za magonjwa ya mifugo kati ya lengo la kuzalisha dozi **100,000,000** kwa mwaka ikilinganishwa na dozi **28,427,100** zilizozalishwa na kusambazwa mwaka 2017/2018. Kati ya dozi hizo, **38,245,800** ni za Mdondo ($1_2$), **1,114,850** ni za Kimeta na **187,850** ni za Chambavu ambapo zote zimesambazwa kupitia vituo saba **(7)** vya TVLA katika kanda ambapo Halmashauri tatu **(3)** za Mkalama, Kondoa na Longido na wasambazaji binafsi **599** wananunua katika vituo hivyo na kuwahudumia wafugaji. Kiwango cha chanjo zilizoagizwa kutoka nje ya nchi ni dozi **26,840,000** za Homa ya Mapafu ya ngómbe (CBPP), dozi **182,000** za Homa ya mapafu ya mbuzi (CCPP), dozi **1,074,230** za Kichaa cha Mbwa (Rabies), dozi **122,505,000** za Mdondo, dozi **2,500** za Kutupa mimba (Brucellosis), dozi **457,000** za Sotoka ya Mbuzi (PPR), dozi **103,984,500** za *Gumboro* na dozi **7,000,000** za *Mareks*.

**91.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) imeanza usajili wa chanjo mchanganyiko wa Kimeta na Chambavu (TECOBLAX) baada ya kufaulu vipimo vya ubora kutoka Maabara ya PANVAC Ethiopia. Aidha, majaribio ya chanjo ya Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP) yamekamilka na sampuli za chanjo zimepelekwa PANVAC kwa ajili ya kupimwa ubora ili hatimaye chanjo hii isajiliwe na ianze kuzalishwa. Pia, maandalizi ya kutengeneza chanjo ya Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Mbuzi (CCPP) na Ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi (PPR) ikiwa ni pamoja na kufundisha wataalam na kununua vifaa yameanza. Lengo ni kuanza kufanya majaribio ya uzalishaji wa chanjo hizo ifikapo mwezi Mei, 2019. Vilevile, ujenzi wa jengo la kuzalisha chanjo za Bakteria unaendelea katika kituo cha kuzalisha chanjo cha Kibaha (TVI) ambapo umekamilika kwa asilimia **45.**

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia TVLA imefanya uchunguzi wa sampuli **8,016** kutoka kwa mifugo**.** Uchunguzi wa sampuli hizo ulibaini uwepo wa magonjwa ya Kimeta, Ndigana Kali, Ndigana Baridi, Homa ya Nguruwe, Mdondo, Gumboro, na Homa ya Mapafu ya Ng'ombe**.** Aidha, jumla ya sampuli **2,861** za vyakula vya mifugo na malighafi zilifanyiwa uchambuzi ambapo asilimia **75** ya sampuli hizo zilionekana kuwa na ubora unaotakiwa. Pia, Wafugaji na watengenezaji wa vyakula vya mifugo walipewa ushauri wa namna ya kudhibiti magonjwa na kuboresha vyakula vya mifugo. Vilevile, Wizara kupitia TVLA imeendelea kufanya tafiti za namna ya kudhibiti magonjwa na teknolojia za kuangamiza mbun'go waenezao magonjwa ya Nagana na Malale.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, TVLA inapanga kuzalisha dozi **milioni 111** za chanjo za mifugo ikiwa ni pamoja na dozi **100,000,000** za chanjo ya Mdondo ya TEMEVAC I2; 5,000,000 za chanjo ya CBPP; **3,000,000** za chanjo ya Kimeta na **3,000,000** za chanjo ya Chambavu. Aidha, Wakala inapanga kuanza majaribio ya kuzalisha chanjo dhidi ya ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (CCPP), chanjo dhidi ya Kichaa cha Mbwa na Chanjo ya Mapele Ngozi (LSD).

**UTAFITI, MAFUNZO NA UGANI WA MIFUGO**

**Utafiti wa Mifugo**

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) imefanya tafiti nane (**8**) vituoni na kwa wafugaji. Tafiti hizo zimefanyika katika Mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mwanza, Simiyu, Dodoma, Pwani, Morogoro, Singida, Lindi Mtwara na Kigoma kwa lengo la kuboresha mbari za ng'ombe wa maziwa na nyama, kuku, mbuzi na kondoo, uzalishaji wa punda, malisho bora na vyakula vya mifugo. Aidha, utaratibu wa ununuzi wa vifaa vya maabara ya viinitete iliyopo TALIRI Mpwapwa vyenye thamani ya shilingi **milioni 189** kupitia Mradi wa Uhawilishaji wa Viinitete *Multiple Ovulation and Embryo Transfer, (MOET)* unaofadhiliwa na Serikali ya Tanzania kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) unaendelea. Manufaa ya teknolojia hii ni:-

(i) Kuwezesha ng'ombe jike kuzalisha viinitete **8** mpaka **450** kwa mwaka;

(ii) Kuzalisha, kuhifadhi na kufungasha viinitete kwa ajili ya uhimilishaji na uhawilishaji; na

(iii) Kuongeza kasi ya uzalishaji wa mifugo nchini hasa mitamba na madume kwa ajili ya maziwa na nyama (ndama **50** kwa mwaka kwa ng'ombe mmoja**).**

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TALIRI, kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), imeendelea kufanya ufuatiliaji wa tija ya ng'ombe wa maziwa ambapo Halmashauri **24** nchini zimeendelea kutekeleza Mradi wa Kuboresha Mbari za Ng'ombe wa Maziwa (*African Dairy Genetic Gain, ADGG*). Halmashauri hizo ni Tanga Jiji, Muheza, Korogwe Mji, Moshi, Rombo, Hai, Siha, Arusha Jiji, Meru, Arusha, Iringa Manispaa, Mufindi, Mafinga Mji, Njombe Mji, Makambako Mji, Mbeya Jiji, Mbeya, Mbozi, Iringa, Rungwe, Lushoto na Bumbuli. Kupitia mradi huu, wafugaji **8,347** wamepata elimu ya ufugaji bora na wanatembelewa kila mwezi. (**Kiambatisho Na. 17).**

**96.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19, Wizara kupitia TALIRI kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la PASS trust (*Private Agricultural Sector Support*) imeanzisha mkakati wa kuwajengea uwezo vijana na kuwavutia kuingia katika ufugaji wa kibiashara. Aidha, ujenzi wa miundombinu yenye uwezo wa kuweka mbuzi **4,000** kwa ajili ya kunenepesha kwa mwaka umekamilika. Pia, mradi huu utawajengea uwezo vijana **20** kwa mwaka kufuga kibiashara.

**97.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TALIRI kwa kushirikiana na mradi wa Kuboresha Mbari za Kuku (*African Chicken Genetic Gain, ACGG*), ilisambaza kuku **468** na mayai **720** kwa wafugaji **1,801**. TALIRI kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo katika maeneo k*ame (International Centre for Agricultural Research in Dry land Areas, ICARDA*) imeendelea kuimarisha tafiti za kuainisha vinasaba vya kuongeza uzalishaji wa nyama katika mbuzi wa asili kwa kuimarisha maabara ya uhimilishaji wa mbuzi katika Kituo cha West Kilimanjaro. Aidha, Mafunzo ya uhimilishaji wa mbuzi kwa wataalamu 18 yametolewa. Vilevile, kupitia Mpango wa Huduma za Jamii na Uhusiano (*Corporate Social Responsibility*) TALIRI ilisambaza teknolojia mbalimbali **27** katika Halmashauri **41** nchini na kuwafikia wadau **23,659** wakiwemo wataalam wa ugani **127**, wanafunzi **346** wa vyuo vya LITA, SUA, Visele na MATI; na wafugaji **23,186** walioko vijiji vya jirani na vituo vya TALIRI kupitia semina za mafunzo.

**98.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia TALIRI itaendelea kuibua, kutathmini na kuendeleza utafiti wa mifugo na malisho ikiwa ni pamoja na kuendeleza kosaafu bora za mifugo ili kuongeza tija katika uzalishaji wa maziwa, nyama, mayai na ngozi kuendana na mnyororo wa thamani na uchumi wa viwanda. Aidha, miundombinu ya mashamba ya Utafiti katika vituo saba **(7)** ikiwemo ujenzi wa Makao Makuu ya TALIRI utafanyika. Pia, uzalishaji wa mbuzi wa nyama na maziwa kupitia uhimilishaji hadi kufikia mbuzi **1,500** na unenepeshaji wa mbuzi **4,000** kwa kushirikiana na PASS utafanyika. Vilevile, TALIRI itashirikiana na Kiwanda cha Maziwa cha Tanga Fresh kuzalisha malisho kwa njia ya umwagiliaji. Aidha, TALIRI ina upungufu wa watumishi **221** ambapo katika Mwaka 2019/2020, imeomba ajira ya watumishi **74** ili kukabiliana na upungufu mkubwa wa Rasilimali Watu.

**Mafunzo ya Mifugo**

**99.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (Livestock Training Agency – LITA) imefanya udahili wa wanachuo **2,536**. Aidha, wanafunzi **580** kutoka vyuo vya Serikali na **398** kutoka vyuo binafsi wanatarajia kuhitimu mafunzo ya Stashahada na Astashahada mwezi Juni, 2019. Vilevile, wafugaji **156** walipatiwa mafunzo katika Kampasi za Wakala juu ya uzalishaji bora wa mifugo na malisho. Pia, Wizara kupitia LITA kwa ushirikiano na Wizara ya Mambo ya Nje ya Jamhuri ya Poland imekarabati mabweni manne **(4)** na Kiwanda kidogo cha kusindika maziwa katika Kampasi ya Tengeru. Aidha, jumla ya mitamba **15** ya maziwa yenye thamani ya Shilingi **22,000,000** imenunuliwa kwa ajili ya Kampasi ya Madaba ili kuongeza uzalishaji wa maziwa na mafunzo. Katika Mwaka 2019/2020 LITA imeomba ajira ya watumishi **239** ili kukabiliana na upungufu mkubwa wa Rasilimali Watu.

**Huduma za Ugani wa Mifugo**

**100.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na sekta binafsi ilitoa elimu kwa Maafisa Ugani na **wafugaji 19,839** kupitia mafunzo rejea, ziara za mafunzo, mikutano ya uhamasishaji na semina zilizoendeshwa wakati wa maonesho ya Nanenane, Sabasaba na Siku ya Chakula Duniani. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa wadau juu ya ufugaji bora kwa njia ya vitabu **9,396**, vipeperushi **29,350**, mabango **1,850**, vipindi **52** vya redio na 12 runinga.

101 ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za Wizara kutekeleza mikakati yake, ilibainisha uhitaji mkubwa wa maarifa na stadi mpya za ufugaji bora kwa wataalam na wafugaji nchini ili kuongeza na kuboresha uzalishaji wa mazao ya mifugo sambamba na falsafa ya uchumi wa viwanda nchini. Wizara imeanza kutoa Mafunzo Rejea kwa Wafugaji na Maafisa Ugani kutoka katika Halmashauri 185 nchini. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wataalam walioko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuamsha ari ya uwajibikaji na kuongeza ufanisi wa utoaji huduma bora za ugani kwa

# HOTUBA YA WIZARA YA UFUGAJI NA UVUVI

wafugaji.

102 ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo hayo pia yanalenga kuwaongezea wafugaji maarifa kwa kuwapatia teknolojia mpya ili kuhamasisha Ufugaji wa Kisasa na Kibiashara nchini. Mpango huu unalenga kuongeza uzalishaji wa malighafi zitokanazo na mifugo zenye viwango bora ili kukidhi mahitaji ya Viwanda vya nyama, maziwa na ngozi vinavyoendelea kujengwa nchini. Mafunzo haya yalizinduliwa mwezi Aprili, 2019 katika Wilaya za Simanjiro na Kaliua ambapo wafugaji **1,840** na Maafisa ugani **65** walipatiwa mafunzo na hivi sasa mafunzo yanaendelea nchi nzima.

103 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma za ugani na kusambaza teknolojia sahihi za ufugaji bora kupitia mashamba darasa, mafunzo rejea, pamoja na maonesho ya Nanenane, Sabasaba na Siku ya Chakula duniani. Aidha, Wizara itatoa mafunzo rejea ya ufugaji wa Kisasa na Kibiashara kwa Maafisa Ugani 1,500 na Wafugaji 80,000 kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Pia, Wizara itaanzisha na kusimamia mashamba darasa 90 ya malisho katika Halmashauri 30 nchini. Vilevile, Wizara itaendelea kuhamasisha wafugaji kuanzisha na kusimamia vyama vya ushirika vya wafugaji ili kuwa na sauti moja na kutetea haki zao.

**Usimamizi wa Uzalishaji wa Mazao ya Mifugo**

**Bodi ya Maziwa**

104 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa imefanya Ukaguzi katika Mikoa ya Songwe, Tanga, Mbeya, Morogoro na Dar es Salaam. Ukaguzi umefanyika katika vituo 42 vya kukusanyia maziwa, viwanda 20 vya kusindika maziwa, Vioski vya maziwa 19 na maghala 12 ya kuhifadhi maziwa kutoka nje ya nchi. Aidha, Bodi imesajili wadau wapya 63 (wazalishaji wa maziwa 25, wakala wa masoko 23, waingizaji maziwa kutoka nje ya nchi 7 na wasindikaji wa maziwa 8). Wadau hao ni kutoka katika Mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa, Pwani, Kilimanjaro, Shinyanga, Arusha,Tanga, Dodoma na Dar es Salaam. Pia, Bodi imefanya marekebisho ya Kanuni za Maziwa chini ya usimamizi wa Wizara ili kuongeza ufanisi na kuondoa muingiliano wa Kisheria na Kanuni na Taasisi za Serikali zinazosimamia **tasnia ya maziwa.**

105. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Maziwa, imetoa mafunzo kwa wadau 148 katika Mikoa ya Mbeya, Songwe, Morogoro, Tanga na Dar es Salaam yaliyohusisha wazalishaji 88, wakusanyaji na wasafirishaji 56 na wasindikaji wanne (4) wa maziwa. Pia, kwa kipindi cha Julai 2018 hadi Machi, 2019, Bodi ya Maziwa imetoa vibali 692 na kuingiza maziwa lita 18,617,659.07 zenye thamani ya shilingi 26,224,025,033.80 ikilinganishwa na maziwa lita 20,920,537.59 zenye thamani ya shilingi 30,290,485,222 zilizoingizwa kipindi kama hiki kwa mwaka 2017/2018 sawa na upungufu wa asilimia 11.01. Aidha, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa imeendelea kuimarisha vyama vya ushirika 18 vya maziwa katika Mikoa ya Tanga, Morogoro, Pwani, Mbeya na Dar es Salaam kwa lengo la kuvijengea uwezo wa ukusanyaji maziwa ili kuongeza upatikanaji wa maziwa kwenye viwanda vilivyopo.

106 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa itaendelea kuimarisha na kuongeza vituo 50 vya kukusanyia maziwa katika maeneo yanayozalisha maziwa mengi katika Mikoa ya Geita (Bukombe na Chato); Iringa (Mufindi na Mafinga); Mara (Bunda); Mbeya (Rungwe na Busokelo); Morogoro (Mvomero); Njombe (Makete na Ludewa); Pwani (Chalinze na Mkuranga); Rukwa (Kalambo); Ruvuma (Mbinga na Madaba); Simiyu (Meatu); Shinyanga (Kahama) na Tanga (Kilindi). Aidha, kituo cha kukusanyia maziwa cha mfano kinatarajiwa kujengwa Mkuranga na Bodi ya maziwa itasimamia ujenzi wa mabanda bora kwa wafugaji watakaokopeshwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB).

**Bodi ya Nyama**

107 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Bodi ya Nyama imetambua na kusajili wadau 179 kutoka katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kagera, Dodoma, Mwanza, Lindi, Kilimanjaro na Arusha. Pia, minada tisa (9) ya mifugo kutoka katika Mkoa wa Singida imetambuliwa na kusajiliwa. Aidha, watumishi 12 wa Bodi wamepewa mafunzo ya kutumia mfumo wa usajili na kutafuta masoko kielektroniki ambapo taarifa za usajili za wadau 404 kutoka Mikoa ya Dar es Salaam (137), Iringa (57), Morogoro (31), Singida (142), Tabora (7) na Mtwara (1) zimeingizwa kwenye mfumo huo. Vilevile, Wizara kupitia Bodi imeendelea kutoa mafunzo ya kutumia mfumo wa usajili na kutafuta masoko kielektroniki katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ambapo wadau 50 walipatiwa mafunzo. Aidha, machinjio/viwanda 15, Karo 25 na Bucha 203 katika Mikoa ya Dodoma (Dodoma Jiji, Dodoma MC na Chamwino); Arusha (Arusha Jiji na Arusha DC); Mwanza (Mwanza Jiji, Ilemela na Magu); Shinyanga (Shinyanga MC) na Kilimanjaro (Moshi MC) zimekaguliwa na wamiliki wamehamasishwa kuboresha miundombinu. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Nyama itatoa mafunzo ya kutumia mfumo wa usajili wa wadau kielektroniki kwa watumishi **52** kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Mara na Mwanza. Aidha, mafunzo ya uzalishaji na uuzaji wa nyama kwa kuzingatia taratibu za usafi yatatolewa kwa wadau wa tasnia ya nyama **150** kutoka Mikoa ya Simiyu, Singida, Manyara, Tabora, Songwe na Njombe. Pia, mafunzo ya Kilimo Biashara na teknolojia ya uzalishaji wa mifugo kwa wafugaji **180** wa ng'ombe, mbuzi, nguruwe, kuku, kondoo na punda yatatolewa. Vilevile, wadau **1,000** wa tasnia ya nyama na vyama vyao watatambuliwa na kusajiliwa.

**Usimamizi wa Viwango vya Huduma ya Afya ya Mifugo na Maadili ya Wataalam**

108 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Baraza la Veterinari imefanya ukaguzi katika Mikoa **24**. Katika ukaguzi huo vituo vya kutoa huduma ya afya ya mifugo **800** vilikaguliwa**.** Aidha, Baraza lilifanya kaguzi katika minada minane **(8)** ya mifugo ambapo wauzaji holela **21** wa dawa za mifugo walikamatwa, kutozwa faini kwa mujibu wa Sheria na kupewa elimu ya namna bora ya utoaji wa huduma ya afya ya mifugo. Pia, Baraza limesajili madaktari wa mifugo 42 kati ya madaktari **60** waliotarajiwa kusajiliwa. Idadi ya madaktari wa mifugo waliosajiliwa sasa imefikia **900.** Vilevile, wataalam wasaidizi wa afya ya mifugo **337** wenye Stashahada na Astashahada waliandikishwa na kuorodheshwa katika kipindi hicho na kufanya idadi ya wataalam wasaidizi walioandikishwa na kuorodheshwa kufikia **3,218.**

109 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Baraza la Veterinari imetoa leseni za kutoa huduma kwa wakaguzi wa nyama **54,** wataalam wa maabara za veterinari watano **(5)** na wahimilishaji tisa **(9)**. Aidha, vituo **111** vya kutolea huduma ya afya ya mifugo vimesajiliwa kati ya vituo **400** vinavyotarajiwa kusajiliwa hadi kufikia mwezi Juni, 2019. Pia, vyuo vitatu **(3)** vya kutolea mafunzo ya mifugo vya *Tanzania Research and Career Development Institute (TRACDI)*, Dodoma; *Institute of Development and Entrepreneurship Studies* (DIDES), Dodoma na *Mahinya College of Sustainable Agriculture* (Ruvuma) vilikaguliwa kwa lengo la kutambuliwa. Hata hivyo, vyuo hivyo vimetakiwa kukamilisha taratibu kabla ya kutambuliwa.

110 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Baraza la Veterinari itasajili madaktari wa mifugo **70,** vituo vya huduma za mifugo **400,** kuorodhesha wataalam wasaidizi **500** na kuandikisha wasaidizi wa wataalam **500.** Aidha, Baraza litatoa leseni kwa wakaguzi wa nyama, wahimilishaji na wataalam wa maabara za veterinari **210** na litafanya ukaguzi wa maadili na viwango vya utoaji huduma kwa kushirikiana na Halmashauri **185** nchini. Pia, Baraza kwa kushirikiana na Baraza la Veterinari la Afrika Kusini na Shirika la Afya ya Wanyama Ulimwenguni litaendelea na mafunzo ya kuwajengea uwezo watendaji wake katika kusimamia utoaji wa huduma ya afya ya mifugo nchini. Vilevile, kwa kushirikiana na Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Jamii ya Chuo Kikuu cha Sokoine Cha Kilimo, Baraza litatoa mafunzo ya kujiendeleza ya miezi mitatu **(3)** kwa watoa huduma wa afya ya mifugo **300.**

**UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA MIFUGO**

111 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Serikali kupitia Wizara imeweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji katika ujenzi wa viwanda vya utengenezaji wa chanjo na uchakataji wa mifugo na mazao yake nchini. Uwekezaji huo umefanywa katika miradi ifuatayo:-

(i) Ujenzi wa jengo la kuzalishia chanjo za aina ya bakteria katika Kiwanda cha Serikali cha uzalishaji Chanjo cha Kibaha (TVI). Gharama ya jengo hilo ni shilingi **milioni 667**. Jengo hilo linatarajia kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2019.

(ii) Ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kuzalisha chanjo za mifugo cha *Hester Bioscience Africa Limited* cha Kibaha. Kiwanda hicho kitazalisha chanjo 27 zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Gharama za uwekezaji wa Kiwanda hicho ni **Dola za Marekani milioni 18** sawa na shilingi **bilioni 41**. Kiwanda hiki kinatarajiwa kuanza kuzalisha chanjo ifikapo Februari 2020.

(iii) Kiwanja cha TAN CHOICE (Kibaha-Pwani) chenye uwezo wa kuchakata ngómbe **1,000** na mbuzi/kondoo **4,500** kwa siku na uwekezaji wake ni **Dola za Marekani milioni 5.5** sawa na shilingi **bilioni 12.5** na kinatarajiwa kuanza kazi mwezi Septemba, 2019. Kiwanda hicho pia kinatarajia kutoa ajira zaidi ya wafanyakazi 500.

(iv) Kiwanda cha *Elia Food and Overseas Ltd* (Longido) chenye uwezo wa kuchakata ng'ombe **400** na mbuzi/kondoo **2,000** kwa siku ujenzi wake ni Dola za Marekani **milioni 5** sawa na shilingi **bilioni 11.3** kitaanza kufanya kazi mwezi Septemba, 2019. Kiwanda hicho kinategemea kutoa ajira zaidi ya wafanyakazi 200.

(v) Kiwanda cha *Galaxy Food and Beverage Limited* (Jijini Arusha) cha kusindika maziwa, kina uwezo wa kusindika lita **75,000** kwa siku na kimeajiri jumla ya wafanyakazi 30 kwa kuanzia. Gharama za uwekezaji wa kiwanda hicho ni Dola za Marekani **milioni 2.5** sawa na shilingi **bilioni 5.7.** Kiwanda hicho tayari kimeshaanza kuzalisha maziwa (Kilimanjaro Fresh) kwa kiwango cha *UHT* tangu mwezi Machi, 2019.

(vi) Viwanda vya nyama vya SAAFI (Rukwa), Tanganyika Parkers (Shinyanga na Mbeya) na Kiwanda cha maziwa cha Utegi na Musoma Dairy. Serikali inatafuta Wawekezaji mahiri wa kuvifufua na kuviendesha viwanda hivyo.

(vii)

(viii)***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia NARCO imesaini Hati ya Makubaliano ya utekelezaji wa Mradi wa *Integrated Rural Development Project (IRDP)* katika Ranchi ya Ruvu na Kampuni ya *National Egyptian Company for Africa Investment (NECAI)* kwa ajili ya uwekezaji mkubwa utakaogharimu **Dola za Marekani milioni 50** sawa na shilingi za Tanzania **bilioni 111**. Mradi wa ujenzi wa machinjio kubwa na ya kisasa utaweza kuchinja ng'ombe **1,500** na mbuzi/kondoo **4,500** kwa shifti moja ya saa nane. Viwanda vingine vitakavyojengwa kwenye mnyororo mzima wa mifugo ni pamoja na Kiwanda cha Ngozi kitakachoweza kusindika ngozi hadi kupata bidhaa zake.

**112.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa Jamii wa PSSSF imepanua Kiwanda cha kuzalisha bidhaa za ngozi cha Gereza la Karanga ili kiweze kuongeza uzalishaji kutoka jozi **150** hadi kufikia jozi **400** za viatu kwa siku. Uboreshaji huu umekamilika mwezi Septemba, 2018 na kiwanda kimeanza kufanya kazi.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** uwekezaji huu utaondoa changamoto zilizopo hivi sasa za wafugaji kutangatanga kutafuta masoko ya mifugo, kukosa bei nzuri, kupoteza fedha nyingi za kigeni kuagiza mazao ya mifugo kutoka nje ya nchi, kupoteza ajira na mapato ya Serikali. Katika mwaka 2019/20 Wizara itaendelea kuhamasisha na kusimamia uwekezaji katika Sekta ya Mifugo kwa kuendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji nchini.

**C: SEKTA YA UVUVI**

**HALI YA SEKTA YA UVUVI**

**114.** ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Uvuvi ni miongoni mwa sekta za kiuchumi ambazo ni muhimu katika kuondoa umasikini na kukuza uchumi wa Taifa kwa ujumla. Sekta hii ina mchango mkubwa katika kuwapatia wananchi ajira, chakula, lishe, kipato na fedha za kigeni. Katika mwaka 2018, Sekta ya Uvuvi ilichangia asilimia **1.71** katika pato la Taifa na imekua kwa asilimia **9.2.**

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** zaidi ya watanzania **milioni 4.5** wameendelea kupata kipato cha kila siku kutokana na shughuli zinazohusiana na Sekta ya Uvuvi ikiwemo kuunda na kutengeneza boti, kushona nyavu, ukuzaji viumbe maji, biashara ya samaki na mazao yake na mama lishe. Kwa upande wa lishe, samaki huchangia takriban asilimia **30** ya protini inayotokana na wanyama. Aidha, ulaji wa samaki kwa sasa katika nchi yetu kwa mtu kwa mwaka ni kilo **8.2** ikilinganishwa na kilo **20.3** zinazopendekezwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO, 2018), hali hii inaonesha bado kuna uhitaji mkubwa wa kitoweo aina ya samaki.

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** taarifa za tafiti zilizofanyika kwa vipindi tofauti katika mwaka 2018/2019 zinaonesha kwamba, kiasi cha samaki kilichopo katika maji yetu ni tani **2,803,000** kwa mtawanyiko ufuatao: Ziwa Victoria tani **2,210,000**, Ziwa Tanganyika tani **295,000** na Ziwa Nyasa tani **168,000**, Maji madogo (maziwa madogo ya kati, mito na mabwawa) tani **30,000** na Maji ya Kitaifa ya Bahari ya Hindi tani **100,000** (**Kiambatisho Na. 18**).

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, jumla ya wavuvi **202,053** wanaotumia vyombo vya uvuvi **58,930** walishiriki moja kwa moja kwenye shughuli za uvuvi. Nguvu hii ya uvuvi iliwezesha kuvunwa kwa tani **389,459.40** za samaki zenye thamani ya shilingi **trilioni 1.83.** Kati ya tani zilizovunwa katika mwaka 2018/2019, tani **333,782.32** (asilimia **85.70**) ni kutoka maji baridi na tani **55,677.08** (asilimia **14.30**) ni kutoka maji bahari (**Kiambatisho Na. 19).**

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, wakuzaji viumbe maji **26,474** walishiriki moja kwa moja kwenye shughuli za ukuzaji viumbe maji na kuzalisha jumla ya tani **18,073.6**. Kati ya tani hizo, tani **16,288** ni za samaki, tani **336.4** ni za kambamiti, tani **1,449** ni za mwani na tani **0.2** ni za kaa pamoja na vipande **395** vya lulu. Aidha, jumla ya vifaranga vya samaki **17,301,076** vilizalishwa.

# HOTUBA YA WIZARA YA UFUGAJI NA UVUVI

**119.** *Mheshimiwa Spika,* Sekta ya Uvuvi imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi, ukosefu na uchakavu wa miundombinu ya uvuvi, uwekezaji mdogo katika uvuvi wa Bahari Kuu, Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 kutokidhi mahitaji ya sasa, upatikanaji wa vifaranga na vyakula vya samaki vyenye ubora, uhaba wa wataalam katika ngazi mbalimbali za utumishi na upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

**120.** *Mheshimiwa Spika,* katika kukabiliana na changamoto hizi Wizara imeandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo: mapitio ya Sheria ya Uvuvi na kuandaa Sheria mpya ya kuendeleza Ukuzaji viumbe Maji; Mkakati wa Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi Nchini; Mkakati wa Kujenga na Kuboresha Miundombinu ya Uvuvi; Mkakati wa Kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO 2018); Mkakati wa kuendeleza tasnia ya ukuzaji viumbe maji; Mkakati wa Kusimamia Samaki aina ya Jodari; na Kuanzishwa kwa Dawati la Sekta Binafsi; Mpango wa Usimamizi wa Samaki wanaopatikana katika Tabaka la Juu la Maji, Usimamizi wa Uvuvi wa Kambamiti; na kusimamia rasilimali ya Pweza. Pia, Wizara inafanya mapitio ya Mpango Kabambe wa usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi Tanzania (Tanzania Fisheries Master Plan).


**MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/2019**

**Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2018/2019**

**121.** *Mheshimiwa Spika,* kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara kupitia sekta ya uvuvi ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi **21,534,305,600.00**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 kiasi cha shilingi **30,330,063,743.25** sawa na asilimia **140.8** ya lengo zilikuwa zimekusanywa kutoka Sekta ya Uvuvi.

**122.** *Mheshimiwa Spika,* fedha hizi zimekusanywa kutoka vyanzo vifuatavyo: leseni za kusafirisha samaki na mazao yake (Export Licences); leseni za uingizaji mazao ya uvuvi (Import Licences); ushuru wa mrabaha (Export Royalty); Mrabaha wa kuingiza mazao ya uvuvi nchini (Import Royalty), leseni za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa bahari Kuu, Tozo ya Maabara; leseni za uvuvi wa kambamiti, mauzo ya vifaranga vya samaki na faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa sheria za uvuvi.

**MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19**



**Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2019/2020**

**123.** *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Fungu 64 inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi **32,301,458,400.** Vyanzo vikuu vya fedha hizo ni pamoja na; leseni za kusafirisha samaki na mazao yake (Export Licences); leseni za uingizaji mazao ya uvuvi (Import Licences); ushuru wa mrabaha (Export Royalty); Tozo ya Maabara; mauzo ya vifaranga vya samaki; mauzo ya mazao ya uvuvi na faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa sheria za uvuvi.

**Fedha Zilizoidhinishwa**

**124.** *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Fungu 64 ilitengewa jumla ya Shilingi **21,093,086,000.00**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **13,966,406,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **7,126,680,000.00** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.Matumizi ya Bajeti ya Kawaida.

**125.** *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2018/2019, Fungu 64 lilitengewa jumla ya shilingi **13,966,406,000**. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2019, jumla ya shilingi **11,135,859,951** zilikuwa zimetolewa, sawa na asilimia **79.7** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi **6,794,398,181** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Wizara (PE) na shilingi **4,341,461,770** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo**

**126.** *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa 2018/2019, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa kiasi cha shilingi **7,126,680,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwa ni fedha za ndani na nje. Kati ya fedha hizo Shilingi **3,000,000,000.00** ilikuwa ni fedha za ndani na shilingi **4,126,680,000.00** ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2019, jumla ya shilingi **4,012,643,853.20** kutoka vyanzo vya nje zilitolewa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

**MAENEO YA VIPAUMBELE KATIKA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2018/2019 NA KATIKA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

**127** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020, Wizara imeainisha maeneo ya vipaumbele katika Mpango na Bajeti ya Wizara kupitia Sekta ya Uvuvi Fungu 64. Utekelezaji wake utafanyika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuhakikisha kwamba Sekta ya Uvuvi inachangia kikamilifu katika kuifikisha nchi yetu kwenye uchumi wa viwanda. Vipaumbele hivyo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha usimamizi, udhibiti na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi pamoja na kutunza mazingira;
(ii) Kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali yatokanayo na Sekta ya Uvuvi;
(iii) Kuimarisha usimamizi wa rasilimali katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu;
(iv) Kuimarisha usimamizi na uthibiti wa ubora, usalama na viwango vya samaki na mazao ya uvuvi;
(v) Kuimarisha Miundombinu na kukuza biashara ya Mazao ya Uvuvi;
(vi) Kuboresha upatikanaji wa taarifa sahihi za Uvuvi;
(vii) Kuongeza upatikanaji wa vifaranga vya samaki;
(viii) Kuandaa kanda za ufugaji wa samaki;
(ix) Kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi; na
(x) Kuimarisha Utafiti, Huduma za Ugani na Mafunzo ya Uvuvi.

**UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KATIKA MWAKA 2018/2019 NA MPANGO WA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

**SERA NA SHERIA**

**128.** *Mheshimiwa Spika,* Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2015 kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uendelezaji, uhifadhi, matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na utunzaji wa mazingira nchini. Katika mwaka 2018/2019, Wizara imechapisha nakala **2,000** za Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 katika lugha ya Kiswahili na jumla ya nakala **1,702** zimesambazwa kwa wadau.

**129.** *Mheshimiwa Spika,* Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni mbalimbali za uvuvi zikiwemo Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009; Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya Mwaka 1994; Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu Na. 1 ya Mwaka 1998 na Marekebisho yake ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009 na Marekebisho yake ya Mwaka 2016; na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Na. 11 ya mwaka 2016.

**130.** *Mheshimiwa Spika,* katika kuhakikisha kwamba Sheria inayosimamia Sekta ya Uvuvi inakidhi mahitaji yaliyopo kwa sasa, Wizara imeamua kuifumua Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009, ambapo itazaliwa Sheria mpya ya Uvuvi na Sheria Mpya ya Ukuzaji Viumbe Maji. Hivi sasa timu ya wataalam wa Wizara imekusanya maoni ya wadau na taasisi mbalimbali nchi nzima ambapo jumla ya wadau **2,156** (watu Binafsi **56**, Vikundi **2,088.** Wizara **6** na Taasisi **8**) wameshiriki kutoa maoni yao. Vilevile, Wizara imeendelea kufanya mapitio ya Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya Mwaka 1994 ili kupanua maeneo ya hifadhi hadi kwenye maji baridi. Pia, imeendelea kufanya maboresho ya Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu Na. 1 ya Mwaka 1998 na marekebisho yake ya Mwaka 2007.


**131.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/2019, Wizara imefanya marekebisho ya dharura ya baadhi ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009 ili kuliwezesha Taifa kunufaika na rasilimali za uvuvi. Miongoni mwa marekebisho hayo ni kuruhusu matumizi ya nyavu za milimita nane (**8**) badala ya kumi (**10**) kwa uvuvi wa dagaa katika ukanda wa bahari, matumizi ya nyavu za makila zenye ukubwa wa macho ya kuanzia inchi saba (**7**) badala ya inchi sita (**6**), uvunaji wa kaa kutoka gramu 500 hadi gramu 450, kuondoa ukomo wa urefu wa sentimita **85** kwa samaki aina ya Sangara, na pia matumizi ya leseni moja kwa kila eneo la maji ya uvuvi badala ya kila Halmashauri kutoa leseni yake. Marekebisho haya yamefanywa chini ya GN Na. 383 ya tarehe 10 Mei ya mwaka 2019 **(Kiambatisho Na. 20).**

**132.** *Mheshimiwa Spika*, marekebisho haya yatawezesha wananchi wa Ukanda wa Pwani kuvua dagaa aina ya mchele kwa kutumia nyavu za milimita nane (8) ambao walikuwa hawawezi kuvuliwa kwa kutumia nyavu za milimita kumi (10) zilizokuwepo kwa mujibu wa Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009, kuwezesha kuvua samaki aina ya Sangara wenye urefu wa zaidi ya sentimita 85 na kuondoa usumbufu wa kukata leseni kwa kila Halmashauri. Matokeo ya marekebisho haya ni pamoja na kuongeza kipato cha wavuvi, kuongezeka malighafi viwandani, kuvutia uwekezaji mpya, kudhibiti utoroshaji wa mazao ya uvuvi na kuongeza mapato ya Serikali. Aidha, Wizara imefanya marekebisho haya baada ya utafiti wa kina na ushirikishwaji wa wadau kwa lengo la kuondoa kasoro zilizokuwepo.

**133.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020, Wizara itakamilisha mapitio ya Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003, Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya Mwaka 1994, Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu Na. 1 ya Mwaka 1998 na marekebisho yake ya Mwaka 2007 na kuandaa Muswada wa Sheria mpya ya Uendelezaji Ukuzaji Viumbe Maji. Aidha, Wizara itaandaa kanuni za kutekeleza Sheria hizi.

**MWENENDO WA UVUNAJI WA RASILIMALI ZA UVUVI**

**134.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kusimamia uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi nchini. Hadi kufikia mwezi Machi 2019 jumla ya tani **389,459.40** za samaki zenye thamani ya shilingi **trilioni 1.83** zilivunwa ikilinganishwa na tani **376,352.72** zenye thamani ya shilingi **trilioni 1.77** zilizovunwa katika kipindi kama hiki mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia **3 (Kiambatisho Na. 21).** Aidha, kutokana na juhudi kubwa iliyofanywa na Wizara katika kudhibiti matumizi ya zana na uvuvi haramu, katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2019 kumekuwa na ongezeko la samaki wanaovunwa ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2018 (**Kielelezo Na.1).**




**Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi 2019**

**135.** *Mheshimiwa Spika,* Wizara imeendelea kusimamia biashara ya samaki na mazao ya uvuvi ndani na nje ya nchi kwa kuzingatia viwango vya kitaifa, kikanda, kimataifa na mahitaji ya soko. Aidha, hadi kufikia mwezi Machi 2019, tani **38,114.72** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **46,098** wenye thamani ya shilingi **bilioni 491.15** waliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani **34,425.56** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **100,110** wenye thamani ya shilingi **bilioni 402.57** waliouzwa nje ya nchi katika kipindi kama hiki mwaka 2018. Aidha, hadi kufikia Machi 2019 mauzo haya yameliingizia Taifa mrahaba wa shilingi **bilioni 15.63** ikilinganishwa na kiasi cha shilingi **bilioni 9.5** katika kipindi kama hiki mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia **64.5 (Kiambatisho Na. 22 na Kiambatisho Na.23).** Ongezeko hili limetokana na kuimarishwa kwa udhibiti na usimamizi wa biashara ya samaki na mazao ya uvuvi uliofanyika kupitia operesheni mbalimbali dhidi ya uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi.

**136.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/2019, kati ya tani **38,114.72** za mazao ya uvuvi zilizouzwa nje ya nchi, tani **36,670.93** ambazo ni sawa na **asilimia 96.21** zilitoka Ziwa Victoria. Sehemu kubwa ya mchango huu inatokana na biashara ya samaki aina ya sangara na mazao yake (tani **28,975.08** zenye thamani ya shilingi **bilioni 346.56**) ambayo ni sawa na asilimia **76.02** ya mauzo yote **(Kiambatisho Na. 24a na 24b)**. Aidha, tani **1,138.27** zenye thamani ya shilingi **bilioni 14.98** kutoka Ukanda wa Bahari ya Hindi ziliuzwa nje ya nchi (**Kiambatisho Na. 25**). Pia, mauzo ya samaki na mazao yake kutoka maziwa ya Tanganyika, Nyasa, na Rukwa ambayo yaliuzwa nje ya nchi ni kiasi cha tani **284.44** zenye thamani ya shilingi **bilioni 2.15** sawa na asilimia **1** ya mauzo yote**.**

**137.** *Mheshimiwa Spika,* hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2019, jumla ya tani **7,760.12** za samaki zenye thamani ya shilingi **bilioni 15.34** zimeingizwa nchini ikilinganishwa na tani **23,806.11** zenye thamani ya shilingi **bilioni 46.98** zilizoingizwa nchini katika kipindi kama hiki mwaka 2018 **(Kiambatisho Na 26).** Uingizaji wa samaki kutoka nje umepungua kwa asilimia **67.4** ikilinganishwa na mwaka 2017/2018. Hii imetokana na kuongezeka kwa uvunaji wa samaki katika maji ya asili, ufugaji wa samaki na udhibiti wa uingizaji holela wa samaki kutoka nje ya nchi.

# HOTUBA YA WIZARA YA UFUGAJI NA UVUVI

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa takwimu za Uvuvi kwa kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa takwimu kwa njia ya kielectroniki ikiwemo matumizi ya simu za viganjani. Katika mwaka 2018/2019 Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Uvuvi ya Ziwa Victoria (LVFO) imeandaa mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za Uvuvi kwa njia ya simu ujulikanao kama e-CAS (electronic catch Assessment Survey). Katika majaribio ya kutumia mfumo huo jumla ya simu **108** zimetolewa kwa maafisa Uvuvi kutoka Halmashauri za Wilaya zenye maeneo ya Uvuvi katika Ziwa Victoria, Ukanda wa Bahari ya Hindi na Ziwa Tanganyika. Ugawaji wa simu ulifanyika sambamba na kutoa mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu za Uvuvi kwa kutumia simu.

**139.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kusimamia uvunaji endelevu wa rasilimali za uvuvi na biashara ya mazao ya uvuvi nchini. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na nchi jirani ikiwemo nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, SADC na IOC - IOTC kutekeleza mikakati mbalimbali ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika maji ya pamoja.

**USIMAMIZI NA UDHIBITI WA RASILIMALI ZA UVUVI**

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara imeandaa na kutekeleza Mkakati wa Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi Nchini. Mkakati huu unalenga kuongeza ufanisi katika usimamizi, ulinzi, uendelezaji na uhifadhi wa rasilimali za uvuvi na mazingira yake pamoja na udhibiti wa uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi. Katika kutekeleza mkakati huu, Wizara imeanzisha Kanda kuu tatu (**3**) za Usimamizi na Udhibiti wa Rasimali za Uvuvi katika Ukanda wa Ziwa Victoria (**1**), Tanganyika (**1**) na Ukanda wa Pwani (**1**). Aidha, Wizara imeanzisha kanda ndogo mbili (**2**) za Ukerewe na Sengerema na kuimarisha Vituo **27** vilivyopo vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi kote nchini.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Mkakati huu, katika mwaka 2018/2019 Wizara imeendesha operesheni mbalimbali zenye siku kazi **10,914** zenye lengo la kuimarisha usimamizi na udhibiti wa uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi. Operesheni hizo ni pamoja na Sangara 2018 Awamu ya III ilifanyika katika Ukanda wa Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Bwawa la Mtera na Nyumba ya Mungu yenye sikukazi **4,170**, MATT iliyofanyika Bahari ya Hindi yenye sikukazi **1,500** na doria za kawaida zilizofanyika nchi nzima zenye sikukazi **5,244**.


**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** Matokeo ya Operesheni hizo ni kukamatwa kwa zana haramu mbalimbali zikiwemo nyavu za makila **168,708**, makokoro **3,715**, nyavu za timba **15,915**, nyavu za dagaa **9,068**, kamba za kokoro zenye urefu wa mita **525,784**, ndoano **568,958**, mitumbwi/boti **2,291**. Pia, samaki wazazi kilo **8,958**, samaki wachanga/kayabo kilo **110,181**, mabondo kilo **634.01**, magari **4,489**, Pikipiki **374**, mitungi ya gesi **236** na watuhumiwa **4,713**. Kati ya watuhumiwa hao wapo Viongozi **17.** (**Kiambatisho Na.27**).

**143.** ***Mheshimiwa Spika***, aidha, Wizara ilikamata jumla ya tani **15.53** za samaki walioingizwa nchini bila nyaraka, leseni na vibali. Samaki hao walipatikana na viambata vya sumu baada ya kufanyiwa uchunguzi ambapo samaki wote waliteketezwa kwa kutokukidhi viwango vya ubora na usalama. Vilevile, jumla ya raia wa kigeni **203** walikamatwa wakijihusisha na shughuli za uvuvi na biashara za mazao ya uvuvi kinyume cha sheria.

**144.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Operesheni Sangara 2018 Awamu ya II iliyofanyika mwaka 2017/2018 katika Ukanda wa Ziwa Victoria, mvuvi maarufu, ambaye alikamatwa na kikosi cha operesheni wilayani Sengerema kwa kosa la kukutwa na nyavu haramu za uvuvi vipande **24,000,** ndoano haramu **1,547,000** na mabunda **6** ya makokoro ambapo alitakiwa kulipa faini ya shilingi **milioni 240,** alikaidi kulipa na hivyo kupelekwa mahakamani. Mahakama ya Hakimu Mkazi Mwanza ilimtia hatiani na kumhukumu kifungo cha miaka mitano au kulipa faini ya shilingi **milioni 306** ambayo aliilipa. Baada ya kulipa faini, mvuvi huyo aliandika barua ya kukiri kosa na kuomba msamaha kwa makosa aliyotenda na kuahidi kuacha vitendo vya uvuvi haramu na kutoa ushirikiano katika kukomesha vitendo hivyo. Aidha, jumla ya watuhumiwa **110** walifungwa kutokana na kupatikana na makosa mbalimbali ya uvuvi na biashara haramu wakati wa kutekeleza Operesheni Sangara na doria.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Sea Shepherd Global mwaka 2017/2018, iliendesha operesheni Jodari katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu. Katika operesheni hiyo, meli iitwayo Buah Naga Na. 1 ya Malaysia ilikamatwa kwa kosa la kukutwa na kilo **90** za mapezi ya papa bila miili na kutozwa faini ya shilingi **milioni 770** ambapo alikaidi na kufikishwa mahakamani. Aidha, Mwezi Desemba, 2018 Mahakama Kuu Kanda ya Mtwara iliwatia hatiani watuhumiwa wakiwemo mmiliki, nahodha na wakala wa meli na kuwahukumu kulipa faini ya jumla shilingi **bilioni 1** au kutumikia kifungo cha **miaka 20** kila mmoja. Watuhumiwa wote wanatumikia kifungo baada ya kushindwa kulipa faini.

**146.** ***Mheshimiwa Spika***, zana haramu zilizokamatwa katika maeneo yote ziliteketezwa kwa amri ya mahakama. Zana hizo haramu kama zingeendelea kutumika zingeathiri uendelevu wa rasilimali za uvuvi na hivyo kuathiri upatikanaji wa malighafi kwenye viwanda vya kuchakata samaki. Samaki wachanga na wazazi waliokamatwa waligawiwa kwa taasisi za umma, vituo vya kulelea watoto yatima na wenye mahitaji maalum na mabondo yalitaifishwa na kupigwa mnada. Aidha, injini na mitumbwi iliyokamatwa ilikabidhiwa kwa wahusika baada ya kulipa faini. Operesheni na doria hizi zimewezesha kuleta matokeo chanya yakiwemo kuongezeka kwa upatikanaji wa samaki wakubwa ambao siku za nyuma hawakuwa wanapatikana. Kutokana na juhudi hizi uvuvi haramu umepungua kwa asilimia **75** kwa maji baridi na kupungua kwa milipuko katika uvuvi kwa asilimia **99** katika mwambao wa Bahari.



**147.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019 Wizara ilishiriki katika Kikao cha Baraza la Mawaziri la Kisekta la Uvuvi la Jumuiya ya Afrika Mashariki kilichofanyika Arusha tarehe 1 Machi, 2019 ambapo baadhi ya maamuzi yaliyofikiwa ni pamoja na nchi wanachama:-

(i) Kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi za kupambana na uvuvi haramu katika Ziwa Victoria kupitia Operesheni Sangara 2018 ambapo kumepelekea kuongezeka kwa wingi na ukubwa wa samaki;

(ii) Kutekeleza Operesheni Okoa Sangara (Operation Save Nile Perch -OSNP);

(iii) Kuendelea na utafiti kuhusu matumizi ya nyavu zilizounganishwa; na

(iv) Kushirikiana katika juhudi za kudhibiti utoroshaji wa mazao ya uvuvi katika maeneo ya mipakani.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa kufanya doria za kawaida zenye sikukazi **6,500**. Aidha, Wizara itafanya Operesheni Maalum kila robo mwaka na kuiwezesha MATT kutekeleza majukumu yake kwa kufanya Operesheni **12**. Vilevile, Wizara itaimarisha vituo **27** na kuanzisha Kanda tano **(5)** za usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Pia, Wizara itaanzisha vituo vipya **10** vya ukusanyaji wa maduhuli katika Ziwa Victoria **(7)** na Ziwa Tanganyika **(3)** na kufanya kaguzi katika maeneo ya mipaka, vizuizi, masoko na kwenye mialo.

**Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu**

**149.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) iliendelea kusimamia hifadhi za bahari na maeneo tengefu kwa kufanya doria zenye sikukazi **677** katika maeneo yote **18** yaliyohifadhiwa ambayo ni Hifadhi za Bahari tatu **(3)** na Maeneo Tengefu **15**. Matokeo ya doria hizo ni pamoja na kukamatwa kwa boti tano **(5),** injini tatu **(3)**, seti tatu **(3)** za vifaa vya kuogelea, magogo kumi **(10),** fito **117** za mikoko na nyavu haramu vipande **58.**

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo yaliyohifadhiwa katika bahari huwa ni kivutio kikubwa cha utalii kwa wageni wa kutoka ndani na nje ya nchi. Vivutio hivyo ni pamoja na fukwe nzuri zenye mchanga laini na mweupe, magofu yenye historia za kusisimua, uoto wa asili, nyasi za bahari za aina mbalimbali, matumbawe laini na magumu yenye rangi mbalimbali, samaki aina ya potwe, silikanti, kasa, kaa wanaokwea minazi waitwao tuyuyu (coconut crab) na samaki wa mapambo. Viumbe hivi vinapatikana katika maeneo machache sana hapa duniani na hivyo kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache zenye vivutio vya aina hii na viwango bora vya utalii wa bahari na pwani ambapo kwa mwaka 2018/2019 jumla ya watalii **46,304** walitembelea hifadhi hizo ikilinganishwa na Watalii **45,091** katika kipindi kama hiki mwaka 2017/2018.

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, MPRU iliendelea kutoa gawio la maduhuli kwa Halmashauri na Vijiji vilivyomo ndani ya maeneo ya Hifadhi, ambazo maduhuli hukusanywa. Jumla ya shilingi **153,793,383** zilitengwa na kutolewa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia kwa ajili ya kugharamia shughuli za uhifadhi na miradi ya maendeleo katika vijiji **17** vilivyomo ndani ya Hifadhi ya Kisiwa cha Mafia. Aidha, kiasi cha shilingi **47,599,141** kimetengwa kwa ajili ya kuwakopesha wananchi wanaoishi katika vijiji vilivyomo ndani ya Hifadhi ya Bahari ya Mafia.

**152.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia MPRU itaendelea kusimamia rasilimali za Bahari na Pwani zilizoko katika maeneo Tengefu kwa kufanya doria zenye sikukazi **700**. Aidha, itaendelea kukiimarisha Kitengo kwa kutekeleza Mkakati wa Kuongeza Mapato kwa kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo katika maeneo ya hifadhi na kuboresha miundombinu iliyopo ili kuvutia watalii na kuendeleza taratibu za kutangaza maeneo ya visiwa vya Ukuza, Nyuni, Fanjove na Simaya kuwa Maeneo Tengefu. Pia, Wizara imejipanga kuongeza idadi ya watalii wa ndani na nje ili kufikia **60,000** kwa mwaka 2020/2021.

**Uvuvi katika Bahari Kuu**

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika 2018/2019, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu iliendelea kuboresha zaidi mfumo wa Kanzidata (Web Based Database) wa ukusanyaji takwimu za meli za uvuvi na uvuvi wa samaki aina ya Jodari na jamii zake katika Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari (EEZ) kwa kuongeza moduli moja ya ukusanyaji wa takwimu za urefu wa samaki kwa kutumia simu ya kiganjani (*mobile phone data collection module*). Aidha, Mamlaka iliendesha mafunzo maalum ya Ukaguzi wa shughuli za uvuvi katika meli zinazopewa leseni ya kuvua katika EEZ ya Tanzania kwa Maafisa Uvuvi **22** kutoka SMT (**9**), SMZ (**8**) na Mamlaka (**5**) yatawezesha Wakaguzi na wachukua takwimu kutekeleza vyema majukumu yao wawapo kwenye meli za uvuvi.

**154.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Mamlaka kwa kushirikiana na Wadau imefanya doria za kawaida za anga na baharini zenye jumla ya saa **24** ili kupambana na uvuvi haramu na kufuatilia mienendo ya meli za uvuvi kwenye eneo la Ukanda wa Kiuchumi wa Bahari ya Tanzania. Aidha, wakati wa doria hizo hakuna meli ya uvuvi iliyoonekana katika maji ya Tanzania.

**155** ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka imeandaa Mapendekezo ya Sera (Policy briefs) ili kuhamasisha Watanzania kuhusu vivutio vya uwekezaji vinavyopatikana katika uvuvi wa Bahari Kuu. Maandiko haya yatachochea wazawa kuwekeza katika uvuvi wa Bahari Kuu, kuwa na vyombo vya uvuvi wa Bahari Kuu vya kitanzania (*Development of National Fishing Fleet for Sustainable EEZ Fisheries*) ili kuchangia katika uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi, Sera ya Uchumi wa Viwanda na kuondokana na mwenendo usioridhisha wa meli za kigeni katika kukata leseni za uvuvi katika EEZ ya Tanzania kama ilivyo hivi sasa. Aidha, makampuni ya uvuvi ya Serikali ya TAFICO na ZAFICO yako kwenye maandalizi ya kuanza uvuvi wa Bahari Kuu.

**UKUZAJI VIUMBE MAJI**

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara imeandaa na kutekeleza Mpango Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji yaani *National Aquaculture Development Strategic Plan* (NADSP) 2018-2025. Mpango huo unalenga kuongeza uzalishaji, ulaji na masoko ya mazao yatokanayo na viumbe maji kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira.

**157.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kujenga uwezo wa kukabiliana na magonjwa ya viumbe maji, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE) iliandaa Mafunzo ya Kimataifa ya Afya ya Viumbe Maji (Aquatic Animal Health) yaliyofanyika nchini na kushirikisha wataalam **61** kutoka nchi **41** za Afrika na nje ya Afrika.

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, jumla ya vifaranga **17,301,076** (samaki **6,221,076** na kambamiti **11,080,000**) vimezalishwa katika vituo vya Serikali na sekta binafsi ikilinganishwa na vifaranga **15,119,757** vilivyozalishwa mwaka 2017/2018. (**Kiambatisho Na. 28**). Pia, idadi ya mabwawa ya samaki imeongezeka kutoka **24,302** mwaka 2017/2018 hadi **26,445**. Vilevile, Wizara inaendelea kuhamasisha uwekezaji na matumizi ya teknolojia stahiki katika kuzalisha viumbe maji. Miongoni mwa teknolojia hizo ni matumizi ya vizimba (Fish cage) ambapo hadi sasa jumla ya vizimba **408** vimewekwa: Ziwa Victoria (**346**); Ziwa Tanganyika (**9**); na malambo (**53**). Aidha, teknolojia ya *Recirculation Aquaculture System* ambayo hutumia maji kidogo katika ufugaji na inawezesha uzalishaji wa samaki wengi katika eneo dogo imeanza kutumika katika mikoa ya Arusha na Dar es Salaam.

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** ongezeko la mabwawa na vizimba limeenda sambamba na ongezeko la uzalishaji ambapo katika mwaka 2018/2019, uzalishaji wa viumbe maji umefikia tani **18,081.6** ikilinganishwa na tani **16,129.6** za mwaka 2017/2018. Vipande **395** vya lulu vilizalishwa mwaka 2018/2019 ikilinganishwa na vipande **180** mwaka 2017/2018.

# HOTUBA YA WIZARA YA UFUGAJI NA UVUVI

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara katika juhudi za kuongeza upatikanaji wa samaki nchini hususan kwa wananchi wanaoishi maeneo yaliyo mbali na shughuli za uvuvi, imepandikiza jumla ya vifaranga **18,700** vya samaki aina ya sato katika malambo mawili ya Mwamapalala - Itilima (**7,000**) na Mwanjolo - Meatu (**11,700**) mkoani Simiyu.

**161.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara imefanya makadirio na mchanganuo wa gharama za ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vituo vya Kingolwira (Morogoro), Ruhila (Songea), Mwamapuli (Igunga) na kujenga upya kituo cha Nyamirembe (Chato) ili kuimarisha uzalishaji wa vifaranga. Pia, Wizara imeendelea na kazi ya kuboresha kituo cha Machui (Tanga) ikiwa ni pamoja na kukiunganisha na umeme wa Tanesco.

**162.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuimarisha vituo vyake vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji ili viweze kutoa huduma bora za ugani na kuzalisha vifaranga **milioni 18** kwa kushirikiana na sekta binafsi. Wizara itakarabati miundombinu ya vituo vya Ruhila (Songea) Kingolwira (Morogoro), Mwamapuli (Igunga), Nyamirembe (Chato) na Machui (Tanga) ili kuboresha mifumo ya maji na miundombinu ya ututoleshaji wa vifaranga vya samaki.

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaandaa miongozo sita (**6**) ya kuimarisha na kusimamia tasnia ya ukuzaji viumbe maji. Aidha, Wizara itafanya kaguzi kwa kila robo mwaka katika mashamba yote ya kuzalisha vifaranga vya samaki, viwanda vya vyakula na mashamba ya uzalishaji samaki nchini. Vilevile, Mpango wa Kudhibiti Magonjwa ya Samaki utaandaliwa ikiwa ni pamoja na kufanya mafunzo kwa mashamba **20** ya ufugaji samaki. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na sekta binafsi itaainisha, kufanya tathmini ya athari ya mazingira na kuingiza kwenye ramani maeneo yanayofaa kwa ajili ya kuunda kanda **3** za ukuzaji viumbe maji kwenye vizimba katika Ziwa Victoria na kanda **2** za ukuzaji viumbe maji bahari katika Mikoa ya Pwani na Mtwara.

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia mradi wa SWIOFish itasimika kanzidata kwa ajili ya kutunza taarifa mbalimbali ikiwemo za mazao yatokanayo na ukuzaji viumbe maji na kutoa mafunzo kwa watumiaji. Kanzidata hii itaimarisha utendaji kazi wa Wizara na wadau wengine kwa kutoa taarifa zenye tija katika kuendeleza tasnia. Vilevile, Wizara itaanza ujenzi wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari kitakachojengwa Kunduchi, Dar es Salaam.

**UBORA NA USALAMA WA MAZAO YA UVUVI**

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, jumla ya viwanda vikubwa **12** vikiwemo viwanda **(8)** Ziwa Victoria na **(4)** Ukanda wa Pwani vilichakata mazao yenye viwango vya kuuzwa katika Soko la nchi za nje hususan nchi za Jumuia ya Umoja wa nchi za Ulaya. Vilevile, viwanda vya kati vinne **(4)** vilichakata mazao ya uvuvi ambayo yaliuzwa katika soko la kikanda la nchi zingine zisizo za Jumuiya ya Ulaya zikiwemo za Bara la Asia na Marekani. Aidha, kuna viwanda vidogo **34** vya kupokelea samaki hai na maghala **52** kwa ajili ya mazao ya uvuvi yaliyokaushwa.

**166** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya kaguzi **3,155** za kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi yanayosafirishwa nje ya nchi. Kaguzi hizo zilifanyika mipakani, viwanja vya ndege na bandarini. Vilevile, vibali **3,108** vilitolewa kwa ajili ya kusafirisha tani **41.2** za samaki kwa ajili ya soko la ndani na vibali **47** vilitolewa kuruhusu mazao ya uvuvi kuingizwa nchini. Aidha, kufuatia doria na Operesheni zinazoendelea nchini, hali ya upatikanaji wa samaki hususan samaki aina ya sangara imeimarika na viwanda kuongeza uzalishaji, ambapo wastani wa tani **180** zinazochakatwa kwa siku katika mwaka 2018/2019 ikilinganishwa na tani **165** za mwaka 2017/2018. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kufuatilia mifumo ya uzalishaji katika viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi, masoko na maghala kwa kufanya kaguzi za kina **120**.

**167.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imefanya kaguzi katika mialo **125** ikiwemo mialo ya kisasa **13** katika ukanda wa Ziwa Victoria **(6)**, ukanda wa Ziwa Tanganyika (**4**) na ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi **(3)** ili kuthibiti ubora na usalama wa mazao ya uvuvi. Aidha, Wizara imefanya tathmini katika maeneo ya vijijini **10** vya Marehe na Katembe (Kagera) Kibuyi, Busekela, Bukima na Kisorya (Mara), Kayenze, Chifunfu na Kijiweni (Mwanza), na Nyamikoma (Simiyu) ili kutambua changamoto katika usimamizi na uendelezaji wa mialo na masoko ya mazao ya uvuvi, usalama na miundombinu iliyopo. Pia, katika kutatua changamoto za miundombinu ya masoko ya uvuvi, Wizara inaendelea na ujenzi wa matundu **12** ya choo na mabafu manne **(4)** katika Soko la Samaki la Feri ambao unatarajia kukamilika katika mwaka huu wa fedha.

**168.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itashirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta binafsi katika kujenga, kukagua na kuendeleza miundombinu ya uvuvi nchini. Vilevile, kaguzi **7,200** za kuhakiki ubora na usalama wa samaki na mazao ya uvuvi kabla ya kusafirishwa nje ya nchi zitafanyika. Pia, Wizara itaimarisha na kuviwezesha vituo **27** vya Uthibiti Ubora na Viwango vya mazao kwa kuvipatia vitendea kazi ili viweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Wizara itaimarisha upatikanaji wa taarifa ya masoko ya mazao ya uvuvi kwa kuanzisha utafiti na ushauri wa masoko (Marketing Intelligence Unit-MIU) kupitia Dawati la Sekta Binafsi la Wizara.

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha Maabara ya Uvuvi - Nyegezi kwa kuipatia vitendea kazi na mafunzo kwa watalaam ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Katika mwaka 2018/2019, watalaam tisa **(9)** wa Maabara walipata mafunzo kuhusu mbinu za ukaguzi, uhakiki wa njia na vifaa vya kupimia na usimamizi wa Maabara. Aidha, Maabara imefanya chunguzi za kimaabara kwa sampuli **3,238** za minofu ya samaki, maji na udongo ili kubaini uwepo wa vimelea, masalia ya madawa ya mimea, kemikali na madini tembo. Vilevile, Maabara imeendelea kukidhi vigezo vya ithibati kutoka Taasisi ya Ithibati ya Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Africa-SADC (SADCAS) kwa vipimo **13** vya maikrobaiolojia kwa maji na chakula. Pia, mwezi Juni, 2018 Maabara hii upande wa kemikali ilipata ithibati katika aina nne **(4)** za vipimo (parameters) ambavyo ni vya madini tembo, unyevunyevu (Moisture content), pH na *Conductivity*.

**171** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuimarisha Maabara kwa kuipatia vitendea kazi na kutoa mafunzo kwa watumishi ili kuiwezesha kupanua wigo wa vipimo vyenye ithibati upande wa maikrobaiolojia na kemikali.

**USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA KATIKA SEKTA YA UVUVI**

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kuimarisha mashirikiano ya kikanda na kimataifa ili kusimamia rasilimali za uvuvi katika maji yanayomilikiwa kwa pamoja na nchi husika. Miongoni mwa maji hayo ni maziwa makuu ya Victoria (LVFO), Tanganyika (LTA), Nyasa na Ukanda wa Bahari ya Hindi (IOTC, WIOMSA, SWIOFC, IORA). Kupitia mashirikiano hayo, nchi yetu inapata fursa ya kushiriki na kutekeleza sheria, miongozo, mikataba, itifaki na taratibu mbalimbali za kikanda na kimataifa zenye lengo la kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa kuzingatia kwamba samaki hawana mipaka. Aidha, nchi yetu ni mwanachama wa mashirika na Taasisi mbalimbali za Kimataifa.

**173.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kushiriki kwenye **mikutano**, makongamano na warsha mbalimbali zenye lengo la kujadili na kuweka mikakati ya pamoja ya kusimamia rasilimali za uvuvi. Miongoni mwa mikakati hiyo ni ya kuendesha operesheni za pamoja dhidi ya uvuvi haramu usioratibiwa na usiotolewa taarifa katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika. Aidha, ushirikiano huo umewezesha nchi yetu kushiriki kwenye operesheni katika Ukanda wa Bahari ya Hindi.

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi za kikanda na kimataifa katika sekta ya uvuvi ili kuboresha usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi. Vilevile, Wizara itaendelea kushiriki katika masuala ya kikanda, kimataifa na kutekeleza mikataba na itifaki mbalimbali za kikanda na kimataifa ambazo nchi yetu ni mwanachama.

**UTAFITI, MAFUNZO NA UGANI**

**Utafiti wa Uvuvi**

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia TAFIRI imefanya tafiti mbalimbali kwa nyakati tofauti zenye lengo la kujua mwenendo wa rasilimali za uvuvi. Matokeo ya tafiti hizi yanasaidia kuandaa mipango ya uvuvi endelevu ili kuleta tija na kusaidia ukuaji wa sekta katika kuchangia pato la Taifa. Tafiti hizo ni pamoja na:-

**Ziwa Victoria**

**Utafiti wa Rasilimali za Uvuvi katika Ziwa Victoria**

**176.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuangalia uwingi wa samaki Ziwa Victoria kwa kutumia Teknolojia ya *Hydro-acoustic survey*, TAFIRI kwa kushirikiana na Taasisi za *Kenya Marine and Fisheries Research Institute (KMFRI-Kenya )* na *National Fisheries Resources Research Institute (NaFIRRI-Uganda),* utafiti uliofanyika mwezi Septemba hadi Oktoba 2018, ulionesha uwepo wa tani **2,210,000** za aina mbalimbali za samaki. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwepo kwa ongezeko la Sangara kutoka tani **417,936** mwaka 2016 hadi kufikia tani **553,770** mwaka 2018. Vilevile, Sangara wa chini ya sentimita **50** wamepungua kutoka asilimia **96.6** mwaka 2017 hadi kufikia asilimia **62.8** mwaka 2018; wale wa kuanzia sentimita **50** hadi **85** wameongezeka kutoka asilimia **3.3** mwaka 2017 hadi kufikia asilimia **32.0** mwaka 2018; na walio juu ya sentimenta **85** wameongezeka kutoka asilimia **0.4** mwaka 2017 hadi kufikia asilimia **5.2** mwaka 2018. Aidha, Takwimu zinaonesha kuwa wastani wa urefu wa Sangara umeongezeka kutoka sentimeta **16** mwaka 2017 hadi kufikia sentimeta **25.2** mwaka 2018.

**177.** ***Mheshimiwa Spika***, matokeo haya yanaonesha kuongezeka kwa Sangara ziwani sambamba na kuongezeka kwa Sangara wazazi na kupungua kwa Sangara wachanga ikilinganishwa na mwaka 2017. Ongezeko hili ni matokeo ya doria na operesheni dhidi ya uvuvi haramu katika Ziwa Victoria zilizofanyika katika vipindi tofauti. Aidha, ongezeko hili la Sangara wakubwa litawanufaisha wavuvi, wenye viwanda na wafanyabiashara ya mabondo kwa vile sangara wenye urefu wa zaidi ya sentimita 85 hutoa minofu na mabondo makubwa ambayo yana thamani ya juu katika soko.

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kushamiri kwa biashara ya mabondo hivi karibuni, ambapo uzalishaji na mauzo nje ya nchi hadi kufikia mwezi Machi, 2019 umefikia tani **884.30** zenye thamani ya shilingi **bilioni 178.31** na kuingiza mrabaha wa shilingi **bilioni 2.87** (**Kiambatisho Na.29**). Aidha, Wizara imefanya tathmini ya kina ili kuangalia mnyororo mzima wa zao hili la uvuvi na utafiti wa kuangalia urefu na uzito wa mabondo ya sangara wa Ziwa Victoria unaofaa kibiashara bila kuathiri rasilimali. Utafiti huu umeonesha kuwa mabondo ya kuanzia sentimita **12** /gramu **13** kwa mabondo mabichi, na sentimita **8** /gramu **4** kwa mabondo makavu ndiyo yanayofaa kuingizwa sokoni.

**Bahari ya Hindi**

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, TAFIRI kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (Deep Sea Fishing Authority - DSFA) imeendelea na utafiti wa vifaa vya kuvutia samaki FADs (Fish Aggregating Devices) ambao unafanyika katika maeneo ya Bagamoyo na Nungwi Zanzibar, ambapo wavuvi wadogo watasogezwa taratibu kutoka maji mafupi hadi kufikia maji marefu. Aidha, tafiti hizi zimeonesha kuwa mapato ya wavuvi walioshiriki kwenye utafiti huu yaliongezeka na kuwa na uhakika wa kupata wastani wa shilingi **20,000** hadi shilingi **35,000** kwa siku na muda wa kuvua umepungua kutoka saa **12** kabla ya FADs na kuwa saa tano (**5**) baada ya FADS. Aidha, katika mwaka 2019/2020, TAFIRI itaendelea kufanya ufuatiliaji wa ufanisi wa FADs katika kukusanya samaki kwa maeneo ya Bagamojo na Nungwi.

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, TAFIRI imeendelea na utafiti wa kujua wingi na biolojia ya Kambamiti katika pwani ya Tanzania. Hali ya rasilimali ya Kambamiti imeendelea kuimarika ambapo Kambamiti wameongezeka katika eneo la Bagamoyo hadi Pangani ambapo utafiti ulionyesha kuongezeka kwa mavuno kutoka kilo **26.16** kwa saa mwaka 2015/2016 hadi kilo **58.45** kwa saa mwaka 2018/2019. Aidha, katika maeneo ya Mkuranga hadi Kilwa mavuno yaliongezeka kutoka kilo **29.58** kwa saa mwaka 2015/2016 hadi kilo **61.38** kwa saa mwaka 2018/2019. Ongezeko hili ni matokeo ya kufunga kwa msimu wa uvuvi wa kambamiti kwa kipindi cha miezi sita **(6)** kila mwaka.

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** TAFIRI kwa kushirikiana na kikundi cha ufugaji samaki cha Barikiwa, Liwale, Lindi inaendelea kufanya utafiti wa kupata samaki wazazi (brood stock) bora wa sato kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora (local fish strain) ili kutatua changamoto ya upatikanaji wa mbegu bora za samaki katika mikoa ya kusini.

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, utafiti wa kuzalisha mbegu bora ya samaki inayofaa kufugwa katika maeneo ya Liwale utaendelea ikiwa ni pamoja na upanuzi wa mabwawa na ujenzi wa vitotoleshi vipya ili kuongeza uzalishaji vifaranga vya sato na vya kambale. Aidha, TAFIRI itaendelea na utafiti wa ufugaji wa samaki kwenye vizimba katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa pamoja na Bahari ya Hindi. Pia, TAFIRI itafanya tafiti za kubaini uwepo, aina na mtawanyiko wa rasilimali za uvuvi nchini.

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020**,** Wizara kupitia TAFIRI itafanya tafiti za kuchunguza uhusiano wa vinasaba kati ya makundi ya samaki aina ya Jodari na jamii zake na kuchunguza mazingira ya Bahari yanayovutia uwepo wa samaki hao wanaopatikana Bahari ya Hindi. Tafiti hizi zitaimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi, kupunguza gharama za uvuvi hususan wavuvi wadogo ili kuwanufaisha na rasilimali za uvuvi na kuongeza mchango wa Sekta ya Uvuvi katika pato la Taifa.

**Elimu na Mafunzo ya Uvuvi**

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) imeende-

# HOTUBA YA WIZARA YA UFUGAJI NA UVUVI

lea kutoa mafunzo ya teknolojia za uvuvi kwa vijana nchini kama Sera ya Uvuvi inavyoagiza. Jumla ya wanafunzi **1,088** walidahiliwa katika masomo ya ngazi za Astashahada na Stashahada kwenye Kampasi zake za Mbegani, Nyegezi na Kigoma. Kwa upande wa kozi fupi, jumla ya wananchi **1,300** wamepatiwa mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo na mbinu za kuvua na ukuzaji viumbe maji.

**185.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019, FETA kwa kushirikiana na NORGES VEL (Asasi isiyo ya Kiserikali ya nchini Norway) na Chama cha Wakuzaji Viumbe Maji Nchini (Aquaculture Association of Tanzania - AAT) walipata ufadhili wa shilingi **bilioni 4.6** kutoka Shirika la Misaada la nchini Norway (NORAD) kutekeleza Mradi wa Uzalishaji wa Samaki aina ya Sato na Kufundisha Stadi za Ufugaji na Biashara. Fedha hizi zitatumika kuanzisha yafuatayo katika Wilaya ya Kibaha**,** Pwani: shamba la ufugaji samaki litakalokuwa na mabwawa **20** na vitotoleshi vya vifaranga vya samaki, kituo cha mafunzo kwa vitendo kitakacholenga umahiri na weledi katika usimamizi wa tasnia ya ufugaji samaki, na kituo atamizi (*Incubation Centre*), kutoa fursa kwa wahitimu kuanzisha mashamba madogo ya ufugaji na kupatiwa pembejeo (vifaranga na chakula) na ushauri ili kuimarisha weledi. Atamizi italenga kufundisha stadi za ufugaji na biashara kwa vijana na wanawake **120** kila mwaka.

**186.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia FETA imeandaa rasimu ya mitaala ya kutoa mafunzo ya rasilimali watu kwa ajili ya uwekezaji katika uvuvi wa Bahari Kuu (Deep Sea Fishing). Hadi sasa, Mitaala hiyo imefikia hatua za mwisho za uhakiki (*validation*). Aidha, Wizara inaendelea na hatua za kuomba ridhaa ya kuridhiwa kwa Itifaki ya *Standards of Training, Certification and Watch keeping for Fishing Vessel Personnel* (STCW – F), 1995. Kuridhiwa kwa Itifaki hii kutasaidia mafunzo hayo kutambulika kimataifa na wahitimu kuwa na sifa ya kufanya kazi katika meli za uvuvi wa bahari kuu.

**187.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/2020, Wizara imepanga kuhakikisha kwamba Vituo vya FETA vya Gabimori (Rorya), Mwanza South (Mwanza), na Mikindani (Mtwara) vinaanza utoaji wa mafunzo na elimu ya ufugaji samaki, ikiwa ni pamoja na kuzalisha vifaranga vya samaki na huduma za ugani katika Kanda husika.

**Huduma za Ugani wa Uvuvi**

**188.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kutoa Huduma za Ugani kwa kutoa miongozo inayotumiwa na Halmashauri mbalimbali na watoa huduma wengine wanaotoa huduma hii kwa wavuvi na wakuzaji viumbe maji. Vilevile, Sekta ya Uvuvi ina hitaji la wagani **16,000** ikilinganishwa na wagani 671 waliopo kwa sasa. Kati ya hao, Wagani **419** ni kutoka Halmashauri na wagani 252 wapo chini ya Wizara. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika mafunzo ya uvuvi kwa lengo la kuongeza wataalam hao. Pia, Wizara inaendelea kushauriana na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga nafasi na kuomba kibali cha kuajiri Maafisa Ugani ili kupunguza pengo hilo. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI inafanya tathmini ili kutambua maeneo yenye upungufu na maeneo yenye ziada ya watumishi/wagani waweze kuhamishimiwa kwenye maeneo yenye uhitaji mkubwa.

**189.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kutoa elimu ya uvuvi endelevu na ukuzaji viumbe maji kwa umma kupitia vipindi **15** vya radio na vipindi vitano (**5**) vya luninga. Aidha, nakala **4,000** za machapisho mbalimbali zimesambazwa kwa wadau. Wizara imeendelea kuhamasisha ukuzaji viumbe maji ambapo idadi ya wadau waliopatiwa elimu ya ufugaji bora wa samaki imeongezeka kutoka **5,229** mwaka 2017/2018 hadi kufikia **7,047** mwaka 2018/2019. Vilevile, elimu ya kuongeza thamani ya zao la mwani imetolewa kwa wadau **492** kutoka vikundi **31** na kuwawezesha kutengeneza bidhaa mbalimbali kama shampoo, sabuni na mafuta ya ngozi. Vilevile, wadau **7,586** walipata elimu ya uvuvi endelevu na ukuzaji viumbe maji kupitia maonesho mbalimbali yakiwemo ya Nanenane, Sabasaba na Siku ya Chakula Duniani.

**190.** ***Mheshimiwa Spika*,** kutokana na changamoto nyingi zinazowakabili wavuvi na Sekta ya Uvuvi kwa ujumla, Wizara imeamua kuendesha mafunzo Rejea kwa wavuvi na maafisa ugani nchi nzima ili kuleta uelewa wa pamoja wa sheria, matumizi ya zana halali za uvuvi, ufugaji viumbe maji, kupunguza uharibifu wa mazao ya uvuvi (Post harvest loss), kuunda ushirika wa wavuvi na urahisi wa upatikanaji mikopo na elimu ya ujasiriamali. Mafunzo haya yamezinduliwa tarehe 14 Aprili, 2019 katika mwalo wa Kilindoni ulioko Wilayani Mafia katika Mkoa wa Pwani. Lengo la Mafunzo hayo ni kubadili mtazamo na fikra za wavuvi juu ya ulinzi, uhifadhi na kuendelea kuvua na kutumia rasilimali za uvuvi ili kuhakikisha rasilimali hizi zinakuwa endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Mafunzo haya yanatolewa kwa awamu ambapo awamu ya kwanza imeanza katika Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani. Jumla ya wavuvi **6,911** kutoka katika mialo ya Kilindoni, Jibondo, Chole, Juani, Nganje, Boza, Kisiju Pwani, Koma, Buyuni, Kimbiji, Minazimikinda, Tandavamba, Ununio, Mbweni, Kwale na Kunduchi wamepata mafunzo.

**191.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/2020, Wizara itarusha hewani vipindi **30** vya radio na **10** vya runinga kuhusu uvuvi endelevu na ukuzaji viumbe maji. Vilevile, itahamasisha wagani **200** na wadau **8,000** kuhusu shughuli mbadala ili kupunguza nguvu ya uvuvi katika maji ya asili. Pia, Wizara itaendelea kusimamia na kufuatilia uanzishwaji wa mashamba darasa ya ukuzaji viumbe maji na kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi na kutangaza bidhaa mbalimbali zinazotokana na Sekta kupitia maonesho mbalimbali.

**MIRADI YA SEKTA YA UVUVI**

**192.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish)". Lengo kuu la mradi huu ni kuimarisha usimamizi madhubuti wa uvuvi katika ngazi ya kijamii, kitaifa na kikanda.

**193.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Mradi wa SWIOFish umeiwezesha TAFIRI kufanya tafiti mbalimbali katika ukanda wa Bahari ya Hindi; Doria na Operesheni MATT; mafunzo kwa vikundi **50** vya BMUs; uandaaji wa mitaala ya FETA; tathmini ya matumbawe katika maeneo yaliyohifadhiwa na mazao ya uvuvi; mafunzo kwa watumishi wa sekta ya uvuvi na semina kuhusu madhara ya uvuvi haramu kwa wadau.

**194.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Mradi itafanya kazi zifuatazo:- Kuwezesha TAFIRI kufanya tafiti za mavuvi ya kipaumbele; Kuimarisha ushiriki wa jamii za wavuvi katika usimamizi na ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi; Kuwezesha Doria katika ulinzi wa rasilimali za uvuvi katika mavuvi ya kipaumbele; Kuiwezesha Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU); Kuimarisha Mfumo wa Taarifa zinazohusu Uvuvi kulingana na matakwa ya kikanda. Kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi wa Samaki wanaopatikana katika tabaka la juu la maji ifikapo Juni 2020; na kuzijengea uwezo Taasisi za Uvuvi pamoja na Taasisi za Umma.

**195.** ***Mheshimiwa Spika*,** pia, mradi huu utaboresha miundombinu kwa gharama ya shilingi **8,191,312,294.20** kama ifuatavyo: ujenzi wa maabara ya utafiti wa samaki Temeke shilingi **403,053,600.00**; ujenzi wa maabara ya TAFIRI shilingi **2,609,491,754.20**; ujenzi wa nyumba za watumishi wa MPRU Tanga shilingi **962,918,940.00;** ujenzi wa jengo la ofisi MPRU - Mafia shilingi **926,560,000.00;** ukarabati mkubwa wa miundombinu ya soko la Feri - Dar es Salaam shilingi **1,667,808,000.00**; na ujenzi wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari (Mariculture Centre) Kunduchi, Dar es Salaam shilingi **1,621,480,000.00.**

**KUWEZESHA WAVUVI WADOGO NA WAKUZAJI VIUMBE MAJI**

**196.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019, jumla ya vikundi **50** vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs) katika Wilaya tano (**5**) za Pangani (**12**), Mkinga (**14**), Jiji la Tanga (**5**) Bagamoyo (**9**) na Lindi Vijijini (**10**) vimeimarishwa kwa kupatiwa mafunzo ya uvuvi endelevu. Vilevile, mafunzo juu ya kuendeleza Maeneo ya Usimamizi wa pamoja yamefanyika kwa maafisa uvuvi **10** wa Halmashauri na watano (**5**) wa Serikali Kuu.

**197** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019, kupitia Mradi wa Kupunguza Uharibifu wa Samaki baada ya Mavuno unaotekelezwa katika Ziwa Tanganyika, majiko banifu **100** yamesambazwa katika Vijiji/mialo ya uvuvi **16** katika Mkoa wa Kigoma. Vilevile, wachakataji wa samaki **640** katika vijiji **16** wamefundishwa jinsi ya kutumia majiko na kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi katika Ziwa Tanganyika. Pia, Wizara imewezesha vikundi vya ushirika vya wavuvi vya Igombe – Mwanza, Ikumba itale – Chato, Nkasi (Ziwa Tanganyika), Migoli - Mtera na vikundi viwili vya ushirika wa ufugaji samaki Peramiho (Ruvuma) kwa kupatiwa fedha na vifaa.

**UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA UVUVI**

**198.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kuhamasisha Sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya uvuvi kwa kuweka mazingira mazuri ikiwemo uwepo wa malighafi kwa viwanda vya kusindika mazao ya uvuvi hususan viwanda vya kuchakata samaki aina ya Sangara. Aidha, kiwanda kimoja (**1**) kimejengwa wilaya ya Mkuranga katika mkoa wa Pwani.

**199.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara inaendelea kuchukua hatua ya kuhakikisha kuwa viwanda vilivyofungwa vya *Prime Catch* cha Musoma, *Supreme Perch* (zamani VicFish) na *TanPerch* vya Mwanza vinafufuliwa. Aidha, Serikali inahamasisha ujenzi wa viwanda vipya vya kuchakata samaki katika ukanda wa bahari na maziwa makuu. Kwa sasa, mazungumzo yanaendelea na wawekezaji kutoka nchi za Japan, Mauritius, Korea kusini na Misri ili waweze kujenga viwanda hivyo.

**200.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019, Wizara inafanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari ya uvuvi kupitia Mshauri Mwelekezi Kampuni ya *Sering Ingegneria* ya nchini Italia kwa gharama ya shilingi **bilioni 1.4**. Mkataba wa kazi hiyo ulisainiwa tarehe 2 Julai, 2018 na kazi hiyo ilianza tarehe 2 Agosti, 2018. Kukamilika kwa upembuzi yakinifu kutaiwezesha Serikali kutambua maeneo yanayofaa kwa ujenzi wa bandari ya uvuvi na kujua gharama za ujenzi wa bandari hiyo. Aidha, uwepo wa bandari ya uvuvi utawezesha meli za uvuvi zinazovua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari ya Tanzania na Bahari Kuu kutia nanga, kushusha na kupakia mazao ya uvuvi.

**201.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Bahari na Uvuvi (Ministry of Oceans and Fisheries – MOF) ya Jamhuri ya Korea ya Kusini inafanya mazungumzo kwa ajili ya kufadhili ujenzi wa Bandari ya Uvuvi kupitia *Exim Bank* ya Korea baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu. Mkataba wa Makubaliano (MoU) wa ujenzi wa Bandari hiyo ya uvuvi utasainiwa mwishoni mwa mwezi Mei 2019.

**202.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara inaendelea na juhudi za kufufua lililokuwa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) ili kuimarisha uwekezaji katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari, na Bahari Kuu. Katika mwaka 2018/2019, Wizara imezindua Menejimenti ya kusimamia ufufuaji wa TAFICO. Aidha, Wizara imeandaa na kutekeleza Mkakati wa kufufua TAFICO. Katika kutekeleza mkakati huo, menejimenti ya TAFICO inaendelea kutambua mali za lililokuwa shirika la Uvuvi ambapo hadi sasa mali zenye thamani ya shilingi bilioni **118** zimetambuliwa.

**203.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara inaendelea kuwasiliana na wadau mbalimbali wa maendeleo ili kupata fedha za kuendesha Shirika ikiwemo kununua meli mbili **(2)** za uvuvi, kukarabati majengo na miundombinu ya TAFICO inayojumuisha mitambo ya kuzalisha barafu, gati, vyumba vya ubaridi na kuzuia mmomonyoko wa ardhi.

**204.** ***Mheshimiwa Spika*,** kupitia Serikali ya Japan zimepatikana jumla ya Yen za Japan **milioni 200** sawa na takriban shilingi **bilioni 4.2** kwa ajili ya ununuzi wa meli ya uvuvi kwenye maji ya Kitaifa, ukarabati wa chumba na ununuzi wa mtambo wa barafu na gari maalum la kubebea samaki. Hadi sasa Serikali ya Japan kupitia *Japan Tuna Fisheries Cooperative Association* (JTFCA) wameonesha nia ya kuyarejesha makampuni ya meli ya Japan kukata leseni za uvuvi katika maji ya Bahari Kuu ya Tanzania. Hii itasaidia kuongeza mapato ya Serikali yanayotokana na tozo za leseni kupitia Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA).

**205.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/2020, Wizara itakamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari ya uvuvi na kuendelea kutekeleza mkakati wa kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) na kuweka mazingira mazuri kwa wananchi kuwekeza katika tasnia ya ukuzaji viumbe maji.

**D: MASUALA MTAMBUKA YA MIFUGO NA UVUVI**

**Dawati la Sekta Binafsi**

**206.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019, Wizara ilianzisha Dawati la Sekta Binafsi lililozinduliwa rasmi tarehe 01 Oktoba, 2018. Lengo la kuanzishwa kwa Dawati la Sekta Binafsi ni kufuatilia kwa karibu changamoto zinazoikabili Sekta Binafsi (Sekta ya Mifugo na Uvuvi), kuzitafutia ufumbuzi na kuongeza uwekezaji na uchangiaji kwenye Pato la Taifa ili kufikia azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuelekea kwenye Uchumi wa Viwanda.

**207.** ***Mheshimiwa Spika*,** Dawati la Sekta Binafsi limesaidia kutatua migogoro ya kampuni za Sekta Binafsi na Taasisi za Serikali pamoja na kuharakisha upatikanaji wa huduma zilizokuwa zinachelewesha ufanisi wa kampuni hizo. Baadhi ya kampuni zilizowasilisha changamoto zao dhidi ya Taasisi za Serikali na kutatuliwa kwa wakati ni Kiwanda cha nyavu za samaki Sun flag na TBS, Kiwanda cha chakula cha mifugo na samaki-Marenga Milers na TBS, Kampuni ya kutengeneza madawa mifugo-Farm Base na TRA, kiwanda cha kuzalisha maziwa cha AZAM na Wizara, Viwanda vya kusindika minofu ya samaki na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC - kuanzisha Ofisi Mwanza), Kiwanda cha kusindika nyama za kuku (Kuku Poa) na Bodi ya Nyama.

**208.** ***Mheshimiwa Spika*,** Dawati la Sekta Binafsi limesaidia kuunganisha kampuni zinazohitaji huduma ya mikopo hususan kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa kusaidia utayarishaji wa Andiko la Biashara (*Bankable business Plan*). Jumla ya kampuni tano (5) zimefaidika na huduma ya Dawati la Sekta Binafsi kwenye huduma ya Maandiko ya Biashara. Hadi kufikia mwezi Aprili 2019, Dawati la Sekta Binafsi limewezesha mikopo yenye thamani

ya shilingi bilioni **17.3.** Aidha, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni **55** inategemewa kutolewa wakati wowote (Mifugo bilioni **26** na Uvuvi bilioni **29**).

**209.** ***Mheshimiwa Spika***, Dawati limewezesha Wizara kuingia katika Makubaliano (MoU) na Viwanda Vinne vya kimkakati vinavyosindika maziwa yanayokaa muda mrefu bila kuharibika *(Ultra Heat Treatment – UHT)* ambavyo ni ASAS LTD, Tanga Fresh Ltd, MilkCom Ltd na AZAM Dairy Products. Lengo ni kuongeza usindikaji wa Maziwa kutoka lita **154,100** hadi lita **284,500** kwa siku, sawa na ongezeko la lita **130,500** kwa viwanda vyote kufikia Desemba 2019.

**210.** ***Mheshimiwa Spika***, Dawati limesaidia kurejesha uzalishaji wa Kiwanda cha AZAM kilichopo Zanzibar baada ya Wizara kuwezesha unafuu wa tozo wa shilingi **250** kwa lita badala ya shilingi **2,000** kwa lita kwa maziwa yaliyozalishwa kwa malighafi kutoka nje ya nchi. Vilevile, kusamehe tozo zote za maziwa yanayozalishwa na kusindikwa Zanzibar yanapoingizwa Tanzania Bara, pia maziwa ghafi yanayosafirishwa kwenda Zanzibar na baadaye kusindikwa na kuuzwa katika soko la Tanzania Bara.

**211.** ***Mheshimiwa Spika,*** Dawati limetembelea na kukutana na wadau **213** wa Sekta za Mifugo na Uvuvi na kutoa ushauri wa kitaalam. Wadau waliotembelewa ni pamoja na viwanda vya kusindika samaki, nyama, ngozi, maziwa, kuku pamoja na wafugaji wa samaki katika vizimba na mabwawa (**Kiambatisho Na. 30).**

**212.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi inaendelea kuunganisha vyama vya Ushirika **86** vya Wavuvi na taasisi za kifedha ili waweze kupata mikopo. Pia, Dawati limewezesha kuanzishwa kwa vyama vya Ushirika vipya vitatu (3) vya Wavuvi vya Kikumba Itale katika Wilaya ya Chato, Igombe katika Wilaya Ilemela na Kasera cha Tanga Mjini. Vilevile, Dawati limewezesha vyama vya ushirika viwili (**2**) vya wafugaji kupatiwa mkopo wa ng'ombe bora wa maziwa **73** kati ya vyama saba (**7**) vilivyoomba kukopeshwa ng'ombe **350**.

**213.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina dhamira ya dhati ya kuimarisha ushirikiano na Sekta Binafsi na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na wadau wa maendeleo (World Bank, DALBERG, ANSAF, ASPIRE, TADB, PASS, TPSF na SAGCOT) kwa lengo la kukuza mchango wa Sekta Binafsi katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**214.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Dawati la Sekta Binafsi litaendelea kuainisha, kuratibu na kufuatilia changamoto na kuzitafutia ufumbuzi kwa haraka ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara katika Sekta za Mifugo na Uvuvi. Aidha, Dawati litaendelea kuhamasisha uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi ikiwemo: uwekezaji katika viwanda vya kusindika mazao ya mifugo (maziwa, ngozi na nyama), vyakula vya mifugo, ufugaji samaki katika vizimba, mabwawa, uzalishaji wa vifaranga na vyakula bora vya samaki; kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika mashirika ya NARCO na TAFICO; na kuwaunganisha wadau wa mifugo na uvuvi na taasisi za kifedha.

**Utawala Bora, Jinsia na UKIMWI**

**215.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara imehamasisha watumishi **420** kupima afya zao kwa hiari na watumishi watatu (**3**) wanaoishi na Virusi vya UKIMWI wamepatiwa huduma ya lishe. Aidha, Wizara imeendelea kuwaelimisha watumishi kuhusu kuzingatia maadili, haki na wajibu katika Utumishi wa Umma. Vilevile, Wizara imewezesha viongozi kutimiza majukumu yao katika Wizara, Majimbo pamoja na kusimamia ujenzi wa jengo la Ofisi za Wizara kwenye eneo la Mji wa Serikali Jijini Dodoma.

**216.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019 Wizara imeajiri watumishi wapya watatu (**3**) wakiwemo Madereva wawili (**2**) na Mkemia mmoja (**1**), vikao viwili (**2**) vya Kamati ya Ajira vimefanyika ambapo watumishi **50** wa kada mbalimbali walithibitishwa kazini baada ya kumaliza vizuri muda wa majaribio. Aidha, watumishi wamehamasishwa kushiriki michezo na kuwezeshwa kushiriki kwenye maonesho mbalimbali ya kitaifa. Pia, watumishi **19** wamewezeshwa kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na **11** kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi. Vilevile, Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Utumishi na Mishahara (HCMIS) na wa Malipo ya Mishahara kwa watumishi (GSPP) imeendelea kusimamiwa ipasavyo.

**217.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara iliandaa mahitaji ya kazi pamoja na maelezo ya kazi kwa kila nafasi ambapo katika kipindi cha miaka mitatu ijayo watumishi **1,893** watahitajika wakiwemo **1,001** wa Sekta ya Mifugo na **892** wa Sekta ya Uvuvi ikilinganishwa na watumishi **824** waliopo sasa kwa Sekta zote. Kati ya hao, watumishi **465** ni wa Sekta ya Mifugo na watumishi **359** ni wa Sekta ya Uvuvi, hivyo kuwa na upungufu wa watumishi **1,069**. Kati ya upungufu huo watumishi **536** ni wa Mifugo na **533** ni wa Uvuvi. Aidha, Wizara imepata kibali cha UTUMISHI cha kuwahamisha watumishi **224** kwenda kwenye Wakala ya Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA). Vilevile, Wizara imeendelea kushirikisha watumishi kupitia Baraza la Wafanyakazi ambapo kikao kimoja cha Baraza kilifanyika kwa ajili ya kujadili bajeti pendekezwa ya Wizara kwa mwaka 2019/2020. Pamoja na watumishi waliopo Wizarani pia katika Serikali za Mitaa kuna jumla ya watumishi **3,795** wa Sekta ya Mifugo **(Kiambatisho Na. 31)** na watumishi **419** wa Sekta ya Uvuvi katika Halmashauri **(Kiambatisho Na.32).** Katika mwaka 2019/20 Wizara itaendelea kuwatembelea watumishi katika maeneo yao ya kazi ili kubaini changamoto zinazowakabili na kuzitafutia ufumbuzi.

**218.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inafanya tathmini ili kutambua maeneo yenye upungufu na maeneo yenye ziada ya watumishi/wagani waweze kuhamishimiwa kwenye maeneo yenye uhitaji mkubwa.

**219.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itatekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa na kuelimisha watumishi kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya kazi katika Utumishi wa Umma. Pia, Mkataba wa Huduma kwa Mteja utatekelezwa, mafunzo kwa watumishi kuhusu Mfumo wa Wazi wa Upimaji wa Utendaji Kazi (OPRAS) yatatolewa. Aidha, Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Utumishi na Mishahara (HCMIS) na Mfumo wa Malipo ya Mishahara ya watumishi (GSPP) itawezeshwa na kusimamiwa ipasavyo. Vilevile, Wizara itasimamia utekelezaji wa Waraka Na.2 wa Mwaka 2006 pamoja na mwongozo wake wa mwaka 2014 unaohusu VVU, UKIMWI na magonjwa Sugu yasiyoambukiza. Aidha, Wizara itahamasisha watumishi kupima afya zao ili wale watakaobainika kuathirika wajitokeze na kupatiwa huduma zinazostahili.

**220.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaajiri watumishi **295** wakiwemo **176** wa Sekta ya Mifugo na **119** Sekta ya Uvuvi na watumishi **10** watathibitishwa kazini. Aidha, Wizara itaendelea kufanya uhakiki wa watumishi **824**. Vilevile, vikao vinne (**4**) vikiwemo viwili (**2**) vya Kamati ya Ajira na viwili (**2**) vya Baraza la Wafanyakazi vitawezeshwa. Pia, majukumu ya Vyama vya Wafanyakazi yatawezeshwa.

**Mwingiliano wa Majukumu, Sheria na Tozo**

**221.** ***Mheshimiwa Spika,*** kumekuwepo na mwingiliano wa majukumu, sheria, kanuni na tozo kati ya Wizara yangu na wizara nyingine hali ambayo imesababisha urasimu katika utoaji vibali na leseni katika ujenzi wa viwanda na uanzishaji wa biashara. Aidha, utitiri wa kodi na tozo umesababisha ongezeko la gharama za uwekezaji na uendeshaji wa biashara na hivyo kuwepo kwa malalamiko makubwa kutoka kwa wawekezaji na wafanyabiashara.

**222.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na mwingiliano huu Waziri Mkuu **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)** alitoa agizo la kuzitaka Wizara tano (5) na Taasisi zake kutatua changamoto hizi. Wizara yangu imeshiriki katika majadiliano na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; Viwanda na Biashara; Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Elimu, Sayansi na Teknolojia na Kilimo. Aidha, katika majadiliano hayo Taasisi zilizohusika ni pamoja na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA); Shirika la Viwango Tanzania (TBS); Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC); Wakala wa Barabara (TANROADS) na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA). Majadiliano yanaendelea kwa kuzingatia vigezo muhimu vilivyoainishwa kwenye Majukumu ya Wizara *(Instrument)*, Muundo, Sera, Sheria, *Blueprint*, weledi, viwango na utendaji bora wa kimataifa, jukumu la kiutendaji, kiusimamizi na kiuangalizi kwa lengo la kuondoa kasoro zilizopo na kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu katika Sekta husika.

**223.** ***Mheshimiwa Spika,*** Utatuzi wa changamoto hizi utapunguza urasimu wa upatikanaji wa vibali na leseni, kupunguza gharama za uwekezaji na uendeshaji biashara, kuvutia uwekezaji na kupanuka kwa Sekta Binafsi, Ajira na ukuaji wa Uchumi nchini.

**Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

**224** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara imetoa mafunzo na kusambaza vifaa maalum vya kukusanyia maduhuli kwa njia ya kielekroniki (PoS) kwenye vituo vyote vya ukusanyaji nchi nzima. Kwa upande wa Sekta ya Mifugo vifaa vimesambazwa kwenye Minada yote ya Upili na ya mipakani ambayo ni Pugu, Igunga, Ipuli, Nyamatala, Mhunze, Korogwe, Meserani, Themi, Weruweru, Kirumi, Lumecha, Longido, Waso, Murusagamba, Buhigwe na Kasesya. Aidha, kwa upande wa Sekta ya Uvuvi vifaa vimepelekwa katika vituo vya Mtukula, Simiyu, Rusumo, Murusagamba, Sirari, Sota, Kanyigo, Kabanga, Mganza, Bukoba, Ikola, Kasanga, Kipili, Tunduma, Kasumulu, Horohoro, Mbeya, Kilwa, Mwanza, Geita, Musoma, Mtwara na Mbamba-bay. Pia, Wizara imesimika mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji maduhuli ambayo imeunganishwa na mfumo wa malipo ya Serikali (*Government Electronic Payment Gateway*) katika Taasisi na Wakala zake za FETA, LITA TALIRI, TAFIRI, TVLA, LMU na MPRU. Lengo likiwa ni kuongeza tija na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na kupunguza mianya ya upotevu wa mapato.

**225.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuboresha na kusimika mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji maduhuli ya Mifugo kwenye minada yote ya awali husuan katika ukusanyaji wa Tozo za vibali vya kusafirisha Mifugo *"Animal Movement Permit''*. Pia, kuboresha Mfumo wa Uvuvi ili kuwezesha wafanyabiashara wanaosafirisha mazao ya uvuvi ndani na nje ya nchi kuomba leseni zao kwa kupitia mfumo wa kielektroniki *"Fisheries Licence Online Application"* tofauti na ilivyokuwa ikifanyika awali.

**Hifadhi ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi**

**226.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara imeanzisha Kitengo cha Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi katika Sekta za Mifugo na Uvuvi. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na Utekelezaji wa Azimio la Kilimo na Ufugaji Linazozingatia Tahadhari ya Mabadiliko ya Tabianchi (*Climate Smart Agriculture* – CSA). Azimio hilo liliandaliwa kwa pamoja kwa ushirikiano na Wizara ya Kilimo, na utekelezaji wake unafanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs). Aidha, tathmini ya athari ya Mazingira *(Environmental Impact Assessment – EIA)* za Miradi mitano (**5**) na *Environmental Audit – EA* kwa miradi miwili (**2**) zilifanyika katika utekelezaji wa Miradi inayohusu Sekta ya Mifugo kama ujenzi wa machinjio, viwanda vya kuchakata nyama, viwanda vya vyakula vya mifugo na maziwa. Katika tathmini hizo, Wizara imetoa maelekezo ya kimaandishi kuhusu miradi hiyo ili kulinda maslahi ya Sekta ya Mifugo bila kuathiri Mazingira.

**227.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kufuatilia athari za mabadiliko ya tabia nchi katika Ziwa Tanganyika. Matokeo yanaonesha kwamba mabadiliko ya tabia nchi yamesababisha ongezeko la joto katika Ziwa hali inayoathiri uzalishaji wa viumbe wa awali kwenye Ziwa (*Primary Productivity*) ambao ni chakula cha samaki. Pia, Wizara imeendelea kufuatilia na kufanya tathmini ya mifumo ya ikolojia husuan matumbawe, majani bahari na mikoko. Matokeo ya ufuatiliaji huu yatatoa hali halisi ya mifumo ikolojia katika maeneo yaliyohifadhiwa na kusaidia katika maamuzi ya usimamizi endelevu wa rasilimali hizo. Aidha, Wizara inaendelea kufuatilia hali ya mmomonyoko wa fukwe pamoja na kiasi cha taka zinazotupwa kwenye maeneo ya hifadhi kwani taka hizo ni hatari kwa mazingira.

**228.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara imedhibiti uvuvi haramu wa nyavu, mabomu na sumu ambapo uvuvi haramu umepungua kwa asilimia kubwa na kusababisha ukuaji wa bioanuai na viumbe hai. Aidha, wizara imetoa elimu kwa wagani wa mifugo na uvuvi pamoja na wadau wa sekta hizi juu ya kuzuia na kuhimili mabadiliko ya tabia nchi (Mitigation and Adaptation measures).

**229.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendesha mafunzo kwa wawezeshaji (TOT) kuhusu Azimio la Kilimo na Ufugaji linalozingatia Tahadhari ya Mabadiliko ya Tabianchi (*Climate Smart Agriculture* – CSA) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Jiji la Dodoma, Chamwino, Bahi, Kongwa, Chemba, Dodoma Vijijini, Mpwapwa, Ikungi, Iramba na Manyoni**.** Pia, Mradi wa miaka mitano (2018-2022) wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Maeneo ya Vijijini (*Ecosystem Based Adaptation for Rural Resilience* in Tanzania - EBARR) unaotekelezwa kwa pamoja na Wizara za Maji, Kilimo na Ofisi ya Rais - TAMISEMI utatekelezwa katika Halmashauri za Mvomero, Mpwapwa, Kishapu, Simanjiro na Wilaya ya Kaskazini A Unguja. Aidha, Wizara itaendelea kufuatilia athari za mabadiliko ya tabia nchi katika Ziwa Tanganyika na maziwa mengine.

**E: HITIMISHO**

**MAMBO YA KIUJUMLA**

**Gawio la Serikali**

**230.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Taasisi, Bodi na Wakala zilizopo chini ya Wizara ikijumuisha Sekta ya Mifugo (NARCO, LITA, TALIRI, TVLA, Bodi ya Nyama na Bodi ya Maziwa) na Sekta ya Uvuvi (TAFIRI, FETA na MPRU) zimetoa gawio kwa Serikali kwa mara ya kwanza lenye jumla ya shilingi **milioni 520** ikilinganishwa na miaka iliyopita ambapo hapakuwa na gawio (**Kiambatisho Na. 33).**

**Michango katika shughuli za Kijamii**

# HOTUBA YA WIZARA YA UFUGAJI NA UVUVI

**231.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Taasisi, Bodi na Wakala zilizopo chini ya Wizara zimetoa mchango wa shilingi **411,793,383** kwa jamii kwa ajili ya kuchangia shughuli za maendeleo na kukarabati miundombinu muhimu ikiwemo ukarabati wa majosho; kuchimba visima vya maji kwa matumizi ya binadamu na mifugo; kujenga kituo bora cha kukusanyia maziwa; ununuzi wa zana za uvuvi; ukarabati wa masoko na mialo; na kusaidia vyama vya ushirika vya wafugaji na wavuvi (**Kiambatisho Na. 34).**

**Miundombinu ya Kiuchumi**

**232.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu inayo faraja kubwa kuhusu ujenzi wa miundombinu mikubwa ya kiuchumi inayoendelea kujengwa nchini ikiwemo Reli ya Kisasa ya Mwendokasi (SGR), Mradi mkubwa wa Umeme wa Mto Rufiji (Stieglers' Gorge), upanuzi wa viwanja vya ndege na ununuzi wa ndege kubwa. Kuboreshwa kwa miundombinu hii, pamoja na mambo mengine utachochea uwekezaji mkubwa katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, kurahisisha usafirishaji wa mifugo, samaki na mazao yatokanayo na mifugo na uvuvi, kupunguza gharama za uzalishaji na hivyo kuwezesha viwanda vya ndani kushindana kibiashara na bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya nje ya nchi. Kwa muktadha huo, Wizara yangu inayo kila sababu ya kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanya maamuzi mazito na sahihi ya kutekeleza miradi hii mikubwa tena kwa fedha za ndani.

**234.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaendelea kufanya tathmini ya ubora wa miundombinu muhimu katika uhifadhi na usafirishaji wa mazao ya mifugo na uvuvi. Hatua hii itawezesha kuondoa kasoro zilizopo kwa kujenga na kufanya ukarabati wa miundombinu muhimu kama *refrigerated facilities* katika maeneo ya viwanja vya ndege na bandari. Ninamshukuru Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, **Mhe. Mhandisi Isack Aloyce Kamwelwe (Mb)** kwa kufanya ziara ya kubaini mahitaji ya utunzaji, usafirishaji wa mazao ya mifugo na uvuvi kwa masoko ya ndani na kimataifa.

**Uchumi na Biashara ya Mifugo na Uvuvi**

**235.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara hii imeendelea kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa. Katika mwaka 2018/2019 mauzo ya ndani ya nchi katika Sekta za Mifugo na Uvuvi (nyama, samaki, maziwa, mayai, ngozi na vifaranga) yanakadiriwa kuwa shilingi **trilioni 6.57**. Pia, mauzo ya mazao ya mifugo na nje ya nchi yalifikia jumla ya **shilingi 508,973,674,981.** Uzalishaji huu umechangia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa chakula nchini (kitoweo). Vilevile, mapato haya yanawezesha nguvu ya manunuzi (**Purchasing Power**) kwa wananchi na kuwezesha kulipwa kwa kodi mbalimbali wanaponunua mahitaji yao. Aidha, kwa upande mwingine mazao haya yanapouzwa nje ya nchi huliingizia Taifa fedha za kigeni, pia kuokoa fedha za kigeni ambazo zingetumika kuagiza mazao hayo nje ya nchi.

**236.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa nguvu kazi, mifugo inachangia asilimia 27 ya nguvu kazi katika kilimo (Kati ya Hekta milioni 16 zinazolimwa nchini hekta milioni 4.3 hulimwa kwa kutumia wanyama kazi) Chanzo: Wizara ya Kilimo**),** mifugo imekuwa ikifanya kazi nyingi ikiwemo usafirishaji wa mazao, usafirishaji wa vifaa vya ujenzi katika shule na zahanati, usafirishaji wa wagonjwa, kusomba maji na mizigo mingine. Mifugo kama mbwa na paka inatoa ulinzi kwa raia na mali zao. Vilevile, mifugo inazalisha nishati na mbolea ya samadi.

**237.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta za Mifugo na Uvuvi pamoja na masuala mengine zimeajiri Watanzania wengi na wawekezaji kutoka nchi za nje. Pia, kwa mujibu wa *National Panel Survey of 2015/16* iliyofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) mwaka 2015/16 ilionesha kuwa jumla ya Kaya **4,493,600** zinajihusisha na ufugaji sawa na asilimia **49.8** ya kaya **9,026,785** zote nchini. Vilevile, kwa mwaka 2018/19 Sekta ya Uvuvi ina jumla ya Watanzania zaidi ya **milioni 4** walioajiriwa katika shughuli zinazohusiana na uvuvi.

**238.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara ilipangiwa kukusanya shilingi **bilioni 40**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 makusanyo yalikuwa yamefikia shilingi **bilioni 63.3** ambayo ni sawa na asilimia **158** ya lengo ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2017/18 ya shilingi **bilioni 39.1** na mwaka 2016/17 shilingi **bilioni 25.9** kwa kipindi kama hiki sawia.

**239.** ***Mheshimiwa Spika,*** licha ya maduhuli yaliyokusanywa na Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi kufikia mwezi Machi, 2019 zimekusanya jumla ya shilingi **26,131,556,564** sawa na asilimia **84** ya lengo la shilingi **31,261,047,057 (Kiambatisho Na. 35).**

**240.** ***Mheshimiwa Spika,*** mapato mengine yanakusanywa kupitia mamlaka nyingine za Serikali ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) hukusanya kodi na tozo mbalimbali zikiwemo *Value Added Tax, Import Duty, Corporate Tax, Service Levy* na *Skills Development Levy*.

**F: SHUKRANI**

**241.** ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka uliopita yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani, mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, taasisi za fedha za kitaifa na kimataifa, taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini bila kusahau hamasa na ushiriki wa wananchi wakiongozwa na wawakilishi wao Waheshimiwa Wabunge na Madiwani.

**242.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua fursa hii kuzitambua na kuzishukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), na Umoja wa Nchiza Ulaya (EU), Serikali za Australia, Austria, Brazil, Canada, Jamhuri ya Czech, Hispania, Iceland, Ireland, Japan, Israel, Korea Kusini, Jamhuri ya Watu wa China, Marekani, Misri, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi pamoja na mashirika ya Umoja wa Mataifa ya FAO, IAEA, UNICEF, UNDP, UNIDO, SIDA, ILRI, CIAT na WHO. Pia, natoa shukrani kwa Mifuko ya Kimataifa ya GEF na IFAD kwa kuchangia katika maendeleo ya Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**243.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kutambua na kuzishukuru taasisi za kimataifa ambazo ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Korea (KOICA) Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Japan (JICA), Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DfID), Taasisi ya Raslimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika (AU/IBAR), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), Shirika la Maendeleo ya Uswisi (SDC), Shirika la Ushirikiano la Ujerumani (GTZ), United Nations University (UNU), Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA) kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**244.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, napenda kushukuru Mashirika na Taasisi za hiari za Bill and Melinda Gates Foundation, Association for Agricultural Reseach in East and Central Africa (ASARECA), International Livestock Research Institute (ILRI), World Wide Fund for Nature (WWF), Indian Ocean Commission (IOC), South West Indian Ocean Fisheries Commission (SWIOFC), Heifer Project Tanzania (HPT), Overseas Fisheries Cooperation Foundation of Japan (OFCF), Vetaid, Care International, OXFARM, Welcome Trust, World Vision, FARM Africa, Land O' Lakes, Building Resources Across Communities (BRAC), World Society for Protection of Animals (WSPA), Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine (GALVmed), Institute of Social Studies (ISS), International Land Coalition (ILC), British Gas International, Sea Sense, Indian Ocean Tuna Commission (IOTC), International Whaling Commission (IWC), SmartFish, Marine Stewardship Council (MSC), Mashirika na Taasisi mbalimbali za humu nchini zinazojihusisha na uendelezaji wa Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**245.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee niwapongeze sana Wafugaji na Wavuvi kote nchini kwa kazi nzuri wanazofanya za kutunza, kuzalisha na kulinda rasilimali za Taifa. Kazi wanazofanya ni nzuri na za heshima na kwamba Wizara yangu itaendelea kusimamia na kuunga mkono juhudi zao. Pia, niwashukuru wafanyabiashara, wawekezaji na wadau wote wa Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa dhamira yao njema ya kuendeleza sekta hizi muhimu.

**246.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Mheshimiwa Abdalah Hamisi Ulega**, Mbunge wa Jimbo la Mkuranga, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa msaada wake wa karibu katika kusimamia kazi za Wizara. Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu kwa Katibu Mkuu Uvuvi, **Dkt. Rashid Adam Tamatamah** na Katibu Mkuu Mifugo, **Profesa Elisante Ole Gabriel**, Wakurugenzi pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi kwa kazi nzuri sana wanazofanya kwa nia thabiti ya kuleta mageuzi makubwa katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, mapambano yanaendelea na kama tulivyokubaliana saa ni namba tu, kamwe hatutafungwa na muda, wala usiku katika kutekeleza wajibu na majukumu yetu "***Leaders must be willing to sacrifice for the sake of the vision***" .

**247.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa shukrani zangu za dhati na za kipekee kwa wananchi wangu wa Jimbo la Kisesa ambao muda wote wameendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya jimbo na kitaifa nataka niwahakikishie kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa juhudi, bidii, maarifa na ujasiri mkubwa sitajali jua wala mvua katika kuwatumikia. "***ni heri punda aumie lakini mzigo wa tajiri ufike***".

**248.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na **Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** imepania kuleta mapinduzi makubwa katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi ambapo uwekezaji unaoendelea nchini utalindwa kwa nguvu zote na hatutakubali nchi yetu kugeuzwa kuwa dampo na kwamba ulinzi wa rasilimali za mifugo na uvuvi utaendelea kuimarishwa.

**G: MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA**

**249.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya **shilingi 64,901,756,551.00.** Kati ya fedha hizo, **shilingi 31,774,378,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Mifugo na **shilingi 33,127,378,551.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Uvuvi. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:-

**Fungu 99: Sekta ya Mifugo**

**250.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaomba kutumia jumla ya shilingi **31,774,378,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Mifugo. Kati ya Fedha hizo, **shilingi 28,774,378,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 3,000,000,000.00** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo**.** Mgawanyiko wake ni kama ifuatavyo:-

(i) **Fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 28,774,378,000.**
- Mishahara: Shilingi 18,870,267,000; na
- Matumizi Mengine (OC): Shilingi 9,904,111,000.

(ii) **Fedha za Matumizi ya Maendeleo shilingi 3,000,000,000.**
- Fedha za Ndani: Shilingi **3,000,000,000; na**
- Fedha za Nje: **Shilingi - Sifuri.**

**Fungu 64: Sekta ya Uvuvi**

**251.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara inaomba jumla ya shilingi **33,127,378,551.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Uvuvi. Kati ya fedha hizo, **shilingi 18,432,461,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **14,694,917,551.00** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mgawanyiko wake ni kama ifuatavyo:-

(i) **Fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 18,432,461,000.00**
- Mishahara: shilingi **11,584,667,000.00; na**
- Matumizi Mengine (OC): shilingi **6,847,794,000.00.**

(ii) **Fedha za Matumizi ya Maendeleo shilingi 14,694,917,551.00**
- Fedha za Ndani: **shilingi 3,000,000,000.00,** na
- Fedha za Nje : **shilingi 11,694,917,551.00.**

**252.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara: www.mifugouvuvi.go.tz.

**253.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

## Wakazi Kidodi wachachamaa kunyanyaswa

INATOKA UK 4

inamuuma...hatumtaki hapa kijijini mtuondolee huyo mtu," alisema Kasasa huku akiwa na jazba.

Mkazi mwingine, Astery Mwanamuhehe, alihoji kama mwenyekiti amejeruhiwa hivyo, raia wa kawaida hali itakuwaje.

"Afande usituone hivi tuna hasira, tulitaka kuandamana kuja ofisini kwako huyu mtu hatufai kabisa hapa kijiji ni muuaji," alidai Mwanamuhehe.

Akihoji kitendo cha mtuhumiwa kuwekwa mahabusu bila kufikishwa mahakamani, mkazi wa kijiji hicho, Mariam Maulid, alisema polisi inangoja nini kumfikisha mtuhumiwa huyo mahakamani.

"Namnukuu Rais Dk. John Magufuli 'mwizi mmemkamata na kielelezo, sasa mnasubiri nini kutoa haki', upelelezi wa kina upi na wakati mwenyekiti amejeruhiwa vibaya na ameandikiwa rufaa kutoka Kituo cha Afya Kidodi kwenda Hospitali ya Mikumi, hamuoni kuwa ni hali ya hatari?" Alihoji Maulid.

Hata hivyo, ASP Mwambigili, akitoa ufafanuzi kuhusu madai hayo, alisema jeshi la polisi halina mamlaka ya kumhamisha mtu sehemu anayoishi na kwamba atahakikisha analifanyia kazi suala hilo na kurejesha amani kwa wananchi.

"Nina miezi miwili tangu nihamie hapa sina kumbukumbu zake za matukio ya nyuma nitalifanyiakazi tukio hili, ninawashukuru kwa utulivu na usikivu wenu jeshi langu limechukua hatua ya kumweka mahabusu mtuhumiwa na hatua za kisheria zaidi zitachukuliwa, msiogope kwenda kwenye shughuli zenu za kujutafutia riziki hakuna atakayewadhuru," alisema ASP Mwambigili.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti Sanane alilalamika mtuhumiwa kumtamka kuwa atamuua kwa madai kuwa anamkwamisha katika masuala yake ya kumiliki ardhi.

Mei 17, mwaka huu, Sanane wakati akitoka kwenye mkutano wa halmashauri ya kijiji kwenda nyumbani kwake akiwa na nyaraka za serikali, alidai kuvamiwa na kushambuliwa na mtuhumiwa.

"Nilivamiwa akanishika shingo akanirushia ngumi kwenye shavu jichoni nikaanza kuvuja damu, polisi walimweka mahabusu na walinipa fomu namba tatu nikaja kupata matibabu, lakini leo (juzi) siku ya tatu daktari ameona jicho na hali yangu kwa ujumla sio nzuri, wameniandikia rufaa kwenda Hospitali ya Mikumi," alisema Sanane.

Alisema kama si wasamaria wema kumwokoa pengine leo angeitwa marehemu.

Mtuhumiwa yuko mahabusu akiendelea kushikiliwa na jeshi hilo.

# Waziri atishia kuvunja mkataba na kiwanda

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, ametishia kuvunja mkataba na kiwanda cha kutengeneza mabomba cha Tanzania Steel Pipe (TSP) kilichopo Ubungo jijini Dar es Salaam baada ya kushindwa kupeleka kwa wakati mabomba kwa ajili ya miradi ya maji katika kijiji cha Nyang'hwale-Geita na Longido mkoani Arusha.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika kiwanda hicho jana, kufahamu tatizo linalosababisha mabomba hayo kushindwa kufika kwenye maeneo ya kazi kwa wakati na kusababisha utekelezaji wa miradi hiyo kusuasua bila sababu za msingi.

"Nategemea kuona Kiwanda cha Tanzania Steel Pipe kinaheshimu mkataba tuliongia nao wa kupeleka mabomba ya maji kwa ajili ya kazi za ujenzi wa miradi ya Nyang'hwale-Geita na Longido-Arusha iweze kukamilika....Kinyume cha hapo sitakuwa tayari kuona miradi hiyo ikishindwa kukamilika kwa wakati na wananchi kukosa maji, niko tayari kutafuta kampuni nyingine itakayofanya kazi yetu kwa uaminifu," lisema Prof. Mbarawa na kuongeza:

"Nimekuwa nikikerwa na tabia ya makandarasi kushindwa kukamilisha miradi ya Nyang'hwale na Longido kwa sababu ya upatikanaji wa mabomba si mzuri bila kuwapo sababu zozote za msingi kufika... kwangu kiwandani hapa ni kutaka kufahamu kuna tatizo gani kwa kuwa ndio wenye mkataba wa kupeleka mabomba kwenye miradi hiyo."

Prof. Mbarawa alikutana na Meneja Biashara wa TSP, Ryan Koh, na kumuonya kuwa endapo wataendelea kutoheshimu mkataba huo na kuendelea kuwa sababu ya miradi hiyo kuchelewa, hatasita kusitisha mkataba huo na kutafuta kampuni nyingine.

Waziri Mbarawa alisisitiza kuwa hatoweza kuvumilia ucheleweshwaji wa mabomba hayo, huku wananchi wa maeneo hayo wakiendelea kuteseka.

"Nimeongea na Mkurugenzi wa Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira wizarani, ahakikishe kama kuna madeni yoyote mnayodai awalipe kufikia Jumatano (leo)," alisema Mbarawa.

Kwa upande wake, Koh alisema amepokea ujumbe huo na wataanza kupeleka mabomba hayo mara moja katika maeneo ya kazi ya miradi hiyo na kumshukuru Prof. Mbarawa kwa kufika kiwandani kusikiliza changamoto zao.

Miradi ya Maji ya Nyang'hwale na Longido ni moja ya miradi mikubwa inayoendelea kutekelezwa na Serikali kwenye maeneo yenye changamoto kubwa ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa lengo la kufikisha huduma hiyo muhimu kwa kila mwananchi.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega, mkoani Simiyu, Vumi Magoti (kushoto), akipokea msaada wa mifuko ya saruji kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya TPB, Sabasaba Moshingi, kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Sekondari Dk. Chegeni, iliyopo Kata ya Nyashimo, wilayani humo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zitto ambana Lugola ubakaji wajane

INATOKA UK. 2

kuonyesha viashiria vya uchochezi kuwa zitachukuliwa hatua kali za kisheria na kwamba serikali inaendelea kuzifuatilia.

Zitto alisema utafiti uliofanywa na taasisi zisizokuwa za kiserikali, umebaini kuwapo kwa vitendo vya unyanyasaji, huku serikali ikiwa imefumba macho kwa kutochukua hatua zozote za haraka na za kisheria.

Zitto alisema katika jimbo lake la Kigoma Mjini, kwa takribani miaka mitatu sasa kumezuka tabia ya vijana kujipata oil chafu na kuvamia wanawake, hasa wajane na wanawake ambao wenza wao hawaishi nao, na kuwabaka na wakati mwingine hata kuwajeruhi kwa kipigo.

Alisema usiku wa kuamkia juzi, mama mmoja alijeruhiwa kwa kupigwa nondo kichwani na mmoja wa vijana na mwingine amechomwa kisu na wote wako hospitalini.

Zitto alibainisha kuwa shirika lisilokuwa la kiserikali la Tamasha, limefanya utafiti wa matukio hayo na tangu mwaka 2016, limebaini matukio 43 ya aina hiyo yametokea Kigoma na limemwandikia barua waziri, mbunge na taasisi mbalimbali zisizokuwa za kiserikali, likiomba vikao ili kuangalia namna ya kutatua changamoto hiyo.

"Kwa hiyo, nimelileta hapa bungeni ambacho ndicho chombo cha wananchi na tukio hili ni tukio la aibu kwa kweli na mimi kama Mbunge wa Kigoma Mjini, najisikia vibaya, najisikia aibu na linanisononesha, inanisikitisha na ninaona aibu sana.

"Kwamba tunaweza tukashindwa kulinda kinamama, dada zetu, shangazi zetu, watoto wetu kufanyiwa vitendo vya kinyama ambavyo wanaendelea kufanyiwa. Kwa hiyo, naomba kiti, nisingependa niombe mjadala kwa kuwa ni jambo ambalo ndio kwanza nimelileta na watu hawatakuwa na takwimu za kutosha ili kujadili.

"Lakini, naomba kiti kiielekeze serikali ilete ndani ya Bunge taarifa ni ya aina gani hatua ambazo wamezichukua mpaka sasa za kukabiliana na hali hii kukomesha vitendo hivi na kuchukua hatua kali za kisheria kwa watu wote ambao wanadhalilisha, kumiza na kunyanyasa wanawake hata katika Kata ya Mwanga Kusini na Kata ya Kasibuba katika Halmashauri ya Kigoma Mjini," Zitto aliwasilisha.

Kutokana na hoja hiyo, Giga aliitaka serikali kutoa taarifa kuhusu matukio hayo.

Baada ya agizo hilo, Waziri Lugola alisimama na kusema: "Mheshimiwa Mwenyekiti, ubakaji ni kosa la jinai, vitendo hivi vya makosa ya namna hii vimekuwa vikitokea katika nchi yetu na siyo Kigoma tu, bali katika maeneo mbalimbali.

"Makosa haya huwa yanadhibitiwa na Jeshi la Polisi na watuhumiwa wanapopatikana na ushahidi, wanafikishwa mahakamani na kuwajibika.

"Lakini, Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende pia kusema bayana kwamba kwa Mkoa wa Kigoma matukio ambayo Mheshimiwa Zitto Kabwe ameyazungumzia ni matukio ambayo ni kweli yanawadhalilisha kinamama, vitendo ambavyo sisi kama serikali hatuwezi kuvipa nafasi na kuvivumilia.

"Na niseme bayana kuwa vilianzia 2014, Mheshimiwa Mwenyekiti, kinamama wa Kigoma ambao ni wajane au wasiokuwa na wanaume au waume zao wamesafiri, walikuwa wanakuta mtu ambaye haonekani kwa macho na mwanamama anajikuta sehemu zake za siri zimeloa halafu anaponyanyuka anaona kama mtu, anapotaka kumshika yule mtu, anateleza.

"Ndipo dhana ya udhalilishaji kwa mtindo wa teleza ilipoanzia na ikaonekana walikuwa wanaingilia kwenye pembe ya nyumba au kwenye kona.

"Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo hivi vimeendelea kudhibitiwa na nilipopata barua hii na kushirikiana na Mheshimiwa Zitto Kabwe pamoja na Mkurugenzi wa Twaweza, Aidani Eyakuze, nilitoa maelekezo kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma.

"Lakini mwenyekiti jambo hili si la ukubwa huo kama inavyoelezwa na hizi taasisi zisizokuwa za kiserikali zinazotoa huu utafiti ambao Mheshimiwa Zitto Kabwe anausema, na tukiangalia kwenye kumbukumbu zetu kwenye vitabu vya polisi, mpaka jana katika mwaka huu hakuna taarifa yoyote ambayo inahusisha tukio la ubakaji.

"Ninachokisema mimi kama Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, sina taarifa yoyote na kama kuna taarifa, nipo tayari kuondoka hata sasa kwenda Kigoma ili kuona kama kuna ukubwa wa taarifa ambayo imetolewa hapa bungeni, sina sababu ya mimi ya kusema uongo."

Hata hivyo, Giga alimtaka Waziri Lugola kwenda Kigoma kushughulikia changamoto hiyo, akieleza kuwa vitendo vya unyanyasaji havipaswi kufumbiwa macho.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.

## MCHANGANYIKO

**KIWANJA KINAUZWA,** KIWANJA KUNAUZWA PLOT NO. 97 BLOCK M, MEDIUM SIZE KILWA MASOKO MTAA MIINA OPOSITE UWANJA WA NDEGE BEI MAELEWANO. TEL. 0712 566677, 0753 907281.

NIPASHE
NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya Mwanzo: **MANZESE / SINZA**
Usimamizi wa Mirathi **No. 83/2019**

Ombi la **OTHMAN RAMADHAN NTARRU** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu **MWAMVUA HASSAN KATALAMBULA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 30/05/2019.

kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe **15/05/2019**

115241002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**IRINGA**

**SHAURI LA MAOMBI YA KUKAZIA HUKUMU NA.9 YA MWAKA 2019**

**SUMI FIDELIS MBANGWA……….......MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**CHINA HENAN INTERNATION COOPERATION GROUP CO. LTD (CHIKO) ..............MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

Shauri tajwa hapo juu limepangwa kutajwa tarehe 28/6/2019 saa tatu kamili (9:00) asubuhi hivyo wajibu maombi haya anatakiwa kufika katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Iringa au atume mwakilishi wake.

Fahamu kuwa endapo hautafika siku hiyo au kutuma mwakilishi wako, maombi yatapangiwa tarehe ya kusikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo.

215239902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA –MWANZA**
**SHAURI NA 523 LA 2018**

**LETSHEGO BANK (T) LIMITED....................................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**DONALD MTATIRO FLAVIAN............................................MDAIWA**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

**KWA: DONALD MTATIRO FLAVIAN**

Unafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua shauri/ ombi dhidi yako katika baraza na nyumba mkoa wa Mwanza, ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 27/06/2019 katika chumba cha baraza, barabara ya posta jengo liko mkabala na mahakama kuu ya biashara, Tanzania.

kwa hivyo unatakiwa kuhudhuria katika baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria.

KAA- ukijua kwamba kushindwa kufika, baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo

imetolewa nami kwa amri na chapa ya baraza leo tarehe 09/05/2019.

115240902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**MAOMBI NA: 111/2018**

**IGNATIO MUHIMBA ................MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
1. YUSUPH H. KAIJAGE
2. ESTER RUHUZI .................. MDAIWA

KWA: ESTER RUHUZI
(POPOTE PALE MLIPO)

Mnaarifiwa/Unaarifiwa kuwa maombi Na. 111/2018 yamepangwa kutajwa tarehe 11/06/2019 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza , E. MOGASA saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 20.05.2019

115241402

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**MATUKI CHACHA MAGERE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 591 DGQ**

**TOYOTA NOAH.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **KY/BI/I/126.**

115240201

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**BUKOBA, KAGERA**
**MAOMBI NA. 85 YA 2019**

SHABAN HUSSEN KICHWABUTA ......MDAI
DHIDI YA
1. FINCA MICROFINANCE BANK LTD
2. JOSINA COMPANY LIMITED & AUCTIONEER
3. NMB BANK BUKOBA BRANCH
4. L. J INTERNATIONAL LTD
5. YASINI B. SWALEHE

... MDAIWA

KWA: YASINI B. SWALEHE
(POPOTE PALE MLIPO)

Unaarifiwa kuwa kesi Na. 85/2018 yamepangwa kutajwa tarehe 20/06/2019 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza , E. MOGASA SAA 2:00 asubuhi, mahali- Bukoba Mjini.

Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa .Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja na hukumu kutolewa dhidi yako.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hii leo tarehe 20.05.2019

115241502

KWA
MATANGAZO
MADOGO
MADOGO
TUPIGIE
0767 223311

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO,
NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku
Tupigie 0767 223 311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI MICHEZO

# MKHITARYAN KUIKOSA CHELSEA FAINALI EUROPA




**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal imethibitisha kwamba, Henrikh Mkhitaryan hataweza kusafiri na timu kwenda Baku kwa ajili ya fainali ya mchezo wa Kombe la Europa wiki ijayo dhidi ya Chelsea.

Awali kulikuwa na jitidaza za kujaribu kumhakikishia usalama wake raia huyo wa Armenia ambaye nchi yake ina mgogoro na Azerbaijan na raia wa nchi mbili hizo hawaruhusiwi kuingia nchi mojawapo.

Mkhitaryan alishindwa kwenda na Arsenal nchini Azerbaijan mapema msimu huu wakati 'Washika Bunduki' hao walipocheza mchezo wa makundi dhidi ya Qarabag, pia alikosa mechi zote zilizochezwa na timu za Azerbaijan wakati akicheza pale Borussia Dortmund kwa sababu hizo hizo.

Mapema wiki hii balozi wa Azerbaijan nchini Uingereza, Tahir Taghizadeh, aliiambia Sky Sports: "Ninachoweza kuwahakikishia ni kwamba serikali ya Azerbaijan itafanya kila kitu kinachohitajika kwa ajili ya usalama wa kila shabiki, wachezaji na benchi la ufundi kwa ajili ya mchezo huu."

Halafu akasema Mkhitaryan, aende Baku, atakuwa salama."

Taarifa ilichapishwa kwenye tovuti ya Arsenal jana ilisema hawatasafiri na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30.

Taarifa hiyo ilisema: "Tunasikitika kutangaza kwamba, Henrikh Mkhitaryan hatasafiri na kikosi kwa ajili ya fainali ya Kombe la Europa dhidi ya Chelsea."

# *Maguire atakiwa kumrithi Kompany*

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inafikiri kumsajili beki Harry Maguire ili kuziba nafasi ya nahodha wake, Vincent Kompany ambaye ametangaza kuondoka katika dimba la hapo Etihad.

Kompany ambaye ameichezea kwa miaka 11 Man City, amemaliza msimu wake wa mwisho na sasa Kocha Pep Guardiola anaelekeza nguvu zake kwa Maguire mwenye umri wa miaka 26.

City wapo tayari kutoa dau la pauni milioni 75 kwa mlinzi huyo ambaye dirisha kubwa lililopita alitakiwa kwa nguvu zote na wapinzani wao Manchester United, lakini inajulikana kwamba Leicester wanataka City wavunje rekodi ya uhamisho ya dunia kwa beki huyo kwa ajili ya kuinasa saini yake.

Leicester watataka dau la pauni milioni 80 kwa ajili ya kumruhusu Maguire kuondoka King Palace na dau hilo litalipiku dau la pauni milioni 75 ambalo Liverpool walitumia Januari mwaka jana kuvunja rekodi ya uhamisho ya dunia kwa walinzi wakati walipomnunua staa wa kimataifa wa Uholanzi, Virgil van Djik kutoka Southampton.

Maguire amekuwa chaguo la kwanza la Guardiola kuchukua nafasi ya Kompany na kocha huyo alidiriki hata kumfuata uwanjani katika mechi dhidi ya Leicester hivi karibuni akimweleza alivyokoshwa na kiwango chake.

Huu ni mwendelezo wa Maguire kung'ara baada ya kutamba katika michuano ya Kombe la Dunia na kikosi cha timu ya Taifa ya England nchini Urusi katikati ya mwaka jana, ambapo United walianza kumfukuzia kwa kasi.

Hata hivyo, Maguire alisaini mkataba mpya wa miaka mitano na Leicester Septemba mwaka jana baada ya uhamisho wake wa kwenda Old Trafford kushindikana na mkataba huo umeiweka Leicester katika nafasi nzuri ya kutomuuza kwa bei rahisi.

Leicester waliweka ngumu wakati City walipomtaka winga wao wa kimataifa wa Algeria, Riyad Mahrez katika dirisha dogo la Januari ambapo walizitia kapuni ofa zao mbalimbali kabla ya kuamua kumuuza katika dirisha kubwa la majira ya joto mwaka jana ambapo waliikamua City pauni 60 milioni ambazo mpaka sasa ni rekodi ya uhamisho klabuni hapo.

Kocha wa Leicester City, Brendan Rodgers ni shabiki mkubwa wa Maguire na Leicester wana historia ya kuwatilia ngumu wachezaji wao pindi wanapotakiwa na klabu mbalimbali nyingine ikiwamo Manchester City yenyewe.




# Ndombele kumbadili Pogba Manchester Utd




**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imeripotiwa kumnyatia Tanguy Ndombele ili kuziba pengo la Paul Pogba kama ataondoka hapo Old Trafford.

Man United imebainisha kwamba, inataka kumsajili kiungo huyo wa Lyon, ambaye amekuwa na msimu bora kabisa huko kwenye klabu hiyo ya Ligue 1.

Lakini uhamisho wa Ndombele utacheleweshwa kidogo ukimsubiri Pogba afanye uamuzi wake.

Pogba ambaye alisajiliwa kwa pauni milioni 89 amekuwa haeleweki kwenye kikosi hicho akidai kwamba ndoto zake ni kwenda Real Madrid.

Pogba alisema anataka kwenda Real Madrid hasa kwa kipindi hiki ambacho Zinedine Zidane amerudi kwenye kikosi hicho hapo Bernabeu.

HABARI MICHEZO

# Lipp awataja Pochettino, Sarri kumrithi Allegri Juve

**LONDON,** England

KOCHA wa zamani wa Juventus, Marcello Lippi, amedokeza kwamba kocha wa Tottenham, Mauricio Pochettino au Maurizio Sarri wa Chelsea ndio wenye nafasi ya kumrithi Massimiliano Allegri kwa mabingwa hao wa Serie A.

Allegri ataondoka Juventus baada ya mchezo wa Jumapili watakaposafiri kwenda Sampdoria na sasa Lippi amezungumzia kuhusu mrithi wa kocha huyo mwenye umri wa miaka 51.

Kocha wa Chelsea na kocha wa zamani wa Napoli, Sarri pia wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kurudi Italia baada ya kudumu kwa msimu mmoja tu kwenye Ligi Kuu, huku Pochettino amekuwa akihusishwa na kupewa nafasi hiyo pamoja na Simone Inzaghi na Antonio Conte.

Sarri na Pochettino wamefuzu kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool, huku Chelsea ikiivaa Arsenal kwenye fainali ya Ligi ya Europa.

Na Lippi ambaye aliiongoza Juventus kushinda mataji matano ya Serie A wakati wa kipindi chake cha ukocha, anaamini majina hayo ndiyo yenye nafasi kubwa ya kutwaa taji hapo Juve.

"Kwa nini klabu kama Juventus bado haijamtangaza mrithi wa Allegri, naamini baada ya muda mfupi," alisema Lippi mwenye umri wa miaka 71.

"Tutaona kama kocha mpya atatoka kwenye majina ya wale waliopo kwenye Ligi Kuu ya England, halafu tutaelewa sababu ya kuchelewa kutangaza jina lake.

"Mwaka huu klabu za Uingereza zimekuwa bora Ulaya, lakini mambo huwa yanazunguka. Nafikiri Sarri ana nafasi kubwa ya kushinda fainali ya Ligi ya Europa, halafu kuna Pochettino."






# EMERY AFUNGUKA MBAPPE MADRID

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa zamani wa Paris Saint-Germain, Unai Emery (kwa sasa Arsenal), amesema Kylian Mbappe alitaka kujiunga na Real Madrid kabla ya miamba hao wa Ufaransa kumshawishi mshambuliaji huyo kubaki.

Mbappe kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na miamba hao wa La Liga baada ya nyota huyo wa PSG wiki hii kudokeza kuhusu majaliwa yake hapo klabuni. Mabingwa hao wa Ligue 1, walikanusha taarifa hizo na kusisitiza kwamba mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwenye umri wa miaka 20, atabakia hapo jijini Paris.

Hata hivyo, kocha wa Arsenal, Emery alibainisha kwamba mpango wa Mbappe kutaka kusajiliwa Madrid wakati wake akiwa PSG, ambapo alitaka kuondoka mwishoni mwa msimu wa 2017-18.

"Kuna wakati, alikuwa analazimisha kutaka kuondoka PSG," alisema Emery akiambia Cadena SER. "Nilizungumza naye na hata baba yake ili aweze kubakia.

"Alitaka kwenda Real Madrid, na pia alikuwa na nafasi ya kwenda Barcelona, lakini alitaka zaidi kwenda Madrid, kati ya watu waliomshawishi kubakia, mimi nilikuwa mmoja wao."

Mbappe alijiunga na PSG kwa mkopo akitokea Monaco, na baadaye akanunuliwa kwa mkataba wa kudumu wa euro milioni 180, Agosti 2017.

Tangu hapo Mbappe alifunga mabao 59 katika mashindano yote, na amefunga mabao 32 kwenye Ligi Kuu msimu huu.

# Kroos akubali kuongeza mkataba Real Madrid

**MADRID,** Hispania

TONI Kroos amekubali kuongeza mkataba wake na Real Madrid hadi mwaka 2023, miamba hao wa La Liga wamethibitisha.

Majaliwa ya kiungo huyo hapo Madrid yalikuwa shakani baada ya kocha wake mkuu, Zinedine Zidane mwezi uliopita kushindwa kuthibitisha kama atabakia klabuni hapo.

Na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, ambaye alijiunga nao akitokea Bayern Munich mwaka 2014, sasa amekubali kusaini mkataba wa miaka minne ambao utamfanya kukaa hapo hadi mwaka 2023. Mkataba wake wa awali ulikuwa unamalizika mwaka 2022.

Kroos amecheza mechi 28 za La Liga msimu huu na alikuwa sehemu ya kikosi kilichoshinda mara tatu mfululizo taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wa zama za mwanzo za Zidane hapo katika dimba la Santiago Bernabeu.

Pia alikuwa kwenye kikosi cha Ujerumani kilichobeba Kombe la Dunia mwaka 2014 na ameshinda mataji manne ya ligi na matano ya Klabu Bingwa ya Dunia.


Madrid walimaliza msimu huu wa Ligi Kuu kwa kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Real Betis Jumapili.

Ilitarajiwa kwamba, Zidane atakifumua kikosi hicho na hivyo kulikuwa na uwezekano wa kiungo huyo kuondoka kwa miamba hao mwishoni mwa msimu huu. Golikipa aliyekaa kwa muda mrefu, Keylor Navas atafuata nyayo zake, Marcelo na Isco wanaweza kubaki, lakini majaliwa ya Gareth Bale bado hayajulikani.

Beki wa Porto, Eder Militao tayari amekubali kujiunga na miamba hao kwa ajili ya msimu ujao wa 2019-20 wakati ripoti kutoka nchini Ujerumani zinaeleza kuwa, mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt, Luka Jovic anakaribia kutua hapo.



# DONDO SOKA
## MAGAZET ULAYA




# POGBA, HAZARD, MBAPPE NDANI REAL, BALE, ISCO NJE

●●● Eder Militao, Luka Jovic, Neymar wanahusishwa kwa kiasi kikubwa kujiunga na klabu hiyo...

**MADRID,** Hispania

UONGOZI wa Real Madrid unaonekana umepania kumwaga fedha sokoni ili kuimarisha kikosi cha Zinedine Zidane na kujaribu kupunguza pengo linalokua kwa kasi kwenye La Liga dhidi ya wapinzani wao, Barcelona.

**Zidane ameonyesha ishara kwamba hataogopa kuisuka upya timu yake ambayo imemaliza msimu ikiwa nafasi ya tatu, pointi 19 nyuma ya vinara Barca, baada ya kupoteza mechi yao ya funga msimu kwa mabao 2-0 nyumbani dhidi ya Real Betis Jumapili.**

Gareth Bale aliishia kukaa benchi bila kutumika dhidi ya Betis, wakati huu mustakabali wake wa baadaye hapo ukionekana safari ya kuondoka Santiago Bernabeu imekaribia, huku kipa Keylor Navas pia akitarajiwa kuondoka.

Lakini ni vipi Madrid inaweza kuonekana kuelekea msimu wa 2019-20? Omnisport imetazama wachezaji wanaoweza kutua na wanaoelekea kufunguliwa mlango wa kutokea kwa 'Los Blancos' hao.

Nyota Eder Militao, Luka Jovic, Kylian Mbappe, Paul Pogba, Neymar, Eden Hazard wanahusishwa kwa kiasi kikubwa kujiunga na klabu hiyo.

Madrid tayari imeshaonekana kuhangaikia saini ya beki wa kati wa Porto, Militao, ili kuimarisha safu yake ya ulinzi ambayo imeonekana kuwa uchochoro kwa kuruhusu mabao 46 kwenye ligi msimu uliopita.

Kocha wa zamani wa Madrid, Fabio Capello amesema klabu hiyo ina euro milioni 500 za kutumia sokoni, hivyo Zidane anaweza kukamilisha malengo yake kwa wachezaji anaowawinda. Pogba kwa muda mrefu amekuwa akiwindwa na klabu hiyo licha ya kuwa kinara wa ufungaji Manchester United kwenye EPL msimu huu, lakini anaweza kuruhusiwa kuondoka.

Mbappe anaweza kuwa usajili sahihi kabisa kwa Madrid na ameonyesha ishara kwamba atafungua milango ya kuondoka Paris Saint-Germain wakati akikabidhiwa tuzo mbili za Ligue 1; Mchezaji Bora wa Mwaka na ile ya Kinda Bora wa Msimu. Mbappe anaweza kuigharimu Madrid rekodi ya dunia wakati Neymar naye akiwa mchezaji mwingine mwenye uwezekano wa kuondoka.

Nyota huyo wa zamani wa Barca, ameripotiwa ameshindwa kuzoea vema katika jiji hilo la Ufaransa na anaweza kuwa nyota ajaye wa Madrid baada ya mwaka jana kushangaza kwa kumuuza Cristiano Ronaldo Juventus, lakini Madrid ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikivutiwa na Eden Hazard - ambaye amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake na Chelsea - inaweza kukomaa zaidi na nyota huyo wa Brazil.

Hata hivyo, licha ya kuwa na fungu kubwa la kutumia sokoni, ni vigumu kuona Madrid ikisajili washambuliaji wanne wapya; Hazard, Jovic, Mbappe na Neymar, na wakati huu PSG - ikitazamwa kwa matumizi makubwa katika usajili kinyume na mapato yake - hakika haitawaruhusu washambuliaji wake wote kuondoka kwa pamoja katika dirisha hili.

Na wakati usajili huo ukitazamwa, mlango wa kutokea tayari unaonekana kuwa wazi kwa Gareth Bale, Keylor Navas, Isco, Raphael Varane na Luka Modric.

Na kikosi cha kwanza cha Madrid kwa msimu ujao wa 2019-20, kinaonekana kinaweza kuwa hivi; Thibaut Courtois, Dani Carvajal, Sergio Ramos, Eder Militao, Marcelo, Toni Kroos, Casemiro, Paul Pogba, Kylian Mbappe, Luka Jovic na Eden Hazard.

## ZISIKUPITE

### BAYERN YAJIAMINI KWA SANE

BAYERN Munich imeongeza kujiamini kwamba inaweza kumsajili mshambuliaji Mjerumani Leroy Sane, 23, kutoka Manchester City majira haya ya joto. ***(Mirror)***

### ARSENAL YAMTAKA MURARA

ARSENAL imetoa ofa ya kumsajili kipa wa Valencia, Mbrazil Norberto Murara baada ya kuzungumza na mawakala wa mlinda mlango huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Star)***

### HAZARD RUKSA KUTUA MADRID

CHELSEA inajiandaa kumuuza mshambuliaji wa kimataifa wa Ubelgiji, Eden Hazard, 28, kwa Real Madrid kwa sababu haitaki kumuacha aondoke bure wakati mkataba wake utakapomalizika mwaka ujao. ***(Mail)***

### UNITED YATAJA DAU LA POGBA

MANCHESTER United itahitaji ada ya uhamisho kiasi cha pauni milioni 138 kwa kiungo wa kimataifa wa Ufaransa, Paul Pogba, 26. ***(Star)***

### FELIX LULU REAL, UNITED

MANCHESTER United ipo tayari kufika dau la pauni milioni 105 zinazohitajika ili kuvunja mkataba wa kiungo mshambuliaji wa Benfica, Mreno Joao Felix, 19, ingawa itakabiliwa na ushindani mkubwa kutoka kwa Real Madrid. ***(Record, via Mirror)***

### ARSENAL KUWAJAZA WACHEZAJI

ARSENAL itawazawadia wachezaji wake bonasi kati ya pauni 100,000 na pauni 500,000 kama itaichapa Chelsea na kutwaa ubingwa wa Europa League katika mechi ya fainali itakayopigwa mjini Baku, Azerbaijan Mei 29, mwaka huu. ***(Mail)***

### GIROUD AONGEZA MWAKA

CHELSEA inatarajiwa kuthibitisha kwamba straika Mfaransa Olivier Giroud, 32, amekubali kuendelea kutumikia klabu hiyo kwa mwaka mmoja zaidi. ***(London Evening Standard)***

### CONTE AKUBALI KUINOA INTER

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Antonio Conte, amekubaliana malipo binafsi ya kuinoa Inter Milan kama kocha wao mpya majira haya ya joto. ***(Guardian)***

### YAGOMEWA KWA KOULIBALY

MANCHESTER United imetoa ofa ya pauni milioni 95 kwa beki wa kati wa Napoli na Senegal, Kalidou Koulibaly, 27, ambazo zimekataliwa. ***(Gazzetto dello Sport journalist Nicolo Schira, via Sun)***

### GOMEZ AIVUTIA SPURS

SPURS inavutiwa na straika wa Celta Vigo, Maxi Gomez, ambaye anaruhusiwa kuvunja mkataba wake kwa pauni milioni 43, na inataka kumsajili mshambuliaji huyo raia wa Uruguay kama msaidizi wa Harry Kane. ***(Star)***

### KOMPANY KUIBOMOA CITY

KOCHA mchezaji mpya wa Anderlecht, Vincent Kompany, 33, yupo tayari kumuona kocha wa makinda wa Manchester City, Simon Davies na Mkuu wa Idara ya Michezo, Sam Erith, wakiachana na mabingwa hao wa EPL na kumfuata katika klabu hiyo ya Ubelgiji. ***(Telegraph)***

HABARI MICHEZO

## Mabondia JKT, Ngome kukinukisha Dar

**Na Mwandishi Wetu**

PAMBANO kali la ngumi za kulipwa na ridhaa litakaloshirikisha mabondia mbalimbali nchini wakiwamo wa Jeshi la Kujenga Taifa na Ngome linatarajiwa kupigwa Juni 7, mwaka huu, katika Ukumbi wa Club 361 Mwenge Jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mratibu wa Ufundi wa pambano hilo, Yassin Abdalah Ustaadh, alisema upinzani wa JKT na Ngome ni wa kihistoria na kuwataka mashabiki na wapenzi wa ngumi kujitokeza kwa wingi kuweza kushuhudia mpambano huo.

Aliwataka mabondia wa ngumi za kulipwa watakaopanda ulingoni siku hiyo kuwa ni Nassib Ramadhani atakayezichapa na Mohamed Kashinde, wakati Kiasi Ally akinyukana na Shadrack Ignas, huku Kudura Tamimu akitoana jasho na Baina Mazola.

Alisema pambano lingine la kuvutia lenye lengo la kuvunja historia ya Japhet Kaseba kumkaribisha katika ngumi, mchezaji wa ngumi na mateke, Jeremia Jackson atakayecheza na Hashim Masungo.

Kwa upande wa Kocha wa Ngome, Hassan Mzonge, alisema wamejiandaa vema na mmoja wa mabondi watakaopambana katika uzito wa kilo 81 ni Koplo Selemani Kidunda na kutuma salamu kwa JKT.

Kwa upande wake Katibu wa Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa nchini, Yahaya Poli, aliwapongeza waandaaji kutekeleza sera ya kamisheni kuchanganya mapambano ya kulipwa na ridhaa na kufafanua kuwa tayari kibali kimetolewa kwa ajili ya kufanyika kwa pambano hilo.

Nao wadhamini wa pambano hilo, Kampuni ya Euromax kupitia kwa Ofisa Masoko wake, Forgiver Tito, aliwaahidi wapenzi wa ngumi kuwa wataendelea kusaidia kukuza mchezo huo kwani ni sehemu ya ajira na kuwataka wadhamini wengine kujitokeza.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 36 | 29 | 4 | 3 | 76 | 14 | 91 |
| 2. Yanga | 36 | 26 | 5 | 5 | 55 | 25 | 83 |
| 3. Azam | 36 | 19 | 12 | 5 | 50 | 21 | 69 |
| 4. Kinondoni MC | 37 | 12 | 16 | 9 | 38 | 25 | 52 |
| 5. Mtibwa Sugar | 36 | 14 | 7 | 15 | 36 | 32 | 49 |
| 6. Lipuli | 36 | 12 | 12 | 12 | 30 | 36 | 48 |
| 7. Mbeya City | 36 | 13 | 8 | 15 | 38 | 38 | 47 |
| 8. Ndanda | 36 | 12 | 11 | 13 | 23 | 33 | 47 |
| 9. Singida United | 37 | 11 | 12 | 14 | 30 | 39 | 45 |
| 10. Stand United | 36 | 12 | 8 | 16 | 36 | 45 | 44 |
| 11. Alliance | 36 | 11 | 11 | 14 | 30 | 39 | 44 |
| 12. Coastal Union | 36 | 10 | 14 | 12 | 31 | 42 | 44 |
| 13. Mbao | 37 | 11 | 11 | 15 | 26 | 40 | 44 |
| 14. TZ Prisons | 36 | 10 | 13 | 13 | 27 | 29 | 43 |
| 15. Biashara United | 36 | 11 | 10 | 15 | 29 | 34 | 43 |
| 16. Kagera Sugar | 36 | 10 | 13 | 13 | 32 | 40 | 43 |
| 17. Ruvu Shooting | 37 | 10 | 12 | 15 | 34 | 43 | 42 |
| 18. JKT Tanzania | 36 | 9 | 14 | 13 | 24 | 34 | 41 |
| 19. Mwadui | 36 | 10 | 8 | 18 | 41 | 51 | 38 |
| 20. African Lyon | 36 | 4 | 11 | 21 | 23 | 49 | 23 |

# YANGA: IRINGA NGOME NGUMU KWETU 2018/19

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI msimu wa Ligi Kuu Bara 2018/19 ukielekea ukingoni, Klabu ya Yanga imeutaja mkoa wa Iringa kuwa ni ngome ngumu kwao na watajipanga kuhakikisha mwakani hawapati tena matokeo mabaya.

**Yanga ilipoteza mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Lipuli FC na pia ikakubali kufungwa na wenyeji hao katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA.**

Akizungumza na Nipashe jana, Mratibu wa Yanga, Hafidh Saleh, alisema kuwa msimu huu wamekutana na changamoto mbalimbali, lakini bado wataikumbuka Lipuli FC kwamba ni klabu iliyowasumbua sana.

Saleh alisema pia changamoto nyingine waliyokutana nayo msimu huu unaoelekea mwishoni ni suala la fedha za uendeshaji na hili lilikuwa ni tatizo la klabu nyingi zilizoshiriki ligi hiyo yenye timu 20 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

"Tunashukuru hadi hapa tulipofika, mambo hayakuwa rahisi sana, lakini tulijitahidi kupambana kusaka ushindi katika kila mechi tuliyocheza, changamoto ni sehemu ya mpira, lakini mkoa wa Iringa haukuwa mwepesi kwetu, wametufunga katika ligi na kututoa kwenye FA, ni matokeo mabaya sana, hatukuyatarajia," alisema kiongozi huyo.

Aliwashukuru mashabiki na wanachama wa timu hiyo kwa kuwachangia fedha na michango yao iliyosaidia katika kuwafikisha hapa walipo ambapo ni nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kila mwaka.

Yanga inaendelea na mazoezi yake chini ya Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera, na leo itashuka Uwanja wa Uhuru kuwakaribisha Mbeya City kutoka jijini Mbeya.

Baada ya mchezo huo, Yanga wataendelea kujiimarisha na kujipanga vema ili kuwavaa mabingwa wa Kombe la Kagame, Azam FC katika mechi ya mwisho wa msimu itakayochezwa Jumanne ijayo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

Mechi hiyo itakuwa ni ya kusaka heshima kwa kila upande baada ya klabu hizo mbili kupoteza matumaini ya kutwaa ubingwa wa msimu huu.

## SEVILLA PIPANI...



Wachezaji wa Sevilla ya Hispania wakiwa kwenye ndege kabla ya kuondoka nchini humo kuja Tanzania kwa ajili ya mechi ya kirafiki dhidi ya Simba iliyoandaliwa na Kampuni ya SportPesa kwa kushirikiana na La Liga. Wachezaji waliowasili jana ni Vaclik, Juan Soriano, Sergi Gomez, Kjaer, Gnagnon, Jesus Navas, Aleix Vidal, Escudero, Arana, Amadou, Roque Mesa, Banega, Franco Vazquez, Nolito, Promes, Bryan Ben na Yeddery Munir. **PICHA: SPORTPESA**

# *Sita wajitosa kuwania urais ZFF*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

JUMLA ya wanamichezo 17 wamejitokeza kuwania nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), utakaofanyika Juni 2, mwaka huu huku sita miongoni mwa hao wakijitosa kuwania kiti cha urais.

Kati ya waliochukua fomu hizo, wagombea wanne wanawania nafasi ya makamu wa rais huku saba wakiwania ujumbe kutokea kila mkoa.

Katibu wa Kamati ya Uchaguzi, Omar Makungu, akizungumza na gazeti hili jana alisema mchakato wa uchukuaji na urejeshaji wa fomu hizo ulimalizika juzi Mei 20 na jana walitarajia kuanza usaili kwa upande wa wagombea wa Pemba, huku Unguja usaili ukitarajiwa kufanyika leo.

Katika nafasi za urais waliojitokeza kuchukuwa fomu ni Khamis Abdalla Said, Suleiman Mahmoud Jabir, Ame Abdalla Dunia, Haji Ali Salum, Seif Kombo Pandu na Abrahman Mohammed Hassan.

Wanaowania umakamu wa rais, alisema kuwa wawili wameombea Pemba ambao ni Salum Ubwa Nassor na Nassor Ali Abdallah na Unguja Ni Khamis Shaali Choum na Hussein Ahmada Vuai.


Aidha, aliwataja wagombea walioomba nafasi ya ujumbe kuwa ni Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja wameomba wawili ambao ni Suleiman Haji Hassan na Faina Idarous Faina, Kaskazini Unguja kumejitokeza wagombea wawili ambao ni Seif Bausi Nassor na Rashid Tamimu Khalfan.

Mikoa iliyobakia kumejitokeza mgombea mmoja ambapo mkoa wa Kusini Unguja Ni Salum Ali Haji, Kusini Pemba ni Seif Mohammed Seif na mkoa wa Kaskazini Pemba ni Omar Ahmed Awadhi.

# Michezo

Jumatano Mei 22, 2019

Nipashe



Pogba, Hazard, Mbappe ndani Real, Bale, Isco nje UK.30

MABINGWA...



Wachezaji wa Simba wakishangilia kwa staili yao ya mabingwa, wakati walipoichapa Ndanda FC mabao 2-0 katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam Jumapili. **PICHA: MTANDAO**

## Fei Toto sasa anukia Azam

**Na Mwandishi Wetu**

MAWINDONI! Ili kujiimarisha na msimu ujao, mabingwa wa Kombe la Kagame, Azam FC wanatarajia kuvunja benki yao katika kufanikisha mchakato wa kumsajili kiungo nyota wa Yanga, Mzanzibar Feisal Salum 'Fei Toto', imefahamika.

Hata hivyo, Fei Toto ambaye anatajwa kuwa kwenye mchakato wa kwenda kufanya majaribio katika klabu ya Ligi Daraja la Pili England, bado ana mkataba na Yanga ambao unatarajiwa kumalizika ifikapo Juni mwakani.

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam zinaeleza kuwa Azam FC inataka kuboresha kikosi chake cha msimu ujao na iko tayari kutumia kiasi kikubwa cha fedha ili kukamilisha malengo yake.

Chanzo chetu kinasema kwamba Fei Toto ni mmoja wa wachezaji ambao benchi la ufundi limempendekeza na matajiri hao wanataka kuifanya Azam FC kuwa na makali yake kama zamani.

"Hatutaki kurudia makosa, bosi amesema yuko tayari kuvunja mkataba wa Fei Toto na mchezaji mwingine ambaye wanaamini atawasaidia kuimarisha kikosi chake, tunataka msimu ujao tuwe na timu yenye ushindani, hata Manula (Aishi) na Bocco (John) wakikubali kurudi tutawarejesha nyumbani," kilisema chanzo chetu.

Azam FC msimu huu iliondoka mapema katika mbio za kusaka ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kutopata matokeo mazuri katika mechi zake mbalimbali, lakini imefanikiwa kutinga hatua ya fainali ya mashindano ya Kombe la FA ambapo watacheza fainali dhidi ya Lipuli FC ya mkoani Iringa.

# SIMBA BINGWA ALIYESTAHILI

**Na Adam Fungamwango**

## ● ● ● Aussems aogeshwa uwanjani, sherehe Singida hadi Dar wakiiwahi Sevilla Taifa kesho huku...

HATIMAYE Simba imefanikiwa kutetea ubingwa wake wa Ligi Kuu Bara, huku ikiweka rekodi ya kulitwaa taji hilo ikiwa ardhi ya Singida kwa mara ya pili mfululizo.

Ilikuwa ni shangwe, nderemo, hoi hoi na furaha kwenye Uwanja wa Namfua mjini Singida jana kwa wanachama, wapenzi, mashabiki, viongozi, wachezaji na makocha wa Klabu ya Simba, baada ya kufanikiwa kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara, ilipoichapa Singida United mabao 2-0 huku Kocha Mkuu, Patrick Aussems akiogeshwa kwa maji na wachezaji wake kwa furaha ya ubingwa.

**Huu unakuwa ni ubingwa wa 20 kwa Simba na kuendelea kuwa timu ya pili kutwaa ubingwa mara nyingi, nyuma ya Yanga ambayo imeutwaa mara 27.**

Simba ambayo tangu kuanza kwa msimu huu ilionekana kustahili ubingwa huo kutokana na usajili makini iliyoufanya na hatimaye kuonyesha kiwango mwanzo mwisho, ilikuwa ikihitaji pointi mbili tu kuweza kufikisha alama 90 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote ile, lakini kwa ushindi huo imefikisha jumla ya pointi 91.

Mabao kupitia kwa Meddie Kagere aliyetupia la 23 msimu huu na lile la kipindi cha pili la nahodha John Bocco (la 16 kwake), yalitosha kuihakikishia Simba inatwaa ubingwa huo msimu huu huku ikiwa na mechi mbili mkononi kufuatia kufikisha pointi 91 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote katika msimamo wa ligi hiyo inayotarajiwa kumalizika Mei 28, mwaka huu ikishirikisha timu 20.

Simba ambayo msimu uliopita ilitwaa ubingwa huo katika Uwanja wa Namfua baada ya kushinda mechi yake ya mwisho dhidi ya Singida United, sasa inarejea jijini Dar es Salaam kushuka Uwanja wa Taifa kesho kuivaa Sevilla ya Hispania kwenye mechi ya kirafiki iliyoandaliwa na wadhamini wao Kampuni ya SportPesa kwa kushirikiana na La Liga.

Kagere alifunga bao hilo dakika ya tisa tu ya mchezo, baada ya kutokea kizaazaa kwenye lango la Singida United. Shambulizi hilo lilikuwa ni la kujibu lile la dakika ya nne wakati Boniface Maganga aliukuta mpira uliokosewa na Nicolaus Gyan na kupiga suti lililotoka pembeni kidogo mwa goli.

Baada ya bao hilo kulikuwa na kosakosa za hapa na pale hadi zilipomalizika dakika 45 za kipindi cha kwanza. Kipindi cha pili kilipoanza, Singida walifanya mashambulizi mawili hatari ambayo nusura yawapatie bao, lakini washambuliaji wao kina Habib Kyombo na Geofrey Mwashiuya waliponasa mpira hawakuwa makini.

Huku Uwanja wa Namfua ukiwa umefurika mashabiki, Simba ilifanikiwa kupata bao la pili lililofungwa kwa kichwa na Bocco.

Bocco alifunga bao hilo dakika ya 61 wakati kipa wa Singida, Said Lubawa akiwa nje ya uwanja baada ya kushindwa kurejea kwa kuumia. Kipa huyo aliufuata mpira aliorudishiwa na beki wake ulioonekana kama unataka kutoka na kuwa kona, aliukimbilia na kuupiga nje, lakini mwenyewe pia akiutoa nje.

Kilichofanyika kwa wachezaji wa Simba, ulirushwa mpira kwa Emmanuel Okwi ambaye alipiga krosi haraka, huku golini kukiwa na mabeki wa Singida na Bocco aliruka juu na kuukwamisha wavuni kwa kichwa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >